# SURA YA 352

# SHERIA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

[SHERIA KUU]

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Kichwa cha Habari*

SEHEMU YA I

VIFUNGU VYA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria na Matumizi
2. Tafsiri.

SEHEMU YA II
MAMLAKA YA MAHAKAMA KATIKA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

3. Mamlaka ya Mahakama Kuu katika uthibitisho wa wosia na usimamizi wa mirathi.
4. Mamlaka ya Mahakama Kuu katika kusajili mirathi.
5. Mamlaka ya mteule wa Wilaya.
6. Mamlaka ya Mahakama za Wilaya.
7. Afisa wa ubalozi.
8. Madaraka chini ya Sheria hii yanaweza kwa usiri.
9. Kanuni za uthibitisho wa wosia.

SEHEMU YA III
ULINZI WA MIRATHI KABLA YA IDHINI YA KUIGAWA NA WASII WAKUJITIA.

10. Mpokeaji kabla ya kutolewa kwa idhini.
11. Kuuza kwa amri ya Mahakama.
12. Matumizi ya kanuni kwa wapokeaji mirathi.
13. Adhabu kwa kudharau Mahakama.
14. Hakuna mashtaka dhidi ya mpokeaji mirathi.
15. Haki tangulifu ya mpokeaji
16. Wasii wakujitia.
17. Uwajibikaji wa wasii aliyejiteua.

SEHEMU YA IV

KUKANA KWA WASIMAMIZI WA MIRATHI.

18. Kanusho la dhahiri la haki ya uthibitisho wa wosia.
19. Dondoo na kukataa kwa vitendo.
20. Madhara ya kukana.

SEHEMU YA V

UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI.

*A. Jumla*

21. Mashirika ya amana
22. Idadi ya wasii na wasimamizi
23. Watoto na watu wasio na akili nzuri

*B. UTHIBITISHO WA MIRATHI*

24. Utoaji wa uthibitisho wa wosia
25. Uthibitisho wa wosia kwa kutumia nakala, hawala, au maandishi ya wosia ulioandikwa au maandishi ya wosia wa mdomo
26. Kibadilisho cha Wosia inachoonekana baada ya mirathi kuthibitishwaa
27. Nakala ya wosia iliyothibitishwa nchi za nje
28. Madhara ya uthibitisho wa wosia

*C. Hati za usimamizi zilizoambatanishwa na wosia*

29. Ushindwa kwa wasii
30. Wakala wa wasii ambaye hayupo
31. Wakala wa mtu anayetakiwa kupewa hati za usimamizi
32. Kibadilisho wosia kinachopatikana baada ya hati za usimamizi kutolewa

*D. Hati ya usimimizi kwa mtu aliyefariki bila kuacha wosia*

33. Hati ya usimimizi kwa mtu aliyefariki bila kuacha wosia
34. Wakala wa mtu anaetakiwa kupewa usimamizi

*E. Hati za usimamizi kwa dhumuni maalumu*

35. Mpaka wosia upatikane
36. Wakati wa utoto
37. Wakati akili siyo nzuri
38. Kusubiri utowaji wa usimamizi
39. Kukusanya na kutunza mali
40. Mashtaka
41. Mali iliyochini ya amana

*F. Utoaji kwa kiasi*

42. Utoaji wa kiasi
43. Utoaji kwa kiasi kilichobaki

*G. Madhara ya utolewaji wa hati za usimamizi*

44. Madhara ya utolewaji wa hati za usimamizi

*H. Kifo cha wasii au wasimamizi na kuisha kwa muda katika utolewaji wenye kikomo*

45. Kifo cha mmoja kati wa wawakilishi
46. Kifo cha mwakilishi mmoja au mwakilishi aliyebakia
47. Kuisha kwa muda wa utolewaji wenye kikomo

SEHEMU YA VI
KUBATILISHWA NA KUBADILISHA TOLEO NA UONDOAJI WA WASII AU WASIMAMIZI

48. Kubadilisha makosa
49. Kubatilishwa kwa toleo na uondoaji wa wasii
50. Malipo ya wasii au msimamizi aliyebatilishwa
51. Kurudishwa kwa toleo lililobatilishwa

SEHEMU YA VII
MAZOEA NA MUONGOZO KATIKA UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI (TOFAUTI NA ZILE ZA MALI CHACHE)

52. Mwenendo mahakamani.
53. Ombi kwa Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya.
54. Mteule wa wilaya kusimamisha mwenendo wa kesi na kuipa taarifa Mahakama Kuu katika hali itakayojitokeza
55. Uombaji wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na na wosia
56. Maombi ya hati za usimamizi
57. Uthibitisho wa maombi
58. Pingamizi dhidi ya utoaji wa uthibitisho wa mirathi au usimamizi
59. Mwenendo wa kesi bayana ya pingamizi
60. Amri ya kutoa vidhibiti vya wosia
61. Mahakama inaweza ikamtafiti muombaji, kuhitaji ushahidi mwingine au kutoa wito
62. Muda kabla utolewaji wa usimamizi wa mirathi haujafanywa

63. Utoaji wa uthibitisho wa mirathi na usimamizi
64. Kukataliwa kwa hati za usimamizi wa mirathi
65. Maelekezo kwa wasii au msimamizi
66. Kiapo
67. Udhamini wa usimamizi
68. Utoaji wa masharti/hati ya usimamizi wa mirathi
69. Kutunzwa kwa wasii halisi
70. Uhalali wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi
71. Mpewaji pekee kuwa mwakilishi
72. Rufaa na mapitio

SEHEMU YA VIII
A. MAZOEA NA MAELEKEZO YA UCHAGUZI, NA UBATILISHAJI WA UCHAGUZI WA, WASIMAMIZI WA MALI CHACHE

73. Kutumika kwa Sehemu ya VIII
74. Uchaguzi wa wasimamizi
75. Usimamizi wa Kabidhi-Wasii na uchaguzi wa afisa wa mahakama au mtu muadilifu
76. Uchaguzi uthibitishwe muhuri wa moto
77. Dhamana ya usimamizi
78. Wosia
79. Uchaguzi unaweza kuwa kwa mali yote au baadhi ya mali
80. Athari za kuchaguliwa
81. Mali ambazo hazijadaiwa
82. Kupingwa kwa uchaguzi
83. Rufaa katika Mahakama Kuu
84. Mahakama za wilaya kupeleka taarifa Mahakama Kuu
85. Vizuizi katika utoaji wa uthibisho wa mirathi na hati za usimamizi wa mali chache.
86. Uhalali wa uchaguzi kuhusiana na mali inayozidi shilingi elfu kumi.
87. Usimamizi wa mirathi iliyo chini ya shilingi elfu moja

B. USIMAMIZI WA MALI CHACHE

88. Sheria inayotumika kwa mtu wa kabila fulani
89. Wosia wa mtu wa kabila fulani
90.-91. (Imefutwa)

SEHEMU YA IX
MALI ZINAZOSIMAMIWA KUTOKANA NA SHERIA ZA KIJADI, MILA NA SHERIA ZA KIISLAM.

92. Vipengele ambapo Sheria hii itatumika katika mali inayosimamiwa kwa kutumia sheria za kijadi pamoja na mila.
93. Athari za maelekezo ya Mahakama Kuu katika amri zilizowekwa na Mahakama ya Mwanzo.

SEHEMU YA X
USAJILI WA UTHIBITISHO WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI

94. Tafsiri
95. Usajili wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi iliyotolewa nje ya Tanzania
96. Vigezo vinavyotakiwa kabla ya kusajili mirathi
97. Dhamana
98. Madurufu na nakala

SEHEMU YA XI
MAMLAKA NA MAJUKUMU YA WASII NA WASIMAMIZI

99. Asili na mali ya wasii au msimamizi
100. Mamlaka kuhusiana na mshitaka na madeni
101. Mamlaka ya kuuza vitu
102. Matumizi kwa ajili ya uangalizi na usimamizi
103. Wasii au wasimamizi kutochukua faida yoyote kutoka kwenye mali
104. Mamlaka ya wasii au wasimamizi yanawezwa kufanywa na mmoja wao.
105. Mamlaka ya wawakilishi mahususi
106. Malipo ya gharama za msiba.
107. Orodha na mahesabu
108. Kazi za ujumla za usimamizi
109. Namna ya kulipa madeni
110. Madeni yalipwe kabla ya wausiwa
111. Kupungua kwa hiba ya wazi na usawa wa wausiwa
112. Kupungua kwa hiba mahsusi
113. Haki ya hiba maalum

SEHEMU YA XII
HIBA NA MALIPO YA MWAKA

114. Ridhaa inahitajika kwa muusiwa kupata mali yake
115. Ridhaa kwa hiba mahususi
116. Ridhaa ya wasii katika mali yake mwenyewe
117. Madhara ya ridhaa ya wasii
118. Kuanza kwa malipo ya mwaka kama muda haujawekwa katika wosia
119. Malipo ya malipo ya mwaka kama muda umewekwa
120. Vifungu vya ujumla kuhusiana na malipo ya mwaka
121. Uwekezaji katika amana inayoruhusiwa na Kanuni za Uthibitisho wa Wosia

122. Urithi unaotegemea jambo fulani
123. Maelekezo ya mtoa wosia katika uwekezaji
124. Watoto wanatakiwa wapate malipo au umiliki mara moja
125. Utolewaji wa hiba
126. Riba katika hiba ya wazi
127. Riba katika malipo ya mwaka
128. Baki ilipwe kwa muusiwa wa mali itakayobaki
129. Kuhamisha kwa mali kutoka Tanzania kwa wasii au msimamizi aliyepo katika nchi aliyokuwa akiishi marehemu

SEHEMU YA XIII
URUDISHAJI WA MALI KWA WAUSIWA

130. Urudishaji kama hiba imelipwa chini ya agizo la Mahakama
131. Hakuna urudishaji kama malipo yamefanywa kwa hiari
132. Urudishaji wa mali kama hiba imefikia muda wake baada ya sharti kutimizwa na muda kuongezwa
133. Pale wausiwa watakapotakiwa warudishe kwa usawa
134. Ugawaji wa mali
135. Pale mdai atakapomtaka wasii arudishe mali
136. Haki ya muusiwa kuwataka wausiwa wengine warudishe mali
137. Urudishwaji hautakuwa na riba

SEHEMU YA XIV
UFUJAJI WA MALI

138. Hatia itokanayo na ufujaji
139. Hatia ya kutojali

SEHEMU YA XV
USIMAMIZI WA MALI YA WAKFU

140. Tafsiri
141. Wakfu utakuwa wa halali
142. Uanzishwaji wa Tume ya Wakfu
143. Tume ya Wakfu kuwa mamlaka inayojitegemea na itakuwa na muhuri wa moto
144. Mikutano na kiwango/koramu
145. Usajili wa mali ya wakfu na amana
146. Tume ya Wakfu itafanya uchunguzi kuchukua usimamizi wa wakfu
147. Wadhamini wa wakfu wanaweza kuitwa kuleta uthibitisho wa usimamizi mzuri wa amana zao
148. Mikataba na makubaliano fulani yanayohusiana na mali ya wakfu ni lazima yathibitishwa na Tume ya Wakfu
149. Mali za wakfu hazitamilikiwa kwa maagizo au kwa kabidhi pingamizi baada ya kuanzishwa kwa sehemu hili
150. Jinsi ya kusimamia mali ya wakfu

151. Tume ya Wakfu inaweza ikauza mali ya wakfu katika mazingira fulani
152. Ruhusa inahitajika kujenga msikiti au kuanzisha makaburi
153. Ada
154. Ukaguzi wa mahesabu
155. Akaunti za benki
156. Sheria ya Usimamiaji wa Kodi haitatumika katika mali za wakfu
157. Adhabu
158. Kanuni

SEHEMU YA XVI
MALIPO YA KIISLAM (TUNU AU SADAKA)

159. Upendeleo wa afisa wa wilaya kufanya malipo

SEHEMU YA XVII
MENGINEYO

160. Vifungu vinavyomuhusu msimamizi aliyeambatanishiwa wosia
161. Uhifadhi wa wosia wa watu walio hai
162. Hati ya kiapo kama ni shirika la amana
163. Uhalali wa ugawaji wa mali kama haki ya matunzo imewekwa
164. Madadiliko ya sheria kadhaa
165. Sheria fulani kutotumika
166. Bakizo
167. Vifungu vya mpito
168. Bakizo la mamlaka ya Kabidhi- Wasii na muamana wa serikali

---

MAJEDWALI

SURA YA 352

SHERIA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

**Sheria inayoelezea utolewaji wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi, inaweka vifungu kuhusiana na mamlaka na kazi za wasii au wasimamizi wa mirathi; usimamizi wa mali iliyowekwa wakfu; malipo kwa ajili ya kukirimu au sadaka kwa mali za kiislamu, na masuala yanayohusiana na hayo.**

[1, Machi, 1963]

(Sura ya 445)
(Sura ya 29)
(Sura ya 30)
(Sura ya 326)

Sheria Namba
9 ya1963
55 ya 1963
33 ya 1964
9 ya 1965
41 ya 1966
18 ya 1970
23 ya1971
3 ya1979
12 ya 1979
10 ya1987

SEHEMU YA I

MASHARTI YA MWANZO

Jina la Sheria na atumizi

**1**.-(1) Sheria hii itaitwa Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi.

(2) Sambamba na kifungu cha 87 na Sehemu ya IX, Sheria hii itatumika katika usimamizi wa mirathi wa watu wote waliokufa huku wakiwa wakazi, au wameacha vitu, ndani ya Tanzania iwe kabla au baada ya tarehe ambayo Sheria hii itanza kutumika

Tafsiri

**2**.-(1) Katika Sehemu hi i, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"msimamizi" maana yake ni mtu ambaye amechaguliwa na

mahakama kusimamia mali ya marehemu ambapo hakukuwa na wasii, au hakuna wasii aliye tayari kufanya jukumu hilo, itajumuisha, pale Sehemu ya VIII itakapohusika na itategemeana na vifungu hivyo, mtu anayechaguliwa kuwa msimamizi katika Sehemu hiyo ;

"kibadilisho cha Wosia" maana yake ni hati inayohusiana na Wosia, na inaelezea, badilisha au inaongeza kitu katika ugawaji wa mali;

"shauri mbishano" inapohusishwa na utoaji wa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi maana yake ni kujitokeza kwa mtu kupinga muombaji asipewe usimamizi wa mirathi;

"mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu, na katika hali ambayo mteule wa wilaya ana mamlaka, mteule wa wilaya, lakini haihusishi mahakama ya wilaya;

"hiba maalumu" maana yake ni hiba iliyoelekezwa kulipwa katika mali mahususi;

Sura ya 11 "mahakama ya wilaya" maana yake ni mahakama chini ya Sheria ya Mahakama ya Mahakimu ;

"hakimu mteuliwa" maana yake ni hakimu mkazi aliyechagulia kukaimu wilaya katika kifungu cha 5;

"Wasii" ni mtu aliyechagualia na mtoa wosia asimamie mali zake atakapokua amefariki;

"hiba ya jumla" maana yake ni hiba yoyote isiyo hiba mahususi au maalumu;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya kisheria;

"uthibitisho wa Wosia" maana yake ni nakala ya wosia, au katika wosia wa mdomo, maelezo ya mdomo ya wosia huo, yaliyothibitishwa ma muhuri wa mahakama, inayotoa usimamizi wa mali za mtoa wosia;

"kanuni za uthibitisho wa Wosia" maana yake ni kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu cha 9;

Sura ya 358
Sura ya 33

"kanuni za mahakama" zinajumuisha kanuni zilizotengenezwa na Mahakama Kuu katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria na kanuni zilizomo au zilizotengenezwa na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai;

"mali chache" ni mali ambayo mahakama, mahakama ya wilaya iliyo na mamlaka katika uthibitisho wa wosia au usimamizi, imejirizisha kuwa haizidi shilingi elfu kumi ;
"hiba mahususi" maana yake ni hiba ya kitu kilichotajwa ;

"shirika la amana" maana yake ni-

(a) Muamana wa Serikali; au
(b) Kabidhi Wasii; au

benki yoyote au bima au mdhamini au kampuni ya amana ambayo in mtaji ( katika mali na hisa) isiyopungua paundi laki mbili na nusu wakati inatolewa, ambapo si chini ya paundi laki moja zimelipwa kwa pesa taslimu; au

(c) shirika lolote ambalo lina mtaji (katika mali na hisa) isiyopungua paundi laki mbili na elfu hamsini wakati wa kutolewa, ambapo si chini ya paundi laki moja zimelipwa kwa pesa taslimu, na kwa muda huo zimewezeshwa ( na sheria ya Bunge ya jamuhuri ya muungano, katiba ya kampuni, hati ya makubaliano au kitu kingine kinachohusiana na hiyo au kinachotoa mamlaka) ya kuchukua amana, lakini kwa muda mrefu kampuni hiyo haita, kwa mwaliko wa kampuni, mwongozo, tangazo au kwa nyaraka iliyotolewa na au kwa niaba ya, inasema au kutaja kuwa tuhuma zozote zinazoihusisha muamana wa serikali au mapato ya jumla ya jamuhuri wa muungano kuhusiana na kitendo au kutotendeka kwa jambo fulani katika kampuni hiyo wakati inatumikia kama wasii au msimamizi; na

"Wosia" maana yake ni tamko la kisheria la nia ya mtoa wosia kulingana na mali zake, na jinsi anavyotaka zitumike baada ya kifo chake;

(2) Bila kujali kitu chochote katika maana ya "shirika la amana" katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kampuni ambayo inaweza kuwa ni shirika la amana lakini kwa maana kuwa haijakidhi mahitaji yanayohusiana na mtaji katika aya ya (c) na (d) ya kifungu hicho linaweza likawa wasii au msimamizi katika hali yoyote kama Mahakama Kuu itakavyoamua, na hivyo kwa dhumuni la kuwa wasii au msimamizi litasemekana kuwa na mamlaka, haki na majukumu ya shirika la amana katika Sheria hii

SEHEMU YA II

MAMLAKA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MALI

Mamlaka ya Mahakama Kuu katika uthibitisho wa wosia na usimamizi

**3.** Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka katika masuala yopte yanayohusu usimamizi wa mirathi,ambapo itakuwa na mamlaka ya kugawa mirathi inayotokana na wosia,na ile ya

hati za usimamizi wa mirathi ya marehemu,na pia kurekebisha au kutengua mirathi hiyo.

Mamlaka ya Mahakama Kuu kusajili mirathi fulani

**4.** Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusajili mirathi na hati za usimamizi wa mirathi uliofanywa na Mahakama zenye uwezo wa kusimamia mambo ya mirathi zilizopo katika nchi zilizokuwa koloni la Uingereza kwa mujibu wa Sehemu ya Kumi ya Sheria hii.

Mamlaka ya mteule wa wilaya

**5**.-(1) Katika nyakati tofauti tofauti Jaji Mkuu anaweza kuchagua mahakimu wa Mahakama za Wilaya kusilikiza mashauri ya mirathi kama mahakimu wateule

(2) Mahakimu wateule watakuwa na mamlaka katika mashauri yote yahusuyo mirathi na usimamizi wa mirathi huku wakiwa na malaka ya kuteua msimamizi wa mirathi na kutoa hati za usimamizi wa mirathi ikiwa kama marehemu, katika kipindi cha kifo chake alikuwa akiishi katika eneo ambalo hakimu huyo alichaguliwa-

(a)katika mirathi isiyo bishaniwa;

(b)atika mirathi inayobishaniwa,ila tu kama hakimu atajiridhisha kwamba thamani ya mirathi hiyo haizidi shilingi elfu kumi na tano, au iwapo Mahakama Kuu ikiamuru Hakimu kutekeleza mamlaka yake katika mazingira yanayoonyeshwa katika kifungu kidogocha(3)

(3) Hakuna kitendo cha mteule wa wilaya katika ufanyaji wa majukumu yake katika uthibitisho wa wosia na usimamizi wa mali kitakuwa batili kwa sababu ya kwamba imegundulika kuwa mali inazidi shilingi elfu kumi na tano, lakini hakimu huyo akilijua hilo katika mirathi inayobishaniwa, atatoa ripoti ya suala hilo katika Mahakama Kuu ambayo aidha itaagiza mwenendo wa shitaka uamishiwe kwake au itamruhusu mteule kuwa na mamlaka na suala hilo

(4) Hakimu mteuliwa hatokuwa na uwezo wa kushughulika na mamlaka ambayo bayana yamekewa kwa Mahakama Kuu

Mamlaka ya Mahakama za wilaya

**6**.- Mahakama ya Wilaya inayoongozwa na Hakimu wa Wilaya itakuwa na mamlaka katika usimamizi wa mirathi midogo, wakiwa na nguvu ya kuchagua msimamizi wa mirathi hizo ndogo, pale ambapo marehemu amefia katika sehemu ambayo Mahakama ina mamlaka kwa kutumia mfumo unaoonyeshwa katika jedwali la nne katika Sheria hii.

Afisa wa ubalozi

**7**.-(1) Ikiwa mtu ambaye ni raia wa nchi ambayo kifungu hiki kinatumika amechaguliwa kuwa wasii katika wosia wa marehemu aliyegawa mali zake Tanzania, au ni mtu ambaye anaweza akapewa usimamizi wa mali ndani ya Tanzania, mahakama kama itajiridhisha,

kufuatana na maombi ya afisa wa ubalozi wa nchi hiyo, ya kuwa mtu huyo sio mkazi wa Tanzania, na kama hakuna maombi ya usimamizi yaliyofanywa na wakala aliyeruhusiwa na hati haki ya uwakala kwa niaba yake, mahakama itampa afisa huyo usimamizi wa mali za marehemu kama ambavyo angepewa kama angekuwa amechaguliwa kama ilivyosemwa

(2) Hati inayotolewa kwa afisa wa ubalozi itapewa kwake kwa jina la ofisi na sio yeye binafsi, lakini mtu aliyepo katika ofisi hiyo atakula kiapo yeye mwenyewe binafsi. Hati hizo za usimamizi wa mali zitawekwa kutoka kwa afisa wa ubalozi kwa afisa mwingine atakaemrithi, na zitakuwa katika afisa huyo wa ubalozi kwa muda wote atakapokuwa ofisini pasipo kuwa na agizo la mahakama, au uhamishaji, au ugawaji au hati nyingine yoyote.

(3) Wadhamini hawatahitajika ikiwa kama usimamizi umepewa kwa afisa wa ubalozi katika kifungu hiki.

(4) Mtu yeyote ambaye ni raia wa nchi ambayo kifungu huki kinatumika-

(a) anastahili kupata pesa yoyote au kitu kingine Tanzania, ambacho ni moja kati ya mali za marehemu, au kupokea malipo Tanzania, ya pesa yoyote yaliyotimia kulipwa wakati wa kifo cha marehemu; au
(b) ni mmoja wa watu ambao pesa au kitu chochote cha marehemu, chini ya Sheria hii, kinaweza kulipwa bila ya hati ya uthibitisho wa wosia au uthibitisho wowote, kama ikiwa mtu huyo; sio raia wa Tanzania , afisa ubalozi wa nchi hiyo atakuwa na mamlaka ya kupokea au kutoa malipo halali ya pesa yoyote au mali yoyote kana kwamba ameruhusiwa na wakala aliyethibitishwa na hati ya uwakala afanye kwa niaba yake:

Isipokuwa kwamba hakuna mtu atakayeruhusiwa au kutakiwa na kifungu hiki kidogo kulipa au kupeleka pesa au mali kwa afisa ubalozi kama anajua kuwa kuna mtu alimeruhusiwa kupokea pesa au mali hiyo kwa niaba ya raia huyo

(5) Bila kuzingatia kifungu chochote kinachotoa ulinzi au upendeleo kuhusiana na vitendo vya kiofisi na nyaraka za afisa ubalozi, afisa ubalozi hatakuwa na ulinzi au upendeleo kuhusiana na kitendo alichofanya chini ya mamlaka yaliyowekwa kwake na kifungu hiki, au kuhusiana na nyaraka zozote zilizopo chini yake kwa muda huo.

(6) Kifungu hiki kinatumika kwa nchi zinazoonyeshwa katika Jedwali la kwanza,kupitia gazeti la serikali Waziri anaweza kuongeza au kupunguza nchi nyingine yeyote ya kigeni kutoka katika Jedwali la kwanza

Mamlaka katika Sheria hii yanaweza kufanywa sirini

8.Sambamba na kanuni zozote za uthibitisho wa mirathi, mamlaka ya mahakama au mahakama ya wilaya yanawezwa yakafanywa faraghani-

(a) katika shtaka linalobishaniwa; na

Sura ya 33

(b) katika shtaka lisilobishaniwa kwa kipomo kile kile kama vile mamlaka yakiwa yanafanywa faraghani katika dai linalofanywa kwa kulingana na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai au sheria yoyote itakayowekwa baada ya hiyo au kanuni zozote za mahakama.

Kanuni za uthibitisho wa wosia

**9**. Jaji Mkuu anaweza akaweka kanuni za uthibitisho wa mirathi kwa ajili ya kusimamia mienendo ya utolewaji wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi wa mirathi au uchaguliwaji wa msimamizi, kwa dhumuni hilo, katika Sheria hii imetolewa kuwa kanuni za uthibitishaji wa mirathi zinaweza zikatengenezwa, kwa ajili ya utunzwaji, na unakilishaji na ukaguzi wa wosia, matolea ya uthibitisho wa mirathi na usimamizi wa mali na uchaguzi wa wasimamizi, kwa ada inayojumiusha ada inayotolewa kwa wasimamizi katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 75 na fomu zake, na kwa ujumla kwa ajili ya utumiaji mzuri wa Sheria hii.

## SEHEMU YA III
## UTUNZAJI WA MALI WAKATI USIMAMIZI HAUJATOLEWA NA WASII WALIOJITIA

Mpokeaji wakati usimamizi haujatolewa

**10**. Ikiwa mtu amekufa na kuacha mali Tanzania, Mahakama inaweza, kama itaonekana kutokana na maombi ya Kabidhi Wasii au mtu yeyote mwenye masilahi na mali hiyo, au anayetunza au mwenye nguvu na mali hiyo wakati wa kifo cha marehemu, au kwa muda huyo ni wakili wa marehemu, kwamba kuna hatari kuwa mali hiyo inaweza ikapotezwa, itamchagua Kabidhi Wasii au mtu mwingine yeyote kama mahakama itakavyoona yafaa, kuwa mpokeaji wa mali hiyo huku toleo la uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi ikingojwa.

Mauzo kwa agizo la mahakama

**11**. Mahakama inaweza, kutokana na ombi litakaloombwa na mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10, au mtu yeyote mwenye maslahi na mali, kutoa amri ya kuuzwa kwa mali yote au sehemu ya mali hiyo, kama ikionekana kuwa kuuzwa kwa mali hiyo kutaifaidisha mali yote kwa ujumla.

Matumizi ya kanuni zinazohusu wapokeaji

**12**. Mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10 atatakiwa afuate miongozo yote ya mahakama inayowahusu wapokeaji kwa ujumla:

Ili mradi kwamba siyo Kabidhi Wasii wala Muamana wa Serikali atatakiwa kuweka dhamana ili kusimamia mirathi.

Adhabu kwa kidhihaki mahakama

**13**. Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka yototе, atatoa or atajaribu kutoa kutoka Tanzania sehemu yoyote ya mali ambayo

mpokeaji amechaguliwa katika kifungu cha 10, au ataharibu, au kuficha, or atakataa kutoa mali hiyo kwa mpokeaji, atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalipa fidia isiyopungua shilingi elfu tano au kwenda jela kwa muda usiopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.

Hakuna shtaka dhidi ya mpokeaji

**14.** Hakuna shtaka litaloletwa dhidi ya mpokeaji alichaguliwa katika kifungu cha 10 kutokana na suala lolote alilofanya au analotarajia kufanya linalohusu mali ya marehemu katika utekelezaji wa mamlaka aliyopewa; lakini mtu yeyote aliyeonewa na kitu chochote kilichofanywa, au kinachotarajiwa kufanywa, anaweza akaiomba mahakama muongozo kuhusu suala hilo, na mahakama itatoa amri kama inavyoona yafaa.

Haki tangulifu

**15**. Mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10 atakuwa na na haki tangulifu kwenye mali zilizokabidhiwa kwake kwa gharama na matumizi yote aliyoyafanya sawasawa katika kutimiza majukumu yake.

Wasii wa kujitia

**16**. Mtu yeyote ambaye ataingilia mali za marehemu au akafanya kitu chochote ambacho kingefanywa na ofisi wa msimamizi wa mirathi, kwa kipindi ambacho msimamizi wa mirathi hajachaguliwa, atakuwa amejiweka mwenyewe kuwa wasii aliyejitia.

Ili mradi kwamba-

(a) kuingilia vitu vya marehemu kwa lengo la kuvitunza au kugharamia gharama za mazishi au au kwa hitaji la haraka la familia au kitu; au
(b) kushughulika kwa hali ya kawaida na bidhaa za biashara za marehemu zilizopokelewa kutoka kwa mtu mwingine; au
(c) kitendo cha afisa wa utawala katika kifungu cha 14 cha Sheria ya Kabidhi-Wasii ( Majukumu na Shughuli);

Sura ya 27

(d) kitendo cha mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10, havipelekei mtu kuwa wasii aliyejiamulia

Hatia ya wasii aliyejiteua

**17**. Ikiwa mtu amekuwa wasii aliyejiteua mwenyewe, atatakiwa kujieleza kwa wasii atakae chaguliwa kihalali, au kwa mrithi au mdai wa marehemu, kulingana na mali ambazo zimepita mikononi mwake, baada ya kupunguza malipo apewayo wasii wa halali, na malipo yoyote yaliyofanya katika shughuli nzima ya usimamizi.

## SEHEMU YA IV
## KUJITOA KWA WASII

Ujitoaji dhahiri wa kuchukua usimamizi

**18.** Mtu anaetakiwa kupewa uthibitisho wa usimamizi wa Wosia anaweza kujitoa au kukataa kusimamia mirathi hiyo kwa mdomo siku ya kusikiliza kwa ombi lolote au kwa maandishi yaliyosainiwa na mtu anayejitoa yaliyoshuhudiwa mbele ya mtu ambaye kiapo kinaweza kutolewa mbele yake.

Wito na ujitoaji unaobuniwa

**19**.-(1) Mtu yeyote mwenye au anayedai kuwa na maslahi na mali ya marehemu au mdai wa marehemu anaweza kuomba wito

kwenda kwa msimamizi au wasimamizi wa mirathi waliochagulia na marehemu katika wosia wake, ili waje wakubali usimamizi huo au wajitoe katika usimamizi wa mirathi husika.

(2) Mtu yeyote aliye pokea wito huo anaweza kuhudhuria, lakini kama asipohudhuria, atachukuliwa kuwa amejitoa katika usimamaizi wa mirathi; na kama, alijitokeza, na hajaendelea kuomba uthibitisho wa usimamizi wa mirathi, mtu aliyeomba aitwe anaweza akaomba amri ya kwamba mtu aliyeitwa, isipokuwa kama ataomba na kupata uthibitisho wa usimamizi wa mirathi kwa muda utakaoamriwa, achukuliwe kuwa amejitoa katika usimamizi wa mirathi, na amri inaweza ikatolewa kama inavyopaswa.

Madhara ya kujitoa

**20.** Kujitoa katika usimamizi wa mirathi kuwe kwa maneno au kwa vitendo vinavoashiria kujitoa, hakutamruhusu mtu huyo aliyejitoa kuomba tena usimamizi wa mirathi:

Ili mradi kwamba mahakama kwa muda wowote inaweza ikamruhusu mtu aliyejitoa kufuta kujitoa kwake kwa dhumuni la kuchukua usimamizi wa mirathi, kama itaonekana kuwa ufutaji huo ni kwa faida ya mali au watu wenye masilahi na mali hiyo.

## SEHEMU YA V

## UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI NA MAHAKAMA

*A. Vifungu vya Jumla*

Kampuni ya amana

**21**.-(1) Kampuni yenye dhamana/ kampuni ya muamana

(a) inaweza kuthibitishwa usimamizi wa mirathi inayotokana na wosia wa mtu yeyote,iwapo imetajwa kama msimamizi katika wosia huo;

(b) inaweza kupewa barua ya usimamizi wa mirathi

(2) Kampuni iliyo na dhamana inaweza kuthibitishwa kama msimamizi wa mirathi au kupatiwa barua ya usimamizi wa mirathi pekee yake au pamoja na watu wengine.

(3) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi haitatolewa kwa kundi la watu au mashirika au kwa mtu aliyeteuliwa na kampuni kufanya hivyo kwa niaba yake

Idadi ya wasii na wasimamizi

**22**.-(1) Uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi haitatolewa kwa watu zaidi ya wanne kuhusiana na mali moja, na hati za usimamizi wa mirathi, kama kuna utoto, au maslahi ya maisha yanaibuka katika wosia au katika mtu kifo bila wosia, utapewa ama kwa kampuni ya muamana pekee au pamoja na mtu au si zaidi ya watu wawili:

Ili mradi kwamba katika utoaji wa hati za usimamizi wa mirathi mahakama inaweza ikajikita katika ushahidi unaoonekana, ulioletwa na muombaji au na mtu yeyote, ya kuwa kuna au hakuna utoto au maslahi ya maisha, kama itakavyoelezwa na kanuni za uthibitishaji wa

mirathi.

(2) Kama kuna mwakilishi mmoja tu (na siyo kampuni ya muamana) katika utoto wa mnufaishwaji au uwepo wa masilahi ya maisha na mpaka mali zote zimemamilizwa kusimamiwa, mahakama inaweza, kwa ombi la mtu yeyote mwenye maslahi, au mlezi, kamati au mpokeaji wa mtu yeyote kuchagua mwakilishi au wawakilishi kwa kuongezea wasimamizi waliopo, kulingana na kanuni za uthibitisho wa mirathi.

Watoto na watu wenye matatizo ya akili

**23**. Usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi hauwezi kutolewa kwa mtoto chini ya miaka kumi na nane au mtu aliye na matatizo ya akili

*B- Uthibitisho wa Wosia*

Utoaji wa uthibitisho wa wosia

**24**.-(1)Usimamizi wa mirathi unaweza kutolewa kwa msimamizi aliyetajwa katika wosia

(2)Uchaguzi unaweza ukawa wa wazi au maana inayoashiria usimamizia

(3) Pale inapotokea wamechaguliwa executors tofauti, mirathi inaweza kutolewa kwao kwa pamoja na katika wakati tofauti

(4) Ikiwa msimamizi wa mirathi akichaguliwa kwa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo fulani, basi uteuzi huo utahusisha yale mambo yaliyokusudiwa tu.

Uthibitisho wa wosia kwa kutumia nakala, hawala au maneno ya wosia wa mdomo

**25.**-(1)Pale inapotokea wosia umepotea au hauwezi kupatikana baada ya kufa kwa yule aliyeandika ,au umeharibika kimakosa,ajali na si kwa kitendo chochote cha mtoa wosia-

(a) ikiwa kama nakala ya wosia ilitunzwa, uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi unaweza kutolewa kwa kupitia nakala hiyo, mpaka pale wosia halisi au nakala ya wosia uliothibitishwa umepokelewa katika mirathi.

(b) ikiwa hakuna nakala au hawala ya wosia uliotunzwa, uthibitishwaji wa mirathi unaweza kutolewa iwapo tu kutakuwa na ushahidi wa kuthibitisha yaliyomo katika wosia, yenye ukomo katika hilo

(2) Pale ambapo wosia ulioandikwa unashikiliwa na mtu aliye nje ya nchi, na amekata au kupuuza kuwasilisha, lakini nakala yake inapatikana kwa msimamizi wa mirathi, mirathi hiyo inaweza kutolewa kwa kutumia nakala ya wosia huo kwa manufaa ya mali hiyo ya marehemu pasipo kusubiri nakala halisi.

(3) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi kuhusu wosia uliotolewa kwa mdomo utatolewa iwapo tu kutakuwa na ushahidi wa kuthibitisha yaliyopoa katika wosia

Kibadilisho cha wosia kinachopatikana baada ya uthibitisho wa wosia kutolewa

**26** .Ikiwa uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi umekwishatolewa, na kibadilisho cha wosia kikapatikana, uthibitishwaji mwingine wa usimamizi wa mirathi unaweza ukatolewa kulingana na badiliko hilo.

Ila ikiwa badiliko hilo la wosia kwa uwazi au kwa ufahamuzi linakataa uchaguzi wa msaimamizi wa mirathi ambaye amekwisha pewa mamlaka ya kusimamia mirathi, uthibithishwaji wa mirathi uliofanywa utabatilishwa na uthibishwaji wa mirathi utafanywa upya kwa wosia wa zamani na badiliko lake kwa pamoja

Nakala ya wosia iliyothibitishwa nje ya nchi

**27**. Ikiwa wosia umethibitishwa na kuhifadhiwa katika mahakama yenye mamlaka iliyoko nje ya Tanzania, lakini nakala sahihi na iliyothibitishwa ikaletwa, uthibitishwaji wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na nakala hiyo inaweza kutolewa.

Madhara ya uthibitisho wa wosia

**28.** Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi ukishatolewa huupa wosia nguvu na hushuhudia cheo cha msimamizi wa mirathi baada ya kifo cha mtoa wosia.

Kushindwa kwa wosia

**29**. Ikiwa

(a) hakuna msimamizi wa mirathi aliyechaguliwa; au

(b) msimamizi au wasimmizi wa mirathi waliochaguliwa kwenye wosia wamejitoa, au ni watu ambao hawawezi wakapewa uthibitisho wa usimamiaji wa mirathi; au

(c) wasimamizi wa mirathi waliochagulia wamefariki kabla ya mtoa wosia kufariki; au

(d) wasimamizi wa mirathi waliochagulia wamefariki kabla ya kupata uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au kabla hawajamaliza kusimamia mirathi yote ya marehemu; au

(e) wasimamizi wa mirathi waliochaguliwa hawajajitokeza kuchukua uthibitisho wa usimamizi wa mirathi;

(f) barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia inaweza ikatolewa kwa mirathi yote ambayo haijaamriwa au sehemu ya mirathi hiyo ambayo haijaamriwa kwa mtu au watu ambao mahakama itaona yafaa wao waamru mirathi hiyo.

Ila kipaumbele kitapewa kwa makundi yafuatayo na kwa muongozo huu-

(i) muusiwa wa kwanza au wa mali itakayobaki ;

(ii) mwakilishi wa marehemu au muusiwa wa kwanza au wa mali itakayobaki ;

(iii) mtu au watu, ambao wananufaika na wosia na ambao wangeweza kupewa barua ya usimamizi wa mirathi ikiwa marehemu angekufa bila kuacha wosia;

(iv) mrithi mwenye masilahi yenye faida;na

(v) mdai wa marahemu.

Ili mradi kwamba, mahakama haitatoa barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambataniswa na wosia ambao umemtaja msimamizi wa mirathi husika, na ikiwa msimamizi huyo-

(i) anaishi na mahali alipo panajulikana; na

(ii) ni mtu ambaye anaweza kupewa uthibitisho wa

usimamizi wa mirathi

(iii) hajajitoa katika ofisi ya usimamiaji mirathi:

Isipokuwa kwamba kama wito umetolewa na kumuita msimamizi wa mirathi kuja kutwaa au kujitoa kuwa msimaizi wa mirathi na msimamizi huyo amejitoa au amesajilikiwa kuwa amejitoa kama inavoonekana katika kifungu cha 18 na 19.

Wakala wa wasii asiyekuwepo

**30**. Ikiwa msimamizi wa mirathi hayupo Tanzania na hakuna mtu nadani ya nchi ambaye yupo tayari kuwa msimamizi wa mirathi, barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia itapewa kwa wakala wake aliyewekwa kisheria na anayeishi ndani ya Tanzania, kwa dhumuni lenye ukomo kwa muda ambao msimamizi huyo hayupo mpaka atakaporudi na kuchukua uthibitisho wa usimamizi wa mirathi yeye mwenyewe.

Wakala wa mtu anayestahili kupewa hati za usimamizi

**31**. Ikiwa mtu ambaye anaweza kupewa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi katika kifungu cha 29 hayupo ndani ya Tanzania, barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia itapewa kwa wakala wake aliyewekwa kisheria na anayeishi ndani ya Tanzania, kwa kwa dhumuni lenye ukomo kama inavyoelezewa katika kifungu cha 30.

Kibadilisha wosia kilicho patikana baada ya hati za usimamizi kutolewa

**32**. Kifungu cha 26 kitatumika sawa katika utolewaji wa barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia kama inavotumika katika utoaji wa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi

*D.- Hati za Usimamizi kwenye Kifo bila Wosia*

Hati za usimamizi kwa aliyefariki bila wosia

**33**.-(1) Pale marehemu anapofariki bila kuacha wosia, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikatolewa kwa mtu yeyote ambaye, kufuatana na utumikaji wa kanuni za ugawaji wa mali za mtu anapofariki bila wosia, mtu huyo atakuwa ana haki ya kupata mali yote au sehemu ya mali ya marehemu.

(2) Ikiwa mtu zaidi ya mmoja wameomba hati za usimamizi wa mirathi, itakuwa ni upendeleo wa mahakama kumpa mmoja wao au wengi wao, na katika upendeleo huo mahakama itachukulia maanani maslahi ya haraka ya mali ya marehemu kwa kuangalia mtu mwenye maslahi zaidi kuliko yule mwenye maslahi machache katika mali ya marehemu.

(3) Kama hakuna mtu aliyeomba, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikatolewa kwa mdai wa marehemu.

(4) Kama mahakama ikiona ni muhimu au inafaa kumpa mtu yeyote usimamizi wa mirathi au sehemu ya mirathi zaidi ya mtu yule ambaye kwa hali ya kawaida alitakiwa apewe usimamizi wa mirathi, mahakama kwa upendeleo wake, na kwa kutilia maanani ujamaa, masilahi, usalama wa mali na uwiano wa kuwa mali itasimamiwa vizuri, itamchagua mtu huyo kama inavyoona yafaa kuwa msimamizi; na katika kila hali hiyo hati za usimamizi inaweza ikawa yenye

kikomo au kama mahakama itakavyoona ni sawa.

Wakala wa mtu anayestahili usimamizi

**34**. Ikiwa mtu anayetakiwa achukue hati za usimamizi wa mirathi yuko nje ya Tanzania na hakuna mtu aliye tayari kubeba jukumu hilo, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikapewa kwa wakala aliewekwa kisheria, na anayeishi Tanzania, wa mtu huyo, yenye kikomo mpaka mtu huyo achukue hati za usimamizi mwenyewe na katika muda huyo kwa dhumuni lolote lenye kikomo kutokana na mamlaka aliyonayo wakala huyo.

*E.Hati za Usimamizi wa Mirathi kwa Dhumuni Maalumu.*

Mpaka wosia upatikane

**35.** Pale ambapo hakuna wosia wa marehemu,lakini kuna sababu za kuamini kwamba kuna wosia, hati za usimamizi wa mirathi inaweza kutolewa,mpaka pale wosia au nakala iliyothibitishwa itakapo tolewa.

Wakati wa utoto

**36**.-(1) Ikiwa mtoto alitakiwa, isipokuwa kwa utoto wake, kupewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi, hati ya usimamizi iliyo au isiyo ambatanishwa na wosia inaweza, sambamba na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 22, ikapewa kwa mlezi wa mtu huyo na mali ya mtoto, au kwa mtu yule kama mahakama itakavyoona yafaa, kwa ukomo mpaka mtoto atakapofikisha umri wa kuchukua usimamizi yeye mwenyewe.

(2) Ikiwa kuna wasii wawili au zaidi ambao ni watoto au watu wanaofaa kupewa usimamizi, usimamizi katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatolewa kwa ukomo mpaka mmoja au wengine kati yao watakapochukua jukumu la usimamizi.

Wakati mtu hana akili sawa

**37.** Ikiwa mtu kichaa alitakiwa, ila kwa ukichaa wake, kupewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi iliyo au isiyo ambatanishwa na wosia, inaweza ikapewa kwa mtu ambaye uangalifu wa mali zake umewekwa kwenye mamlaka yenye nguvu, au kwa mtu yule kama mahakama itakavyoona yafaa, kwa matumizi na kwa faida ya mtu kichaa, kwa ukomo mpaka mtu yule atakaporudi kwenye hali yake ya kawaida na kuchukua usimamizi mwenyewe.

*Kusubiriwa kwa utoaji*

**38**. Wakati uamuzi wa shauri lolote linahusu uhalali wa wosia wa marehemu unasuburiwa, au shauri la kuchukua, au kupinga utoaji wa uthibitisho wa wosia au utoaji wa hati za usimamizi, mahakama iinaweza ikamchagua msimamizi ma mali ya marehemu, ambaye atakuwa na haki na mamlaka ya msimamizi mkuu isipokuwa kugawa mali hizo, na kila msimamizi atakuwa chini ya usimamizi wa mahakama na atawajibika kutokana na maelekezo ya mahakama.

Ukusanyaji na utunzaji wa mali

**39**. Kama katika hali yoyote inaonekana ni muhimu kutunza mali ya marehemu, mahakama inaweza ikatoa, kwa mtu yeyote ambaye inaona anafaa, hati za usimamizi yenye ukomo wa kukusanya na kutunza mali ya marehemu, na kulipa madeni yote yaliyofikia muda wake na vitendo vyovyote (tofauti na ugawaji wa mali kama mahakama itakavyoona ni sawa) kulingana na maelekezo ya mahakama.

Mashtaka

**40**.-(1) Ikiwa ni muhimu kwa mwakilishi wa marehemu kuwa

mmoja wa upande wa shauri lililopo mahakamani, na wasii au mtu anayetakiwa kuchukua hati za usimamizi hayupo tayari kuchukua wajibu huo, hati za usimamizi inaweza kupewa kwa mchaguliwa wa upande wa mashtaka wa shauri hilo, lenye ukomo wa kumwakilisha marehemu katika shauri hilo, au au shauri lolote linaloweza kuanzishwa kwenye suala hilo au kwenye mahakama yoyote baina ya pande hizo, au pande zingine, inayogusa shauri hilo, na mpaka amri ya mahakama itoke na utekelezwaji wake ufanywe kabisa.

(2) Ikiwa, miezi kumi na miwili imepita toka uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi itoke, na wasii au msimamizi aliyepewa hayupo Tanzania, mahakama inaweza ikatoa kwa mtu yeyote kama inavyoona sawa hati za usimamizi yenye ukomo katika dhumuni la kuwa na kufanywa upande mmoja wa shauri litakaloletwa dhidi ya wasii au msimamizi, na kuchukua amri ya mahakama itakayotolewa juu ya shauri hilo.

Mali ya amana

**41**. Ikiwa mtu amekufa, na kuacha mali ambayo alikuwa ndio mnufaikaji wa mwisho, au hakuwa na masilahi yeyote yenye faida katika hilo, na hajaacha muwakilishi wa jumla, au mtu ambaye hawezi au hayuko tayari kuchukua jukumu hilo, hati ya wosia, yenye ukomo kwa mali hiyo, inaweza ikatolewa kwa mnufaikaji, au kwa mtu yeeyote kwa niaba yake.

*F. Utolewaji kwa Kiasi*

Utoaji kwa kiasi

**42**. Ikiwa hali ya shauri inahitaji kiasi cha mali kithibitishwe au kitolewe hati za usimamizi iliyo au isiyoambatana na wosia, utolewaji huo utafanywa kulingana na kiasi hicho.

Utolewa wa kiasi kilichobaki

**43**. Ikiwa toleo la uthibitisho wa wosia u hati ya usimamizi iliyo au isiyoambatanishwa na wosia imetolewa kwa kiasi cha mali, toleo lingine linaweza likafanyika katika kiasi cha mali kilichobaki.

*G.Madhara ya Utoaji wa Hati za Usimamizi*

Madhara ya utoaji wa hati za usimamizi

**44.** Sambamba na vizuizi vilivyomo, kama usimamizi umetolewa kwa ajili ya dhumuni maalumu, kwa dhumuni hilo tu, hati za usimamizi inamwezesha msimamizi awe na haki aliyokuwa nayo marehemu kana kwamba amepewa usimamizi wakati wa kifo cha marehemu:

Isipokuwa kwamba hati za usimamizi hakitahalalisha kitendo chochote ingilivu cha msimamizi kinacholenga kupunguza au kuharibu mali ya marehemu aliyefariki bila kuacha wosia

*H. Kifo cha Wasii au Wasimamizi na Kuisha kwa Muda wa Toleo lenye Ukomo*

Kifo cha mwakilishi au wawakilishi

**45**. Ikiwa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi imepewa kwa zaidi ya wasii au msimamizi mmoja na mmoja wao akafariki, usimamizi wa mali zilizobaki, kama hakuna muongozo katika wosia au uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, utabaki kwa wasii au msimamizi au wasimamizi waliobakia.

Kifo cha mwakilishi

**46.** Pale wasii mmoja au wasii aliyebaki na aliyethibitisha

au mwakilishi aliyebaki

wosia akafa, au msimamizi mmoja au msimamizi aliyebaki, hati za usimamizi wa mirathi itatolwa kuhusiana na mali ambazo hazijaamuliwa, na mahakama itatumia vifungu vilevile ilivyotumia mwanzo katika utoaji wa hati hiyo ya ya usimamizi wa mirathi.

Ikiwa wasii mmoja au zaidi wamethibitisha wosia au hati za usimamizi iliyoambatanishwa na wosia imetolewa, mahakama inaweza ikatoa hati za usimamizi wa wa mirathi katika kigungu hiki bila kumuita wasii ambaye hakuthibitisha wasii.

Kuisha kwa muda kwa toleo lenye ukomo

**47**. Ikiwa usimamizi wa mirathi wenye kikomo umekwisha kutokana na kuisha kwa muda uliopangwa, au kwa kutokea suala lenye ukomo, au suala ambalo halikutarajiwa na kuna baadhi ya mali hazijaamuliwa, hati za usimamizi wa mirathi itatolewa kwa watu wale ambao wangeweza kupewa usimamizi huo kwa mara ya kwanza.

## SEHEMU YA VI
## PINGAMIZI NA MABADILIKO YA TOLEO NA KUONDOLEWA KWA WASII AU MSIMAMIZI

Kubadilisha makosa

48. Makosa katika majina au maelezo, au muda na mahali ambapo marehemu alifariki, au dhumuni katika usimamizi wenye ukomo, vinaweza kurekebishwa na mahakama, na tolea la uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi unaweza ukabadilishwa au kurekebishwa kama itavyotakiwa.

Kupingwa wa toleo na uondolewaji wa wasii

**49**.-(1) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au utolewaji wa barua ya mirathi unaweza kutenguliwa au kubatilishwa kwa sababu zifuatazo-

(a) ikiwa mwenendo mzima wa utolewaji ulikuwa na mapungufu;
(b) kwamba utolewaji wa usimamizi wa mirathi ulipatikana kwa udanganyifu kwa kutoa shauri la uongo, au kwa kufichajambo la maana katika shauri;
(c) kwamba utolewaji wa usimamizi wa mirathi ulipatikana kwa njia ya dai lisilo la ukweli katika jambo ambalo ni muhimu katika sheria kuthibitisha utolewaji wa usimamizi wa mirathi, hata kama dai hilo lilitolewa kwa kutojua au kupitiwa;
(d) kwamba uusimamizi wa mirathi hiyo umekuwa duni na haupo tena;
(e) kwamba mtu aliyepewa usimamizi wa mirathi kwa kukusudia na kwa kutokuwa na sababu yoyote hajapeleka orodha ya jinsi alivyosimamia mali za marehemu au mahesabu kama inavyotakiwa katika Sehemu ya XI au ameleta orodha au hesabu ambazo si za kweli katika

sehemu hiyo.

(2) Ikiwa ikathibitika kuwa usimamizi stahiki wa mali za marehemu na masilahi ya wanufaishwaji unahitajika, mahakama itamuondoa wasii au msimamizi (tofauti na kabidhi wasii au muamana wa serikali) na kumuweka mtu mwingine katika ofisi ya wasii au msimamizi ambaye anaachia ofisi na atamuachia kila kitu kinachohusiana na mali husika.

Malipo yaliyofanywa na wawakilishi ambao wameondolewa

**50.**-(1) Ikiwa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi umetenguliwa, malipo yote yaliyofanywa na wasii au msimamizi kwa kipindi alichokuwa akisimamia, yatakuwa ni halali kwa mtu aliyefanya malipo hayo, bila kujalisha utenguliwaji huo.

(2) Wasii au msimamizi aliyetenguliwa kusimamia mirathi anaweza akajilipa kutoka katika mali ya marehemu kuhusiana na malipo aliyoyafanya ambapo mtu ambaye atapewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi angeyafanya kihalali.

Kurudisha toleo lililotenguliwa

**51**.-(1) Ikiwa uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi ikitenguliwa kwa mujibu wa Sheria hii, mtu huyo ambaye alithibitishwa atatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi katika mahakama iliyompatia usimamizi huo.

(2) Ikiwa mtu huyo kwa makusudi na bila sababu yoyote ya msingi akishindwa kuwasilisha uthibitisho wa wosia au barua hiyo atakuwa anafanya kosa lenye adhabu ya faini isiyozidi shilling elfu mbili au kifungo kisichozidi miezi mitatu,au vyote kwa maana ya faini na kifungo

## SEHEMU YA VII
## UTARATIBU WA KUTOA UTHIBITISHO WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI( HAIJUMUISHI MIRATHI YENYE MALI CHACHE)

Kanuni zitakazotumika mahakamani

**52**. Tofauti na itavyoelezwa hapa, na sambamba na kanuni za uthibitisho wa mirathi zilizotengenezwa kwa dhumuni hilo-

(a) kesi zozote za uthibitishwaji wa wosia na utoaji wa hati za usimamizi wa mirathi zitafuata Sheria ya Mashauri ya Madai au marekebisho yoyote yatakoiondoa Sheria ya Mashauri ya Madai; na

Sura ya 33

(b) katika hali ambayo kuna mabishano, mwenendo wa mashtaka utachukua sura hii, muombaji atakuwa mdaawa na mtu yeyote atakayejitokeza kupinga atakuwa mdaiwa

Maombi kwenda Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya

**53**.-(1) Maombi ya uthibitishwaji wa wosia yatafanywa Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya aliyechagulia katika eneo ambalo marehemu alikuwa akiishi katika kipindi cha kifo chake

(2) Ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi kwa mteule wa wilaya, kama imefanywa na imethibitishwa kama inavyotakiwa hapa, itakuwa ushahidi dhumuni la kuthibitisha utoaji wa hati ya uthibitisho au hati za usimamizi, na hakuna toleo litakalo pingwa kwa sababu ya

kwamba marehemu hakuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambayo mteule wa wilaya amechaguliwa isipokuwa kwa mwenendo wa kubatilisha toleo kama lilipatitaka kwa udanganyifu mbele ya mahakama.

Mteule wa Wilaya kusimamisha mashitaka na kutuma ripoti Mahakama Kuu

**54**.-(1) Ikiwa ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi limefanyikwa kwa hatimu mteule au-

(a) ombi limefanyika kuhusu mali inayozidi kumi na tano elfu, na likapingwa; au

(b) kama mteule wa wilaya akiona kuwa uthibitisho wa wasii au hati za usimamizi wa wosia haitakiwi kutolewa naye,

mteule wa wilaya atasitisha mwenendo wa mshitaka na ataipa taarifa Mahakama Kuu.

(2) Baada ya kuupokea ripoti hiyo, Mahakama Kuu inaweza ikamruhusu mteule wa wilaya kuendelea na shauri kwa kuzingatia ushauri ambao mahakana kuu utaona sawa, au inaweza ikakataza mwendelezo wa shauri na mteule wa wilaya kuhusu suala la ombi hilo,na kuwaruhusu mwombaji hao wapeleke maombi yao Mahakama Kuu.

(3) Pale Mahakama Kuu itakapokataza mwendelezo wa shauri hilo na mteule wa wilaya, maombi, pamoja na nyaraka zote zilizoletwa mahakamani, zitarudishwa kwa mleta maombi, ili ziweze kuwasilishwa Mahakama Kuu, isipokuwa kama mteule wa wilaya ataona ni muhimu kwa ajili ya haki kutoruhusu nyaraka hizo zitoke, kwa kuwa anaruhusiwa kufanya hivyo; na katika suala hizo nyaraka hizo zitatumwa na yeye Mahakama Kuu.

Maombi ya uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi iliyoambatanishwa na wosia

**55.**-(1) Ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, yatafanywa kwa maombi pamoja na wosia, au, katika hali zilizotajwa katika kifungu cha 25, nakala au maelezo ya maneno yaliyosemwa ikiambatanishwa na wosia na mmaombi yataeleza-

(a) tarehe and mahali marehemu alipokufa;

(b) kwamba maandishi yaliambatanishwa ni wosia wake wa mwisho na ni agano lake, au kama itakavyokuwa;

(c) kiasi na aina ya mali ambayo itatakiwa isimamiwe na muombaji;

(d) majina na anuani, kama zinajulikana, za wasii waliotajwa kwenye wasii, na, pale maombi yatakapokuwa ni ya uthibitisho wa wosia, kwamba muombaji ni wasii alietajwa kwenye wosia; na

(e) kama mwenendo wowote wa utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, au vinginenevyo kwa usimamizi wa mali umefanyika kabla katika mahakama nyingine yenye mamlaka, ikiwa ni ndani au nje ya Tanzania.

(2) Tofauti na mahitaji hayo, maombi yataelezea, pale maombi yatakapo takiwa kupelekwa kwa hakimu mteuliwa, kwamba marehemu wakati wa kifo chake alikuwa na makazi ya kudumu katika eneo la mamlaka la hakimu huyo mteuliwa.

(3) Ikiwa wosia, nakala, hawala, au maelezo ya maneno yaliyosemwa, yameandikwa katika lugha ambayo si kingereza, tafsiri iliyofanywa na mtu ambaye ni bingwa katika tafsiri, na kuthibitishwa na mtu huyo itaambatanishwa kwenye maombi.

Maombi ya hati za usimamizi

**56**.-(1) Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kuombwa kwa maombi yatakayokuwa na-

(a) tarehe na mahali ambapo marehemu alifariki;

(b) familia au ndugu wa marehemu pamoja na maeneo waishio;

(c) haki ambayo muomba maombi anadai;

(d) kiwango na aina ya mali ambayo yanatakiwa kuwa mikononi mwa muomba maombi;

(e) utafutaji wa kina umefanyika na hakuna Wosia uliopatikana; na

(f) au kama kuna shauri lolote kuhusu maombi ya barua ya usimamizi au lolote lile kuhusu usimamizi, limeanza kushughulikiwa na mahakama yoyote au mamlaka, iwe nadani ya Tanzania au nje ya Tanzania

(2) Ikiwa shauri la maombi ya usimamizi wa mirathi yapo chini ya hakimu wa wilaya mteuliwa, maombi hayo yanapaswa pia kutaja kama ziada, kwamba katika kipindi cha kifo cha marehemu alikuwa akiishi katika eneo hilo la mteule wa wilaya

Uthibitisho wa maombi

**57.**-(1) Maombi ya uthibitishwaji wa usimizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kusainiwa na muomba maombi na wakili wake kama yupo na yanatakiwa kuthibitishwa na muomba maombi

(2) Pale ambapo maombi yanahusu uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi, au ya barua ya usimamizi wa mirathi yaliyoambatanishwa na wosia, maombi hayo yatatakiwa kuthibitishwa na angalau mmoja wa mashahidi katika wosia:

Ilimradi mahakama inaweza isihitaji uthibitisho wa shahidi, kama ikiridhika kuwa uthibitisho hauwezi kupatikana au hauwezi kupatikana kwa muda unaotakiwa, au utahitaji gharama kubwa kupatikana.

(3) Kama maombi au tamko linahitaji kuthibitishwa, na likawa na kitu ambacho mtu anaethibitisha anajua au anaamini kuwa ni uongo au haamini kuwa ni cha kweli, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la jinai and kama akitiwa hatiani atatumikia kifungo cha muda usiozidi miaka saba

Zuio kupinga utoaji wa uthibitisho wa wosia au usimamizi

**58**.-(1) Mtu yeyote aliye na maslahi katika mirathi ya marehemu anaweza kuweka zuio katika utoaji wa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi

(2) Zuio linaweza kuwekwa katika Mahakama Kuu, au pale ambapo marehemu alikuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambapo mteule wa wilaya amechaguliwa au maombi ya uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi imetolewa na mteule wa wilaya, na mteule wa wilaya husika.

(3) Mara baada ya zuio hilo kuwekwa kwa mteule wa wilaya,

hakimu huyo atatuma nakala ya zuio katika Mahakama Kuu.

(4) Ikiwa zuio limepelekwa Mahakama Kuu na inaonyesha kuwa marehemu wakati wa kifo chake, alikuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambayo mteule wa wilaya amechaguliwa, msajili atatuma nakala kwa mteule wa wilaya.

(5) Zuio litakuwa na nguvu kwa muda wa miezi minne baada ya tarehe lilipowekwa (isipokuwa likiondolewa kabla ya muda huo) lakini, sambamba na kifungu cha 59, linaweza likarudishwa.

Mwendendo baada ya kuwekwa kwa zuio

**59**.-(1) Sambamba na kama inavyotolewa na kifungu hiki, hakuna mwenendo utakaofanyika katika uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, baada ya zuio kuwekwa katika mahakama ambapo maombi yamefanyika kwa muda wote ambao zuio litakuwa na nguvu.

(2) Ikiwa zuio limewekwa, mtu yeyote aliyeomba uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi ataomba wito utolewe kwenda kwa mpingaji ili kumuita aje aseme, katika muda utakao kuwa umewekwa, kama anaunga mkono utolewaji wa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi, na kama haungi mkono, kumtaka ajitokeze mbele ya mahakama katika maombi hayo.

(3) Ikiwa mpingaji atajitokeza, mahakama itaendelea na maombi kama invoonyeshwa katika aya (b)ya kifungu cha 52.

(4)Ikiwa mpingaji akitoa notisi ya kuwa anaunga mkono maombi, au akishindwa kutoa notisi kwa jinsi hiyo na akashindwa kujitokeza mahakamani kwa ajili ya maombi yake, kwa muda uliopangwa, zuio litasemekana kuwa limeondolewa na hakuna zuio lingine litakalowekwa na mpingaji mwenyewe au kwa niaba yake.

Agizo ya kuleta mahakamani makaratasi yahusuyo wosia

**60**.-(1) Mahakama inaweza ikatoa amri kwa mtu yeyote kutoa au kuleta mahakamani karatasi yeyote au maandishi ambayo au yanasemakana kuwa ni wosia, ambayo imesemekana kuwa ipo katika umiliki au chini ya uangalizi wa mtu huyo.

(2) Kama haitaonyeshwa kuwa karatasi yoyote au maandishi yapo katika umiliki au chini ya uangalizi wa mtu huyo, lakini kuna sababu ya kuamini kuwa ana uelewa wa uwepo wa karatasi hiyo au maandishi au ya wosia wa mdomo, mahakama itamuhitaji mtu huyo aje mahakamani kwa dhumuni la kuchunguzwa kuhusiana na suala hilo, na mtu huyo atatakiwa ajibu maswali kadri yatakavoulizwa kwake na mahakama na, kama ikiamriwa, kutoa karatasi hiyo au maandishi yaliyo katika umiliki wake au chini ya uangalizi wake.

Mahakama inaweza ikamchunguza mleta maombi, au ikahitaji ushahidi wa ziada na kutoa wito

**61**.-(1) Katika hali yoyote itakuwa halali kwa Mahakama, kama ikiona ni sawa-

(a) kumchunguza muombaji mwenyewe chini ya kiapo;

(b) kuhitaji ushahidi mwingine kuhusiana na kifo cha marehemu na usimamizi sahihi wa wosiawosia, au haki ya mleta maombi kuhusiana na hati za usimamizi, kama hali

itakavokuuwa; na

(c) Kutoa wito wa kuita watu wote au wale wanaodai wana masilahi katika mali ya marehemu waje waone mwenendo wa shauri kabla ya utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi.

(2) Wito utawekwa katika mahali pa wazi katika Mahakama, na viginevyo kuchapishwa au kufanywa ujulikane katika namna ambayo kanuni za uthibitisho wa wosia zitakavyoelekeza au Mahakama itakavyotoa maelekezo hayo.

Muda kabla toleo halijafanywa

**62**. Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi unaotokana na Wosia hauwezi kutolewa mpaka kumalizika kwa siku saba, na barua ya usimamizi wa mirathi haiwezi kutolewa mpaka siku kumi na nne kumalizika, tangu mtoa Wosia au yule ambaye hakuacha Wosia kufariki.

Utolewaji wa uthibitisho wa wosia na usimamizi

**63.** Pale ikitokea kwa Mahakama kwamba uthibitishwaji wa msimamizi wa mirathi anayetokana na Wosia au barua ya usimamizi wa mirathi inatakiwa kutolewa, uthibitishwaji huo au usimamizi huo utatolewa chini ya muhuri wa Mahakama

Kukataa kutoa hati za usimamizi

**64**. Pasipo kuathiri kifungu chochote, Mahakama itakuwa na utashi wa kutoa amri, huku ikitoa sababu zilizo katika maandishi, kukataa maombi ya kutoa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mujibu wa Sheria hii.

Maelekezo kwa wasii au msimamizi

**65**. Mahakama inaweza kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa msimamizi wa mirathi juu ya mali ya marehemu au juu ya usimamizi wa mali hiyo.

Kiapo

**66**. Baada ya kuthibitishwa usimamizi wa mirathi kupitia Wosia au barua ya usimamizi wa mirathi, yule aliyepewa usimamizi atatakiwa kula kiapo cha uaminifu wa kusimamia mali za marehemu

Isipokuwa kifungu hiki hakitatumika pale mpewaji atakapokuwa ni muamana wa serikali au kabidhi-wasihi

Dhamana ya usimamiaji

**67.** Mtu yeyote ambaye amepewa hati za usimamizi na, kama Mahakama itaelekeza, mtu yeyote ambaye amepewa uthibitisho wa wosia atatoa dhamana akiwa mmoja au wadhamini zaidi, katika ukusanyaji, na katika usimamizi wa mali za marehemu

Isipokuwa Mahakama inaweza, kwa sababu nzuri, ikaachilia mbali suala la dhamana na wadhamini, au vyote, katika hali husika.

Kumpa mtu mwingine dhamana ya usimamizi

**68**. Mahakama inaweza, kutokana na maombi yaliyoletwa na ikijiridhisha kuwa uwekwaji wa dhamana haujafutwa, na kulingana na masharti ya dhamana, au kwamba pesa iliyopokelewa ilipwe katika Mahakama, au vinginevyo kama Mahakama inavyoona sawa, ikaweka watu fulani, ambao wataweza kufungua mashtaka katika dhamana hiyo kwa jina lake kana kwamba alipewa dhamana hiyo kwa mara ya kwanza na si Mahakama, na atatakiwa apokee, kama muamana wa watu wote wenye masilahi, kiasi chote kinachotakiwa katika uvunjwaji huo.

Matunzo ya

**69**. Wosia zote halali ambazo uthibitisho wa wosia na hati za

wosia halisi

usimamizi zilizoambatanishwa na wosia zimetolewa na Mahakama zitatunzwa na kuhifadhiwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na wosia wowote uliowekwa na nakala za kutolewa kwa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi, sambamba na uangalizi wa Mahakama Kuu na vifungu vya kanuni za uthibitisho wa wosia, zitakuwa wazi kwa ukaguzi.

Hitimisho la uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi

**70.** Uthibitisho wa wosia na hati ya usimamizi wa mirathi vitakuwa-

(a) Na nguvu kwa mali zote za marehemu zile zinazohamishika na zisizo hamishika zinazopatikana sehemu yeyote Tanzania

(b) Uthibitisho wa mwisho wa uwakilishi juu ya madeni yoyote ya marehemu, na watu wengine wanaoshikilia vitu ambavyo ni mali za marehemu

(c) Itawarudishia wadeni kwa kuwalipa madeni yao, na watu wote wanaoleta mali kwa mtu ambaye uthibitisho wa wosia au hati ya usimamizi wa mirathi umeshatolewa

Mpewaji pekee atakuwa muwakilishi

**71**. Baada ya uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi kutolewa, hakuna mtu zaidi ya yule ambaye usimamizi umetolewa atakaye kuwa na nguvu za kushitaki au kuendesha mashtaka yoyote, au vinginevyo kujifanya kuwa ni msimamizi wa marehemu, mpaka pale uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi itakapotenguliwa au kubatilishwa.

Rufaa na marudio

**72**.-(1) Rufaa itahusu amri ya kutoa au kupinga utolewaji wa wosia au hati ya usimamizi iliyofanyika katika mirathi inayobishaniwa kama kwamba agizo ni amri, na kutoka kwenye agizo lolote lililofikiwa katika hali ambayo rufaa ingekatwa kutokana na vipengele vya Sheria ya Daawa au Sheria yoyote itakayo ipokea Sheria hiyo.

Sura ya 33

Sura ya 33

(2) Vifungu vya Sheria ya Daawa vitatumika pamoja na mabadiliko yatakayobidi, kuhusiana ma mienendo ya shauri mbele ya mteule wa wilaya katika Sheria hii

## SEHEMU YA VIII

## A. MAZOEA NA HATUA ZA KUCHAGUA NA KUPINGWA UCHAGUZI WA, WASIMAMIZI KATIKA MALI CHACHE

Matumizi ya sehemu ya VIII

**73**.-(1) Sehemu hii itatumika pindi maombi yatakapofanyika mbele ya Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi kwa uchaguzi wa msimamizi wa mali chache, au pale maelekezo yatakapo tolewa, katika sehemu ya XI, kwamba sehemu hii itatumika katika mali chache husika.

(2) Isipokuwa kama itakavyotolewa katika sehemu hii, pale ambapo SEHEMU hii itatumika, vifungu vya sehemu ya IV, V, VI, na

VII (tofauti na vifungu vya 52(b), 60, 61, 62, 65, 70 na 71 havitatumika.

(3) Ikiwa sehemu hii itatumika Mahakama ya wilaya itatumia mamlaka yake yaliyowekwa katika Mahakama hiyo katika vifungu vya sehemu ya VII ambavyo vitatumika.

Uchaguzi wa wasimamizi

**74**. Mahakama ya wilaya inaweza ikamchagua kama msimamizi mtu mmoja au wengi wenye masilahi na mali katika usimamizi unaotakiwa na, katika kumchagua msimamizi huyo, isipokuwa kama kwa sababu yoyote inaona si vema kufanya hivyo, itazingatia mapendekezo yoyote ambayo yanaweza yakawa yamesemwa na marehemu.

Usimamizi wa kabidhi-wasihi, na uchaguzi wa afisa wa Mahakama au mtu asiye na masilahi

**75**.-(1)Pale ambapo Mahakama ya wilaya itakuwa na wazo kuwa, kwa kuchukulia a usalama wa mali na usimamizi unaotakiwa, inafaa kwamba mali isimamiwe na kabidhi-wasihi au afisa wa Mahakama ya wilaya, au mtu anayeheshimiwa na muadilifu anayeweza na aliye tayari kusimamia mali hizo, itaaahirisha maombi ya kumchagua msimamizi ili iweze kujiridhisha kuwa kabidhi wasihi atachukua usimamizi huo katika kifungu cha 52 cha Sheria ya Kabidhi Wasihi (Mamlaka na Majukumu)

Sura ya 27

au kumchagua afisa wa Mahakama ya wilaya au mtu yeyote kama ilivyooneshwa kwa msimamizi.

(2) Uchaguzi wa msimamizi katika sehemu hii hautafanyika kama kulikuwa na toleo lingine la uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi, au kama kabidhi wasihi amechukua usimamizi huo kihalali.

Uteuzi uwe na muhuri

**76**.-(1) Uteuzi wa msimamizi wa mirathi ndogo utafanyika chini ya muhuri wa Mahakama ya wilaya

(2) Kila msimamizi ataweka saini kwamba atasimamia mali za marehemu kwa uaminifu

Dhamana kwa usimamizi thabiti

**77**. Mahakama ya Wilaya, pale itakapoona inafaa, inaweza kumtaka msimamizi wa mirathi ndogo kuweka dhamana ili kuweza kusimamia mali za marehemu.

Wosia

**78**.-(1) Mahakama ya Wilaya inaweza kuruhusu Wosia kutolewa kwa ushahidi wa kuzungumza au kwa kiapo, na inaweza kukubali uthibitishwaji wa maelezo yaliyo katika Wosia huo ambayo yanaonekana ni ya msingi japo si ushahidi wa kisheria

(2) Nakala ya wosia, au kama wosia wa mdomo, maandishi ya maneno ya marehemu yataambatanishwa katika uchaguzi wa msimamizi

(3) Wasii halisi utawekwa na kutunzwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na kifungu cha 69 kitatumika, pamoja na mabadiliko yaliyobidi, katika wosia hizo na nakala za uchaguzi uliofanywa katika sehemu hii.

Uteuzi unaweza

**79**.Uteuzi wa msimamizi wa mirathi chini ya sehemu

kuwa kwa mali yote au sehemu ya mali hiyo

hii,inaweza kumpa usimamizi wa mali zote za marehemu au sehemu ya mali hizo zilizoorodheshwa katika uteuzi, na utakuwa na nguvu sehemu yoyote ile katika Tanzania

Madhara ya Uteuzi

**80**.-(1) Uteuzi wa msimamizi katika sehemu hii utaweka mali za marehemu chini ya msimamizi, ambaye, atakuwa na mamlaka sambamba na wajibu wote kama kwamba hati za usimamizi wa mali imepewa kwake.

(2) Msimamizi aliyechaguliwa katika sehemu hii, isipokuwa kama Mahakama ya wilaya ambayo imemchagua au vinginevyo itaamuru, hatatakiwa kupeleka orodha au mahesabu au kuweka dhamana.

(3) Kama msimamizi atatakiwa kupeleka orodha au mahesabu, kifungu cha 103 kitatumika kama kwamba Mahakama ya wilaya imetoa hati za usimamizi wa wosia kwa msimamizi

Mali zisizodaiwa

**81**. Msimamizi aliyechaguliwa katika sehemu hii ambaye ana mali katika himaya yake ambazo hakuna mdai halali kwa mwaka mmoja toka kifo cha mtoa wosia atamtaarifu Kabidhi- Wasii, na kama itahitajika Kabidhi- Wasii atazihamisha mali hizo kwa Kabidhi-Wasii, na mali hizo zitasimamiwa sambamba na vifungu vya 48 na 49 vya Sheria ya Kabidhi- Wasii (Mamlaka na Majukumu).

Sura ya 27

Utenguzi wa uteuzi

**82**. Uchaguzi wa msimamizi unaweza ukatenguliwa na Mahakama ya wilaya ambayo ilimchagua kwa sababu yeyote ambayo itaridhisha kutenguliwa kwa hati ya uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi au uondoaji wa wasii, na hali kama hizo.

Rufaa ziende Mahakama Kuu

**83**.-(1) Sambamba na Kanuni za Uthibitisho wa Wosia, kila uchaguzi, muongozo, au uamuzi wa Mahakama ya wilaya katika sehemu hili unaweza ukakatiwa rufaa katika Mahakama Kuu

(2) Kanuni za Uthibitisho wa wosia zinaweza zikazuia au zitatoa muongozo kuhusiana na haki ya kukata rufaa kwa kiasi chochote na hali yoyote.

Mahakama ya wilaya kutuma ripoti Mahakama Kuu

**84**. Kila Mahakama ya wilaya itapeleka ripoti ya mienendo yote katika sehemu hii Mahakama Kuu kama itakavyoonyeshwa na Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi

Uzuiaji wa kutoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika mali chache

**85**.-(1) Kama msimamizi wa mali chache amechaguliwa katika sehemu hii, hakuna uthibitisho wa wosia wa marehemu au hati za usimamizi wa mali zake utakaotolewa-

(a) na mteule wa wilaya, isipokuwa kama ya uchaguzi wa msimamizi umevunjwa na Mahakama ya wilaya ambayo ilimchagua; au

(b) na Mahakama Kuu isipokuwa kama ikiona kuwa utoaji huo ni muhimu katika kufikia haki, au katika kumlinda mnufaishwaji yeyote au mdeni

(2) Utolewaji na Mahakama Kuu wa uthibitisho wa wosia wa

marehemu au hati za usimamizi wa mali yake hutabatilisha uchaguzi wowote wa msimamizi katika sehemu hii. Na ubatilisho huo utakuwa na nguvu sawa kama ubatilishwaji wa hati za usimamizi.

(3) Isipokuwa kama inavyotolewa katika kifungu cha 86, hakuna kitu katika sehemu hii kitakachoathiri mamlaka ya kutoa au kubatilisha uthibitisho wa wosia wa marehemu au hati za usimamizi wa mali zake.

Uhalali wa uteuzi katika mali zinazozidi shilingi elfu kumi

**86**.-(1) Hakuna uteuzi wa wasimamizi katika sehemu hii utakaokuwa batili kwa sababu tu imejulikana kuwa thamani ya mali ya marehemu imezidi shilingi elfu kumi, lakini, Mahakama ya wilaya ikilijua hilo itatoa ripoti Mahakama Kuu, ambayo kama itaona sawa itatoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi.

(2) Kama Mahakama Kuu ikitoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika kifungu hiki, kifungu kidogo cha (2) 85 kitatumika.

Usimamizi wa mali chini ya shilingi elfu moja

**87.**-(1) Ikiwa thamani ya mali ni chini ya shilingi elfu moja haitakuwa na umuhimu wa kumchagua msimamizi, na mali hizo zitasimamiwa na mwenza wa marehemu aliyebaki au, kama hakuna mwenza, ndugu wa karibu wa marehemu ambaye yuko tayari, ambaye kwa dhumuni hilo atakuwa ameteuliwa kuwa msimamizi wa mali hiyo.

Ila kama Sheria hii inatumika katika sehemu ya IX, mtu atakayesimamia mali hiyo atakuwa ni ndugu wa kiume wa karibu wa marehemu;

Ila waziri kama akiona yafaa, ataagiza katika gazeti la serikali, kuongeza pesa itakayosimamiwa katika kifungu hiki.

(2) Kama Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi kuhusiana na mali yoyote chini ya mamlaka yake, anaweza kuzuia au kutoa mwongozo katika utekelezaji wa majukumu yaliyowekwa na kifungu hiki na anaweza akamuweka mtu yeyote badala ya mwenza au ndugu wa karibu, kama hali itakavyokuwa, kusimamia mali hiyo, ikiwa kwa mawazo ya Mahakama ubadilishwaji huo ni wa muhimu kuendana na mazoea na mila ambazo zinatumika na pande za mashitaka katika shauri hilo au inahitajika kwa sababu nyingine.

## B. USIMAMIZI WA MALI CHACHE

Sura ya 30

Sheria inayotumika kwa mtu wa kabila fulani

**88**.-(1) Mali yoyote ya marehemu, kutokana na agizo na maelekezo ya sehemu ya IX, zitasimamiwa kutokana na vifungu vifuatavyo-

Namba 33 ya mwaka 1947 kifungu cha 5; 35 cha mwaka 1961 jedwali la pili; sura

(a) Mali ya mtu wa kabila fulani zitasimamiwa kutokana na Sheria za kabila hilo isipokuwa kama marehemu katika muda wowote alikuwa ni mfuasi wa dini ya kiislam na

ya 277 kifungu cha 3 { sura ya 30 vifungu vya 19,20,na 21}

Mahakama yenye mamlaka na mali yake imejiridhisha kutokana na maneno au maandishi ya marehemu au matendo yake au aina ya maisha yake kuwa marehemu alikuwa na nia ya kuwa mali isimamiwe, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa kufuata Sheria za kiislam, na kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria hiyo.

(b) Mali ya mswahili itasimamiwa kwa kufuata Sheria za kiislam isipokuwa Mahakama iliyo na mamlaka na mali hiyo imejiridhisha kuwa kutokana na maneno au maandishi ya marehemu au matendo yake au aina ya maisha alikuwa na nia kuwa mali yake isimamiwe, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa kufuata Sheria za kimila, na kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria za kimila.

(2) Kama mtu yeyote katika muda wowote ambaye Sheria hii inatumika katika mali yake kwa ajili ya agizo, au maelekezo katika sehemu ya ix alikuwa anaamini katika dini ya kikristu, na Mahakama iliyo na mamalaka na mali yake imejiridhisha kuwa marehemu alikuwa ana nia ya Sheria zinazotumika Tanzania kwa watu wanaoamini dini ya kikristu zitumike katika usimamizi wa mali yake, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria hiyo

(3) Rais anaweza, kama akiona sawa, baada ya muda fulani, kwa agizo litakalochapishwa katika gazeti la Serikali, kusema ipi ni Sheria ya kabila, ikiwa kwa ujumla wake au katika kipengele maalum

(4) Bila kujali Sheria yoyote ya mila au ya kiislam tofauti-

(a) kila mdai atakuwa na haki katika mali ya marehemu (ikijumuishwa haki ya kufuata mali); na

(b) Mtu yeyote hatanyimwa haki yake ya kurithi kitu chochote kwa sababu tu mtu huyo amejitoa katika dini fulani

Wosia wa mtu wa kabila

**89**.-(1) Katika usimamizi wa mali za marehemu, kwa kufuata agizo au maelekezo ya sehemu ya IX ya Sheria hii, mgao wowote wa mali unaogawa sehemu yoyote ya mali utatambuliwa kama wasii, kama utatimiza mahitaji haya-

(a) kama mali itasimamiwa kwa kutumia Sheria za kimila kama aidha-

(i) Ugawaji unatambuliwa kuwa halali na Sheria hiyo ya mila; au

(ii) Ugawaji ni halali kwa kufuata maelekezo ya

agizo la Waziri, ambapo linasema kuwa ugawaji wa mali, ulifanywa na marehemu au na mtu yeyote wa tabaka fulani ambalo linamjumuisha marehemu na limefanywa kwa kuzingatia Sheria ya Indian Succession Act, 1865, inayohusu wasii, na wa kiasi na vikwazo vitakavyowekwa ili uweze kuwa halali.

(b) ikiwa mali itasimamiwa kutokana na Sheria inayotumika kwa mali za watu wanaoamini dini ya kikristo, kama mgao huo umefanywa kwa kuzingatia vifungu vya Indian Succession Act, 1865, inayohusu wasii; na

(c) Ikiwa mali itasimamiwa kwa kuzingatia Sheria za kiislam, kama mgao utajulikana kuwa ni wa halali na Sheria hiyo.

(2) Ugawaji wa mali ambao kifungu hiki kinatumika, hautafuatwa mpaka uwe umethibitishwa kuwa ni halali na Mahakama iliyo na mamlaka katika mali hiyo

(3) Uhalisia wa ugawaji uliotajwa kuwa ni halali katika kifungu hiki, kama upo katika maandishi, utatunzwa na Mahakama; katika hali ambayo itakuwa imetolewa na kanuni za Mahakama, na nakala ya wosia atapewa msimamizi wa mali hiyo.

(4) Ikiwa mgao wowote wa mdomo umetajwa kuwa ni wa halali katika kifungu hiki, mgao huo utawekwa katika maandishi na Mahakama, na nakala moja atapewa msimamizi wa mali hiyo.

{Imefutwa na sura ya 277 kifungu cha 5; sheria namba 35 ya 1961 ya jedwali la pili}

**90**. (Sheria inayotumika katika mali za wasomali}

Imefutwa na sheria na 33 ya mwaka 1947 kifungu cha 35 cha mwaka 1961 jedwali la pili}

**91.** {Rejea sura ya 16 iliyofanyiwa mabadiliko 1928, katika sheria zingine}

## SEHEMU YA IX
## MALI ZINAZOSIMAMIWA KWA KUTUMIA SHERIA ZA KITAMADUNI, MILA NA SHERIA ZA KIISLAM

Hali ambazo Sheria hii itatumika kwa mali zinazosimamiwa kwa Sheria za kimila namba 9 ya 1963; 9 ya 1965
Sura ya 29

**92**.-(1) Vifungu vya Sheria hii havitatumika katika usimamizi wa mali ambazo Mahakama ya mwanzo ina mamlaka isipokuwa-

(a) kama waziri, akitoa agizo litakalochapishwa katika gazeti la serikali, kuwa itatumika katika aina fulani ya mali, au mali zilizopo mahali fulani, katika mali fulani zilizopo mahakama fulani; au

(b) Mahakama Kuu, aidha yenyewe au kwa maombi ya Mahakama ya wilaya, au mali ikiwa si mali chache, ya mtu mwenye masilahi, ikitoa maelekezo kuwa itatumika; au

(c) Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi, yenyewe au kutokana na maombi ya mtu yeyote mwenye masilahi, ikitoa maelekezo kuwa itumike katika mali fulani chache,

katika hali hiyo vifungu vya Sheria hii vitatumika kwa namna na kiasi ambacho Sheria hii imetaja

Ila Mahakama ya wilaya haitatoa maelekezo yoyote katika aya ya (c) ya hiki kifungu kidogo ikiwa agizo la usimamizi wa mirathi limefanywa, au mwenendo kuhusiana na urithi umeanza katika Mahakama ya mwanzo, isipokuwa kama mwenendo umehamishiwa katika Mahakama ya wilaya katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mahakimu wa Mahakama

Sura ya 11

(2) Ikiwa Mahakama imetoa mwongozo kwamba Sheria hii itatumika, yenyewe itakuwa na mamlaka ya mwanzo kuhusiana na mali hiyo, au itatoa agizo kwa mteule wa wilaya awe na mamlaka (na aidha katika hali zote vifungu vya Sheria hii tofauti na SEHEMU YA VIII, vitatumika) au inaweza kama mali ni chache, itaiamuru Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu wa wilaya iwe na mamlaka (ambapo vifungu vya Sheria hii tofauti na sehemu ya IV,V na VI na vifungu vya 51 (1), 53, mpaka 59 (kwa pamoja), 63,64,66, mpaka 69 (kwa pamoja) na 72 vitatumika)

(3) (Imefutwa na Sheria namba 55 ya mwaka 1963:Sura ya 537)

Madhara ya maelekezo ya Mahakama Kuu kwa agizo lililofanywa na Mahakama ya mwanzo

**93**.-(1) Ikiwa agizo la kusimamia mali limefanywa na, au mwenendo kuhusiana na mirathi umeshaanzishwa katika Mahakama ya mwanzo, Mahakama Kuu haitatoa agizo lolote katika aya (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 88 isipokuwa kama ikiona ni sawa kwa masilahi ya haki au kwa ulinzi wa mnufaishwaji yeyote au mdai mali hiyo isimamiwe kwa kutumia Sheria hii.

(2) Kama Mahakama Kuu imetoa agizo lolote katika mazingira yoyote ambayo yamekwishasemwa, itaijulisha Mahakama ya mwanzo ambayo agizo la usimamizi lilitolewa, au mashtaka yalipoanzishwa, kama hali itakavyokuwa, au kusitisha mwenendo huo mpaka utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi ukamilike, au msimamizi amechaguliwa katika Sheria hii.

(3) Ikiwa agizo la usimamizi limepingwa na Mahakama ya mwanzo chini ya kifungu hiki, malipo yote ya halali yaliyofanywa na mtu aliyekuwa akitekeleza agizo hilo, bila kuzingatia upingwaji huo, yatakuwa ni malipo halali kwa mtu aliyeyafanya, na mtu anayestahili kutimiza agizo hilo atakuwa na mamlaka ya kujilipa kana kwamba alikuwa ni msimamizi ambaye usimamizi wake umepingwa katika sehemu ya VI.

## SEHEMU YA X
## USAJILI WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI

Tafsiri

**94**. Katika sehemu hili na kifungu cha 4-

"Mahakama ya uthibitisho wa wosia" inamaanisha Mahakama yoyote au mamlaka, kwa jina lolote linalojulikana, ambayo ina mamlaka katika masuala ya uthibitisho wa wosia.

"Uthibitisho wa wosia" na "hati za usimamizi" inajumuisha uthibitishwaji na Sheria yoyote katika Jumuiya ya Madola ambayo uwiano sawa katika Sheria hii unapewa katika uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi

Usajili wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi zilizotolewa nje ya Tanzania

**95**. Ikiwa Mahakama ya uthibitisho wa wosia katika sehemu yoyote ya Jumuiya ya Madola, aidha kabla au baada ya kupitishwa kwa Sheria hii, imetoa uthibitisho wosia au hati za usimamizi kuhusiana na mali ya marehemu, na uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi zilizotolewa, kama iliyotolewa na nakala yake ikapelekwa Mahakama Kuu, na kusajiliwa na muhuri wa Mahakama hiyo, itakuwa na nguvu na mamlaka sawa katika Tanzania kama imetolewa na Mahakama hiyo.

Masharti ya kuzingatiwa kabla ya kusajili

**96.** Mahakama Kuu, kabla ya kusajili uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika sehemu hii, itajiridhisha ikiwa ni hati za usimamizi kuwa dhamana imetolewa kwa kiasi kinachotosheleza kuilinda mali hiyo, kama ipo, Tanzania, na katika hali yoyote inaweza ikaomba ushahidi kama itakavyoona sawa, juu ya makazi ya marehemu.

Dhamana

**97.** Mahakama Kuu, kama ikiona sawa, ikiwa kuna maombi ya mdai yeyote, itahitaji kabla ya usajili, dhamana iwekwe kwa ulipaji wa madeni yaliyofikiwa muda wake kutoka kwenye mali kwa mdeni anayeishi Tanzania

Nakala zilizodurufiwa na kunakiliwa

**98**. Kwa dhumuni la Sheria hii, rudufu ya uthibitisho wa wasii au hati za usimamizi iliyosajiliwa na muhuri wa Mahakama iliyotoa vitu hivyo, au nakala iliyothibitishwa kuwa sahihi au chini ya mamlaka ya Mahakama iliyotoa vitu hivyo, vitakuwa na nguvu sawa kama nyaraka halisi.

## SEHEMU YA XI

## MAMLAKA NA MAJUKUMU YA WASII NA WASIMAMIZI

Namna na mali za wasii au msimamizi

**99**. Wasii au msimamizi wa marehemu, kwa hali yoyote, ni muwakilishi wa marehemu kwa dhumuni lolote,na mali zote za marehemu zitakuwa chini ya uangalizi wake

Isipokuwa, kifungu hiki hakimuwekei wasii au msimamizi-

(a) kitu chochote cha marehemu ambacho kinatakiwa kwenda kwa mhalifiwa.

(b) Kitu chochote kilichowekwa chini ya kampuni

Mamlaka juu ya mashitaka na madeni

**100**. Wasii au msimamizi ana mamlaka ya kushitaki kuhusiana na mashitaka yote yaliyoachwa na marehemu, na ana mamlaka ya kudai madeni yaliyofikiwa muda wa kulipwa wakati marehemu anafariki, kama alivyokuwa marehemu wakati wa uhai wake.

Mamlaka ya kuuza mali na kadhalika

**101**.Wasii au msimamizi anayo mamlaka , kutokana na mali iliyowekwa chini yake katika kifungu cha 99, ya kuuza kitu kinachohamishika, kama anavyoona ni sawa, na mamlaka na kuuza, kuweka rehani, kupangisha kuhusiana na mali isiyo hamishika iliyowekwa na Sheria iliyoandikwa juu ya muamana ya amana inayouzwa.

Matumizi ya uangalizi na usimamizi

**102**.Wasii au msimamizi anaweza, juu ya mamlaka nyingine ya matumizi yanayofanywa kihalali na yeye, kuingia gharama-

(a) kwa vitendo vile kama vitakavyokuwa sawa kwa utunzaji wa kitu chochote kinachohusu mali ya marehemu; na

(b) Kwa ruhusa ya Mahakama, au ya Mahakama ya wilaya iliyo na mamlaka katika shauri, juu ya vitu vilivyotolewa kidini, msaada au vitu vingine, na kwa maboresho, kama itakavyokuwa sawa na inavyotakiwa na vitu hivyo.

Wasii au msimamizi wasipate faida yoyote katika ofisi

**103**.-(1)Isipokuwa kama imesemwa waziwazi katika wosia, hakuna wasii au msimamizi anayetakiwa ajinufaishe kifedha kutoka katika ofisi ya usimamizi

(2) Kama wasii au msaidizi akinunua, moja kwa moja au vinginevyo, sehemu yoyote ya mali za marehemu, mauzo hayo yanaweza kubatilika kama kuna mtu mwingine ana masilahi na kitu hicho au mapato ya kitu hicho.

(3) Hakuna chochote katika kifungu hiki, kitakachotumika kwa ada yoyote iliyosemwa na Sheria.

Mamlaka ya wasii au wasimamizi yanaweza kufanywa na mtu mmoja

**104**. Ikiwa kuna wasii au wasimamizi, mamlaka yao yote yanaweza, kukiwa hakuna lolote ndani ya wosia au katika hati za usimamizi wa mirathi, kufanywa na mmoja wao aliyethibitisha wosia au aliyechukua usimamizi.

Mamlaka ya

**105.** Kwa kuondoa shaka, inatamkwa kuwa-

(a) msimamizi wa vitu ambavyo havijasimamiwa anayo

muwakilishi mahususi

mamlaka kuhusiana na vitu hivyo sawa na yule wasii au msimamizi wa kwanza; na

(b) Msimamizi ambaye amepewa usimamizi kutokana na kifungu cha 36 wakati wa utoto ana mamlaka yote ya wasii wa kawaida au msimamizi.

Orodha na mahesabu

**107**.-(1) Wasii au msimamizi, ndani ya miezi sita ya kupewa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, au katika muda ambao Mahakama iliyotoa usimamizi huo itahitaji, atatakiwa alete orodha ya vielelezo, vinavyoonesha vitu vyote vilivyo chini yake, na mikopo yote, na madeni yote aliyonayo mtu yeyote ambapo wasii au msimamizi anatakiwa katika mwaka mmoja baada ya kupewa usimamizi au kwa muda ule ambao Mahakama itahitaji, atoe mahesabu yanayoonyesha mali zilizokuja kwenye mikono yake na jinsi gani amevigawa.

(2) Kama usimamizi haujakamilika katika mwaka mmoja baada ya kutoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, wasii au msimamizi katika kipindi kisichozidi miezi sita, au katika muda wowote ambao Mahakama iliyotoa usimamizi huo itachagua, na baada ya kumaliza usimamizi, atatakiwa atoe vidhibiti vya hesabu vikionyesha mali ambazo zimepitia mikononi mwa msimamizi na namna ambavyo zimetumiwa tangu hesabu za mwanzo zitolewe.

(3) Kama wasii au msimamizi, akitakiwa na Mahakama kutoa orodha au hesabu katika kifungu hiki, akaacha kuitikia wito katika muda uliopangwa, atakuwa ametenda kosa la jinai, na akitiwa hatiani atatakiwa atoe fidia isiyopungua shilingi elfu mbili au atumikie kifungo kisichozidi miezi sita.

(4) Kama wasii au msimamizi akitoa orodha au hesabu za uongo huku akijua kuwa ni za uwongo katika kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa la jinai na kama atakutwa na hatia atatakiwa atumikie kifungo cha muda usiozidi miaka saba.

(5) Mnufaishwaji yeyote katika wosia, au mtu anayetakiwa apate sehemu ya mali katika urithi usiokuwa na wosia, au mdai ambaye hajaridhika anayo ruhusa ya kukagua orodha na mahesabu ya wasii au msimamizi.

(6) Kipengele hiki hakitatumika kwa kabidhi-wasii isipokuwa kama Mahakama itatoa maelekezo hayo.

Shughuli za ujumla za usimamizi

**108**.-(1) Wasii au msimamizi, anatakiwa, kwa uadilifu unaotakiwa, akusanye mali za marehemu, na madeni ambayo yamefika muda wake, alipe madeni ya marehemu na madeni na gharama za usimamizi, na kugawanya mali kwa watu au kwa dhumuni linaloendana na hilo au muamana kwa ajili ya watu hao au dhumuni au kwa kufuatisha vifungu vya Sheria hii kama itakavyotakiwa.

(2) Sambamba na vifungu vya Sheria hii, wasii au msimamizi hatakiwi kugawa mali za marehemu kabla ya kuisha kwa mwaka mmoja baada ya kifo cha marehemu.

Namna ya ulipaji wa madeni

**109**. Madeni yatalipwa kwa mpango ufuatao, kabla ya madeni yote-

(a) kwanza, gharama za mazishi kwa kiasi kinachotakiwa, kufuatana na hali ya marehemu, na gharama za kuuguzwa, zikijumuisha gharama za tiba, usafiri na malazi kwa mwezi mmoja kabla ya kifo chake.

(b) pili, gharama za kupata uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, ikijumuisha gharama zilizotumika kuhusiana na mienendo yoyote ya Mahakama inayotakiwa ifanyike kwa ajili ya usimamizi wa mali; na

(c) tatu, ujira unaotakiwa kulipwa kwa kazi alizofanyiwa marehemu na mfanyakazi yoyoye, kibarua au mtumishi wa ndani, ndani ya miezi minne kabla ya kifo chake.

(2) Baada ya kulipa madeni yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1), kisha yatalipwa madeni mengine yeyote ya marehemu kulingana na jinsi yalivyoingiwa

(3) Sambamba na kilichoelezwa katika kifungu hiki, wasii au msaidizi atalipa madeni yote anayoyajua, kwa usawa na kwa idadi sawa, kama vile mali za marehemu zinavyoweza kutosha.

Madeni yalipwe kabla ya wausiwa

**110**.-(1) Madeni ya kila namna yatalipwa mbele ya muusiwa yoyote.

(2) Kama mali ya marehemu, inatakiwa ilipe madeni ya mbeleni, wasii au msimamizi hatatakiwa kulipa urithi wowote bila kuwa na malipo ya kutosha ya kulipa madeni kwa muda wowote yatakapojitokeza.

Kupungua kwa hiba wazi na usawa wa wausiwa

**111**.-(1) Kama mali, baada ya kulipa madeni, matumizi ya muhimu na hiba mahususi, hazitoshi kulipia hiba za wazi kwa kiasi kinachotakiwa, hiba ya wazi itapunguzwa kwa urari.

(2) Kama hakuna maelekezo mengine tofauti katika wosia, wasii hana haki ya kumlipa muusiwa mmoja na kumuacha mwingine au kubaki na pesa yoyote ya hiba yeye mwenyewe au kwa mtu yeyote ambaye ni muusiwa.

(3) Kwa dhumuni la mapunguzo, hiba ya maisha, kiasi kilichotengwa na wosia kitatoa malipo ya mwaka, na gharama ya malipo ya mwaka ikiwa hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili hiyo, kitakuwa kama hiba za wazi.

Kupunguwa kwa hiba mahususi

**112**.-(1) Ikiwa kuna hiba mahususi, na mali zinatosha kulipa madeni na matumizi ya muhimu, kitu kilichotajwa lazima kitolewe kwa muusiwa bila punguzo lolote.

(2) Ikiwa mali hazitoshi kulipa madeni na matumizi na hiba mahususi, punguzo litafanywa kutoka katika hiba mahususi kwa urari wa kiasi chake

Haki ya hiba maalum

**113**. Ikiwa kuna hiba maalumu, na mali zinatosha kulipa madeni na matumizi ya muhimu, muusiwa atakuwa na dai la juu la kulipwa hiba yake kutoka katika pesa ambazo anatakiwa kulipwa mpaka pesa hizo zitakapokwisha, na kama mpaka mali hizo

zinakwisha sehemu ya hiba hiyo haijalipwa, anaruhusiwa, kudai baki kwenye mali ya jumla juu ya hiba yake ambayo haijalipwa

## SEHEMU YA XII
## HIBA NA MALIPO YA MWAKA

Ridhaa ya inahitajika kwa muusiwa kupata hiba yake

**114**.-(1) Ridhaa ya wasii ni muhimu kwa muusiwa kuwa na haki na hiba yake.

(2) Ridhaa ya wasii katika hiba inaweza kuwa yenye sharti, na kama ina sharti lile ni lile linalotimilizika na kama halitatimizwa, hakuna ridhaa.

Ridhaa kwa hiba mahsusi

**115**.-(1) Ridhaa ya wasii katika urithi mahususi itatosha kuondoa masilahi yake kama wasii, na kuiweka mali hiyo kwa muusiwa, isipokuwa kama hali au mazingira ya mali yanahitaji mali hiyo iwekwe kwake kwa namna fulani

(2) Ridhaa inaweza kuwa ya mdomo, na inaweza kuwa ya moja kwa moja au kwa kuangalia matendo ya wasii.

Ridhaa kwa hiba ya wasii mwenyewe

**116**.-(1) Ikiwa wasii ni muusiwa, ridhaa yake inatakiwa ili apate hiba yake, katika njia ileile inayotakiwa ili kukamilisha urithi kwa mtu mwingine, na ridhaa hiyo yaweza kuwa iliyo wazi au ya vitendo.

(2) Ridhaa itakuwa ya vitendo kama katika hali ya kusimamia mirathi wasii akafanya kitendo chochote kinachoashiria tabia yake kama muusiwa na si kama wasii

Madhara ya ridhaa ya wasii

**117**. Ridhaa ya wasii katika hiba itaipa utambuzi toka kifo cha marehemu.

Kuanza kwa malipo ya malipo ya mwaka kama muda haujapangwa na wosia

**118**. Ikiwa malipo ya mwaka yametolewa na wasii, na hakuna muda uliowekwa kwa kuanza kulipa, yataanza katika kifo cha marehemu, na malipo ya kwanza yatafanywa baada ya kupita kwa mwaka mmoja.

Ila wasii anaweza akalipa malipo ya awali kabla muda huo haujaisha kwa kiasi ambacho kitakuwa kimetimia wakati wa kufanya malipo hayo ya awali.

Malipo ya mwaka kama muda umepangwa

**119.** Ikiwa kuna maelekezo kuwa malipo hayo yatafanyika kwa kipindi cha robo mwaka, au kwa mwezi, malipo yatafanywa mwisho wa robo ya kwanza au mwezi wa kwanza, kama hali itakavyokuwa, baada ya kifo cha marehemu, na kama wasii akiona yafaa, yatalipwa pale muda utakapofika; lakini wasii hatabanwa kulipa mpaka mwisho wa mwaka.

Vifungu vya jumla juu ya malipo ya mwaka

**120**.-(1) Malipo ya mwaka, kama hakuna maelekezo mengine tofauti, yatajilimbikiza siku hadi siku, na kama mlipwaji wa mwaka akifa katika vipindi vya malipo, sehemu ya malipo yake yatalipwa kwa wawakilishi wake.

(2) Ikiwa kuna maelekezo kuwa malipo ya kwanza yatalipwa ndani ya mwezi mmoja au katika mgawanyo wowote wa muda baada ya kifo cha mtoa wosia, au katika siku maalumu, malipo yanayofuata yatafanywa katika maadhimisho ya siku ambapo wosia unaruhusu malipo ya kwanza yafanyike

Uwekezaji wa amana inayoruhusiwa na kanuni za uthibitisho wa wosia

**121**.-(1) Ikiwa hiba, isiyo hiba mahususi, imepewa kwa maisha, kiasi kilichorithishwa mwisho wa mwaka baada ya kifo cha mtoa wosia itawekwa katika amana kama Kanuni za Uthibitisho wa wosia zitakavyoruhusu au kuongoza, na mapato yake yatalipwa kwa waasiwa kama yatakavyokuwa yamepatikana

(2) Ikiwa hiba wazi imepewa ilipwe katika muda ujao, wasii atawekeza kiasi kinachotosheleza katika amana kama Kanuni za Uthibitisho wa Wosia zitakavyo ruhusu au kuongoza, na masilahi yatakayo patikana yatawekwa katika mapato ya mali za marehemu.

(3) Ikiwa malipo ya mwaka yametolewa na hakuna pesa za kuilipia au zilizotengwa na wosia kuilipia, kiasi kinachotosha kutoa malipo ya mwaka kitawekezwa kwa dhumuni hilo katika amana kama Kanuni za Uthibitisho zitakavyoruhusu au kuongoza.

Urithi unaotegemea tukio fulani

**122**. Ikiwa urithi unategemea kitu kitokee mbeleni ndio urithi ugawiwe wasii habanwi kuwekeza kiasi cha hiba, lakini anaweza akaihamisha mali yote iliyobaki kwa muusiwa aliyebaki (kama yupo) kama akitoa dhamana ya kutosha kulipia hiba hiyo wakati kitu hicho au muda huo ukifika

Maelekezo ya mtoa wosia juu ya uwekezaji

**123**.-(1) Ikiwa mtoa wosia amerithisha baki ya mali yake kwa mtu na kwa masiha yake yote kwa maelekezo kuwa itawekwa katika amana zilizotajwa, mali ambazo hazikuwekwa katika amana wakati wa uhai wake zitabadilishwa katika pesa na zitawekwa katika amana

(2) Mabadiliko hayo na uwekezaji utafanywa katika muda na hali kama wasii atakavyoona yafaa, na, mpaka mabadiliko hayo na uwekezaji utakapokamilika, mtu ambaye kwa muda huo angestahili pato la pesa kama uwekezaji ungeshafanyika atapata riba ya asilimia nne kwa mwaka kulingana na bei ya soko (malipo yatalipwa kama ambavyo yangetakiwa wakati wa kifo cha mtoa wosia) ya sehemu hiyo ya pesa kama bado haijawekezwa.

Watoto wanaotakiwa wapate malipo au umiliki mara moja

**124**.-(1) Ikiwa, kwa masharti ya urithi, muusia anatakiwa apate malipo au apewe pesa au kitu alichorithishwa mara moja, lakini ni mtoto na hakuna maelekezo katika wosia wa kumpa mtu yeyote kwa niaba yake, wasii au msimamizi, isipokuwa kama mali hiyo italipwa au itawekwa kwenye Muamana wa Serikali kutokana na Sheria ya Muamana wa Serikali ( Mamlaka na Majukumu), atalipa au kupeleka mali hiyo katika Mahakama ambapo uthibitisho wa wopsia, au hati ya uthibitisho wa wosia ilitolewa, kwa ajili ya muusiwa

Sura ya 33

(2) Malipo hayo katika Mahakama, yatakuwa ni malipo halali ya pesa zilizolipwa

(3) Pesa hizo, zikilipwa katika Mahakama, zitawekezwa katika ununuzi wa amana kama Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi zinavyoruhusu au kuelekeza, ambapo, riba itayopatikana, itawekwa au italipwa kwa mtu anayestahili, au vinginevyo kutumika kwa faida yake, kama Mahakama itakavyosema

(4) Ikiwa muusiwa ni kata ya Mahakama Kuu, malipo yatafanywa katika Mahakama Kuu bila kuzingatia kwamba utolewaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa wosia ulifanywa na mteule wa wilaya na bila kujali kuwa vifungu wa Sheria ya Muamana wa Serikali itatumika.

(5) Ikiwa mali inasimamiwa na msimamizi aliyeteuliwa katika SEHEMU YA VIII la Sheria hii na hiba haijalipwa au kuhamishiwa kwa Muamana wa Serikali, msimamizi atalipa au atahamisha hiba hiyo kama vifungu vya Kanuni ya Uthibitisho wa Wosia vinavyohitaji.

Utoaji wa hiba

**125**.-(1) Muusiwa wa hiba mahsusi, anatakiwa apate sehemu yake, kama lipo, baada ya kifo cha marehemu

Ila urithi mahsusi unategemea kitu au jambo litokee mbeleni ili kupata nguvu, haitahitaji, utolewaji wa mali katikati ya kifo cha mtoa wosia na wakati wa kupewa hiba: utoaji wa mali katika hali hiyo hufanya baki katika mali ya mtoa wosia

(2) Muusiwa wa mali itakayobaki atatakiwa apate mali yake kutoka kwenye mfuko wa mali baki baada ya kifo cha marehemu

Ila ikiwa mali itakayobaki urithi wake utategemeea jambo au kitu kitokee mbeleni katika masharti yake haitajumuisha kipato kinachoweza kutokana na pesa zilizorithishwa katikati ya kifo cha mtoa wosia na kukabidhiwa kwa hiba; kipato hicho hakitagawiwa

Riba ya hiba ya wazi

**126**.-(1) Ikiwa hakuna muda uliowekwa kwa malipo ya hiba ya wazi, riba itaanza kuhesabiwa baada ya mwaka mmoja ya kifo cha mtoa wosia.

Ila-

pale hiba itakapokuwa imerithishwa ili kumaliza deni, riba itaanza kuhesabiwa wakati wa kifo cha marehemu

Ikiwa kiasi kimerithishwa kwa mtoto kwa masharti ya kulipiwa kwa matunzo yake kutoka katika kiasi hicho, riba italipwa wakati wa kifo cha marehemu.

(2) Ikiwa muda umewekwa kwa malipo ya hiba ya wazi, riba italipwa katika muda uliowekwa. Riba katika muda huo itakuwa ni sehemu ya mali ya marehemu iliyobaki.

(3) Kiasi cha riba kitakuwa ni asilimia nne kwa mwaka

Riba ya malipo ya mwaka

**127**.-(1) Hakuna riba itakayolipwa katika malimbikizo ya riba katika mwaka wa kwanza baada ya kifo cha mtoa wosia, japokuwa

kipindi kifupi kabla ya kuisha kwa mwaka huo kinaweza kuwa kimewekwa na wosia kwa kulipa malipo ya kwanza ya malipo ya mwaka.

(2) Ikiwa kiasi cha pesa kimetakiwa kiwekezwe ili kupata malipo ya mwisho wa mwaka, riba ya asilimia nne italipwa kuanzia siku ya kifo cha mtoa wosia.

Baki ilipwe kwa muusiwa wa mali itakayobaki

**128.** Ziada au baki ya mali ya marehemu, baada ya kulipa madeni na wausiwa, italipwa kwa muusiwa aliyebaki kama akiwa amechaguliwa na wosia.

Kuhamisha mali kutoka Tanzania kwenda kwa wasii au msimamizi katika nchi ambayo mtoa wosia alikuwa akiishi

**129.** Ikiwa mtu hana makazi ya kudumu Tanzania amekufa na kuacha mali Tanzania na nchi ambayo alikuwa na makazi ya kudumu wakati wa kifo chake na uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi imetolewa Tanzania kuhusiana na mali zake na utolewaji wa usimamizi katika nchi aliyokuwa akiishi kuhusiana na mali zake zilizopo nchini humo, wasii au msimamizi, kama itakavyokuwa, Tanzania, baada ya kupewa notisi kama inavyotakiwa na kifungu cha 134 na baada ya kulipa madeni yote halali yaliyofikisha muda wake kama anavyoyajua, anaweza, badala ya yeye mwenye kugawa mali iliyobaki kwa watu wanaokaa nje ya Tanzania ambao wanastahili, kuhamisha, kwa ruhusa ya wasii au msimamizi, kama itakavyokuwa, katika nchi aliyokuwa akiishi marehemu, mali iliyobaki kwake kwa ajili ya ugawaji kwa watu hao.

## SEHEMU YA XIII
## URUDISHAJI WA MIRATHI

Kurudishwa kwa hiba iliyolipwa kwa agizo la Mahakama

**130**. Wasii aliyelipa mirathi kwa kuzingatia agizo la Mahakama anaruhusiwa kumuita mrithi yeyote arudishe mali kama ikitokea kuwa mali hazitoshi kuwagawia warithi wote.

Hakuna urudishwaji kama malipo yamefanyika kwa hiari

**131**. Ikiwa wasii amelipa mirathi yeye mwenyewe, hawezi akamuita muusiwa kurudisha mali kama ikiwa mali zilizopo hazitatosha kulipa wausiwa wote.

Urudishwaji pindi hiba inapofikia muda wake na uongezwaji wa muda

**132.**-(1) Ikiwa muda uliotolewa katika wosia wa kutimiza sharti umepita, bila sharti hilo kutimizwa, wasii, bila udanganyifu, akagawa mali iliyowekewa sharti hilo, katika hali hiyo, kama muda zaidi umetolewa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mtu huyo akaruhusiwa atimize sharti hilo, mali haitadaiwa kwa wasii, lakini wale ambao aliwagawia watatakiwa warudishe kiasi hicho

(2) Kama wosia ukitaka muusiwa afanye kitu kwa muda uliotolewa, aidha kama sharti la kutimizwa ili apewe urithi wake au kama sharti ambalo lisipotimizwa bali mali ya urithi itapewa kwa mtu mwingine, au urithi utakuwa haina nguvu, kitu hicho ni lazima kifanywe kwa muda uliopangwa, isipokuwa kama ufanywaji wake

utazuiliwa kwa udanganyifu, na katika hali hiyo muda wa kutimiza utaongezwa kufuatiwa udanganyifu huo.

Pindi wausiwa wanapotakiwa warudishe kwa usawa

**133**. Kama wasii amelipa mali za urithi, na baadaye anatakiwa kulipa deni ambalo hakulijua mwanzo, anaruhusiwa kuwaita wausiwa warudishe kiasi kilicho sawa.

Mgawanyo wa mali

**134**.-(1) Ikiwa wasii au msimamizi ametoa notisi kama inavyotakiwa na Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi, kwa wadeni na wengine wamtumie madai yao dhidi ya mali ya marehemu, muda wa kuleta madai ukiisha, atakuwa huru kugawa mali, au sehemu ya mali, katika kulipa madai halali anayoyajua, na hatakuwa na hatia kwa mali zilizogawiwa kwa mtu yeyote ambaye hakujua dai lake wakati wa ugawaji

(2)Kifungu hiki hakitazuia mdai au mlalamikaji yeyote kufuata mali, au sehemu ya mali, zilizopo kwa mtu aliyepokea mali hizo.

Pale ambapo wadai watamuita muusiwa arudishe

**135**. Mdai ambaye hajapokea malipo yake anaweza akamuita muusiwa ambaye amepokea mali arudishe, ikiwa kama mali za marehemu zilitosha ama hazikutosha wakati wa kifo chake kulipa madeni pamoja na warithi, na ikiwa kama malipo yalifanywa na wasii mwenyewe au la.

Haki ya wausiwa kuwataka wausiwa wengine warudishe

**136**.-(1) Ikiwa mali zilikuwa zinatosha kuwagawia wausiwa wote wakati wa kifo cha mtoa wosia muusiwa ambaye hajapokea urithi wake au ambaye ametakiwa arudishe, katika kifungu cha 135, hawezi akamtaka muusiwa ambaye amepokea mali yake kurudisha, ikiwa mali ililipwa kwake katika shitaka au la, hata kama mali zimekuwa chache kwa upotevu uliofanywa na wasii.

(2) Kama mali zilikuwa hazitoshi kuwalipa wausiwa wote wakati wa kifo cha mtoa wosia, muusiwa ambaye hajapokea urithi wake lazima, kabla hajamuita muusiwa yeyote kurudisha, amwendee wasii kama bado ana mali; lakini kama wasii hana mali au hatakiwi kulipa, muusiwa ambaye hajaridhika atawataka wausiwa wote walioridhika warudishe kwa usawa

(3) Urudishaji wa muusiwa mmoja kwenda kwa mwingine hautazidi kiasi ambacho mali ingetakiwa ipunguzwe kama mali zingegawiwa ipasavyo

Marudisho hayana riba

**137**. Urudishaji wa mali, hautakuwa na riba.

SEHEMU YA XIV

UHARIBIFU NA UFUJAJI WA MALI

Mashitaka kwa ufujaji

**138.** Pale wasii au msimamizi atatumia vibaya mali za marehemu, au akaiweka katika hatari ya kupotea au kuharibika, atapaswa kulipa hasara hiyo au uharibifu huo uliojitokeza

Mashitaka kwa kutojali

**139.** Pale wasii au msimamizi anasababisha hasara katika mali kwa kukataa kuwa sehemu ya mali ya marehemu, atapaswa kulipa fidia.

## SEHEMU YA XV
## USIMAMIZI WA MALI YA WAKFU
[R.L. Sura ya 326]

Tafsiri

**140**. Katika SEHEMU hii, isipokuwa kama maana itahitaji-

"kamishna" inamaanisha mwanachama wa Tume ya Wakfu aliyechaguliwa katika kifungu cha 142 cha Sheria hii.

"Muamana/kabidhi" inajumuisha mtu yeyote, aidha peke yake au pamoja na mwingine, anayesimamia kitu chochote sambamba na wakfu au kupokea kodi au fidia

"Wakfu" ina maanisha tunu au kujitoa katika Sheria za Kiislamu katika kitu chochote ndani ya Tanzania kwa ajili ya dini, neema au tunu kwa dhumuni au kwa matunzo na msaada kwa mtu yoyote wa familia ya mtu aliyepewa kitu hicho

"Tume ya Wakfu" ina maanisha Tume wa wakfu ya Tanzania iliyowekwa katika kifungu cha 142 ya Sheria hii.

Wakfu kuwa halali na wenye nguvu
Sura ya 114

**141**. Bila kujali vifungu katika Sheria ya ardhi na uhalalishwajina Sheria yeyote inayohusika Tanzania, mtu yeyote aliyeweka wakfu baada ya tarehe ambapo Sheria hii itaanza kutumika, kwa kutumia vifungu vya Sheria zilizotajwa na Sheria zilizotumika, wakfu utakuwa madhubuti na halali, hautakuwa kinyume na Sheria, dhoofu au batili na vifungu vyovyote vya Sheria iliyosemwa au Sheria inayotumika ambayo itaufanya wakfu huo uwe dhoofu au batili havitakuwa na nguvu.

Kuanzishwa kwa Tume ya Wakfu

**142**.-(1) Kinaanzishwa chombo kitakachojulikana na Tume ya Wakfu Tanzania

(2) Tume ya Wakfu itajumuisha watu wasiopungua nane watakao chaguliwa na Rais ambapo watu wasio pungua watano watakuwa Waislamu.

(3) Rais atamchagua mwenyekiti na katibu kutoka katika wanachama wa Tume ya Wakfu.

(4) Wanachana wa Tume ya Wakfu wataitumikia ofisi kwa kipindi chote Rais atakapokuwa madarakani

(5) Hakuna mwenendo au kitendo chochote cha Tume ya Wakfu kitakachobatilishwa kwa sababu ya kuwepo kwa upungufu wa wanachama wakati wa mwenendo huo au kitendo hicho.

Tume ya Wakfu itakuwa ni mamlaka inayojitegemea na itakuwa na muhuri

**143**.-(1) Tume ya Wakfu itakuwa ni kampuni, ambayo ina maisha ya muendelelezo, na mhuri wa moto na yenye mamlaka ya kupata, kumiliki au kujipatia mali aidha inayohamishika, au isiyo hamishika, na itakuwa na mamlaka yote, majukumu na kazi kama zitakavyokuwa zimewekwa na Sheria hii

(2) Tume ya Wakfu inaweza ikashitaki au kushitakiwa kwa jina la kampuni na inaweza kwa madhumuni yote kutajwa kwa jina hilo.

(3) Mhuri wa Tume ya Wakfu, ambavyo utakuwa wa namna

kama ambavyo Rais atathibitisha, itathibitishwa na saini ya mwenyekiti, au kamishna ambaye siye katibu aliyeruhusiwa kumwakilisha, na katibu, na mhuri huo utajulikana kiofisi na kimahakama.

(4) Nyaraka zote (zaidi ya zile zinazohusika na ardhi ambazo zitathibitishwa na mhuri wa moto wa Tume ya Wakfu) zinazotengenezwa, na maamuzi yote ya, Tume ya Wakfu yanaweza yakathibitishwa kwa mkono wa mwenyekiti, na kamishina aliye thibitishwa kumwakilisha, au katibu.

Mikutano na akidi

**144**.-(1) Tume ya Wakfu itafanya mkutano japo mara moja katika kila miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti ataongoza mikutano yote ya Tume ya Wakfu ambayo atakuwapo na kama asipokuwapo katika mkutano, makamishna waliopo watamchagua kamishna aongoze mkutano.

(3) Akidi ya Tume ya Wakfu itakuwa watu wanne ambao mmoja atakuwa aidha mwenyekiti au katibu.

Masijala ya mali za wakfu na amana Agizo namba 9 la 1956

**145.**-(1) Waziri anaweza kutoka kipindi fulani hadi kingine kwa kutumia notisi katika gazeti kuagiza kuwa kifungu hiki kitatumika katika sehemu yoyote Tanzania iliyoelezwa katika maelekezo hayo, na ikiwa hivyo kifungu hiki kitatumika kama inavyoelezwa

(2) Kama maelekezo yametolewa, kama inavyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha sehemu hii sehemu hii itatumika katika wakfu zifuatazo (ambazo zitajulikana kama wakfu zilizosajiliwa), na hii ni kusema kwamba-

(a) Wakfu yoyote ambayo mali yote au sehemu ya mali inajumuisha mali isiyohamishika, yote au sehemu iliyo katika sehemu yote au kipande cha sehemu ambapo kifungu hiki kimetumika; na

(b) Wakfu yeyote ambayo wadhamini wanakaa katika eneo ambalo kifungu hiki kimetumika

(3) Aidha wakfu imekuwa wakfu iliyosajiliwa, itaendelea kama wakfu iliyosajiliwa bila kujali mabadiliko yoyote katika hali ya kitu kilichomo, au hali iliyopo, au badiliko katika hali ya kawaida ya wadhamini hao;

(4) Tume ya Wakfu itaweka, maelezo kama itakavyoelezwa, orodha ya mali zote zilizo chini ya wakfu iliyosajiliwa pamoja wadhamini wote wa mali hiyo.

(5) Kila mdhamini wa mali iliyopo chini ya wakfu iliyosajiliwa, ndani ya miezi mitatu ya tarehe ambapo itakuwa ni wakfu iliyosajiliwa, ataiomba Tume ya Wakfu kuisajili wakfu hiyo, na maombi hayo yatakuwa katika fomu, na yatajumuisha maelezo yote na yataambatana na malipo yote yanayotakiwa.

(6) Kila mdhamini wa mali iliyoko chini ya wakfu iliyo sajiliwa, ndani ya miezi mitatu tangu iwe wakfu iliyosajiliwa au tangu awe mdhamini, ataomba tume ya wakfu asajiliwe, na maombi hayo yatakuwa katika fomu na yataambatanishwa na ada inayotakiwa.

(7) Ikiwa mtu ameacha kuwa mdhamini wa mali iliyoko chini ya wakfu iliyosajiliwa mtu huyo, ndani ya mwezi mmoja kabla hajaacha kuwa mdhamini, ataitaarifu tume ya wakfu kuwa anaacha kuwa mdhamini, na atajulikana kama mdhamini mpaka tume ya wakfu itakapojulishwa:

Isipokuwa-

(a) mtu huyo amecha kuwa mdhamini kwa sababu ya kifo chake, mtu aliyemrithi udhamini atatoa taarifa zinazohitajika katika hiki kifungu kidogo;

(b) Ikiwa kuna mdhamini zaidi ya mmoja wa mali iliyo chini ya wakfu iliyosajiliwa, taarifa inayohitajika katika kifungu hiki kidogo itatolewa na mdhamini aliyebakia.

(8) Katibu wa Tume ya wakfu, kwa cheti kitakachotolewa na kilichotiwa saini na yeye, atajulisha kila badiliko litakalofanyika katika wadhamini wa mali iliyo chini ya wakfu iliyosajiliwa-

Sura ya 334

(a) katika suala la mali inayohusiana na ardhi iliyosajiliwa katika Sheria ya Usajili wa Ardhi, au Sheria yoyote itakayo irekebisha au itakayokuja badala ya hiyo kwa msajili wa hati;

(b) kuhusu mali nyingine yoyote inayohusu ardhi ambayo haijasajiliwa, kwa msajili wa nyaraka,

Na kila hati husika itaeleza kinagaubaga ardhi inayohusika

(9) Ada zote zilizoelezwa katika jedwali la tano la Sheria hii, ambayo ni ya usajili au mali, zilizopo chini ya wakfu iliyosajiliwa na kwa ajili ya usajili wa wadhamini zitatozwa na Tume ya wakfu na kuwekwa katika mfuko utakaoitwa Mfuko wa Usimamizi.

(10) Mdhamini yoyote ambaye, bila sababu za kuaminika, akishindwa kutekeleza maelezo ya vifungu vidogo vya (2) au (3) vya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai katika Sheria hii

Tume ya Wakfu inaweza kufanya uchunguzi na kuchukua usimamizi wa wakfu

**146**.-(1) Ikitokea katika Tume ya wakfu kuwa-

(a) hakuna mdhamini wa wakfu aliyewekwa; au

(b) mdhamini yeyote ambaye amefanya au anafanya katika hali ambayo si sahihi, haijaruhusiwa au si halali; au

(c) badiliko katika usimamizi wa wakfu ni muhimu kwa ajili ya wakfu hiyo,

Tume ya Wakfu inaweza, kwa uamuzi wake yenyewe, au uamuzi wa mtu yeyote aliye na maslahi na wakfu hiyo, kufanya uchunguzi. Notisi ya uchunguzi huo itatolewa, kwa namna ambayo inakuwa inatakiwa, kwa watu wote wenye masilahi na wakfu na watu hao wataalikwa kwa notisi hiyo ili waje kutoa ushahidi mbele ya tume ya wakfu

(2) Baada ya kufanya uchunguzi huo, tume ya wakfu ikigundua kuwa hakuna mdhamini wa wakfu, au mdhamini yeyoye amefanya au anafanya katika hali ambayo si sahihi, haijaruhusiwa, au si ya kihalali, au mabadiliko katika usimamizi wa wakfu utakuwa wa faida katika

wakfu, tume ya wakfu itatoa agizo aidha mali iliyoko chini ya wakfu itasimamiwa na wakfu tume au kumchagua mtu au watu awe/ wawe mdhamini/wadhamini wa wakfu na agizo hilo litasema mali ambayo inahusika.

(3) Baada ya kutoa agizo katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki-

(a) kutangaza kuwa mali iliyochini ya wakfu itasimamiwa na tume ya wakfu, mali hiyo itakuwa sambamba na Sheria yoyote inayohusika na usajili wa ardhi kwa muda itakayo kuwa na nguvu, itawekwa chini ya tume ya wakfu;

(b) kumchagua mdhamini mpya au wadhamini wa wakfu, mali iliyo chini ya wakfu itaenda sambamba na Sheria yoyote inayohusiana na usajili wa ardhi kwa muda itakaokuwa na nguvu, kuwa chini ya msimamizi au wasimamizi wapya.

Isipokuwa maelezo ya kifungu kidogo hakitatumika katika hali ambayo agizo lililowekwa na tume ya wakfu limebadilishwa katika rufaa katika kipengele kidogo cha (5) cha kifungu hiki.

(4) Katibu wa tume ya wakfu atatuma nakala iliyothibitishwa na saini yake ya agizo lolote katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kwa msajili wa hati ikiwa agizo linahusu ardhi yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa ardhi au Sheria yoyote itakayobadilisha, au kuja badala yake na msajili wa nyaraka kama agizo litahusu ardhi yoyote ambayo haijasajiliwa.

Sura ya 334

(5) Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na agizo la tume ya wakfu katika kifungu hiki anaweza akakata rufaa katika baraza la rufaa, litakalo chaguliwa na Rais kwa ajili hiyo, kuwezesha kusikilizwa kwa suala hilo na baraza la rufaa, na uamuzi wa baraza la rufaa utakuwa wa mwisho na wenye hitimisho

(6) Mtu yeyote anayekata rufaa katika baraza la rufaa katika kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki atakuwa na haki ya kutokea au kuwakilishwa na wakili mbele ya baraza la hukumu katika usikilizwaji wa rufaa hiyo.

Wadhamini wa wakfu wanaweza wakaitwa kutoa ushahidi wa usimamizi mzuri wa amana

**147**.-(1) Tume ya wakfu wakati wowote itamuita mdhamini wa mali ya wakfu kuja kuiridhisha kama mali inasimamiwa vizuri na inaweza ikamuhitaji mdhamini atoe nyaraka au vitabu, aidha vya mahesabu au vinginevyo, anavyovimiliki au vilivyoko chini ya ulinzi wake vinavyohusu mali hiyo.

(2) Mdhamini yeyote atakayeshindwa kutimiza kigezo cha kutoa nyaraka au vitabu alivyonavyo au vilivyoko katika himaya yake kama inavyotakiwa na tume ya wakfu katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai tofauti kinyume na Sheria hii.

Mikataba na

**148.** .Hakuna mkataba au makubaliano ya aina yoyote

makubaliano Fulani yanayohusu wakfu lazima isibitishwe na tume ya wakfu

yanayohusu kuuza au vinginevyo kuchukua kitu chochote kilichopo chini ya wakfu au kutaka kuweka rehani kitu hicho au kutaka kupangisha kitu hicho kwa muda unaozidi mwaka mmoja utakuwa na nguvu isipokuwa ruhusa ya maandishi kutoka katika tume ya wakfu kutolewa kwanza.

Mali ya wakfu haitapatikana kwa maagizo au kwa kabidhi pingamizi baada ya kuanza kwa sehemu hii

**149.** Bila kuathiri kitu chochote tofauti na Sheria hii au Sheria itakayo kuwa na nguvu kwa muda huo, hakuna hati ya mali yoyote iliyopo chini ya wakfu, baada ya kuanzishwa kwa sehemu hii, itachukuliwa na mtu yeyote kwa sababu ya pingamizi au kwa sababu yoyote Sheria ya maagizo.

Namna mali ya wakfu itakavyosimamiwa

**150**.-(1) Sambamba na kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki mali zote zilizo chini ya wakfu ambazo zinasimamiwa na wakfu tume zitasimamiwa kwa kuzingatia nia ya muwekaji wa wakfu kama nia hizo ni halali katika Sheria za Kiislamu na zinaweza kufanikishwa, na ikiwa nia hizo zinaweza zikathibitishwa kwa kuangalia mila au ushahidi wowote unaopatikana kihalali.

(2):Katika hali ambayo katika wazo la tume ya wakfu, nia ya mtoa wakfu si halali, au haithibitiki au haiwezi kutimilika au kama mapato ya ziada yamebaki baada ya kutimiza nia ya mtoa wakfu, tume ya wakfu itatumia mali iliyo chini wa wakfu au mali ya ziada au mapato hayo, kwa ajili ya dini, tunu au kwa dhumuni la msaada kwa ajili ya Waislamu kama tume ya wakfu itakavyoona ni sawa.

Ila haitakuwa halali kwa tume ya wakfu kutumia mali yoyote, au mali ya ziada, au mapato katika hiki kifungu kidogo kwa dhumuni linalohusiana na wakfu nyingine kwa sababu tu kuna mali yoyote katika wakfu hiyo ya kwanza

Tume ya Wakfu inaweza ikauza mali ya wakfu katika hali Fulani

**151.** Kama itaonekana kwa tume ya wakfu kuwa nia yoyote ya mtoaji haitaweza kufanikishwa na kwamba ni vema kuwa mali au sehemu ya mali iliyowekwa chini ya wakfu ipangishwe, kubadilishwa au kuuzwa, tume ya wakfu itafanikisha mali hiyo au sehemu yake kupangisha, kubadilishwa au kuuzwa kama inavyotakiwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 150 cha Sheria hii.

Ruhusa inatakiwa kujenga au kuanzisha makaburi

**152.**-(1) Hakuna mtu ambaye ametoa mali kama wakfu au mdhamini wa kitu hicho atajenga au atasababisha kujengwa kwa msikiti au ataanzisha au kusababisha kuanzishwa kwa makaburi isipokuwa, kabla ya hapo amepata ruhusa ya tume ya wakfu kwa niaba hiyo, na ameiridhisha tume ya wakfu kuwa msikiti huo au makaburi hayo yametunikiwa au yatatunikiwa kwa hali inayoridhisha kwa utunzwaji wake na kuyaweka katika hali nzuri.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutimiza maelezo ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai tofauti na Sheria hii.

Ada

**153**.-(1) Kama mali yoyote ambayo iko chini wa wakfu inasimamiwa na tume ya wakfu, itatozwa ada kama itavyokuwa

inatakiwa

(2) Pesa zinazopatikana kutoka kwenye ada hizo zitatumiwa na tume ya wakfu katika shughuli za kila siku za Tume ya Wakfu.

(3) Kama baada ya miezi kumi na mbili ada hiyo itazidi matumizi ya kila siku ya tume ya wakfu, ziada itapewa kwa mfuko wa msaada wa tume ya wakfu.

(4) Mfuko wa msaada wa Tume ya Wakfu utatumia pesa hizo kwa ajili ya kutoa misaada kama tume ya wakfu itakavyoona inafaa.

Hesabu na Ukaguzi wa mahesabu

**154**. Tume ya Wakfu inaweka mahesabu sawa ya mali zote na pesa zinazopokelewa na mahesabu yatakaguliwa na mkaguzi aliyethibitishwa na rais kwa muda huo kama waziri atakavyoongoza.

Akaunti za benki

**155.** Tume ya Wakfu itafunguaa akaunti ya benki au hesabu za kibenki ambayo pesa zote zinazopokelewa na tume ya wakfu zitawekwa na pesa zote zitakazothibitishwa na tume ya wakfu zitatolewa. Akaunti hizo zitakuwa zinatunzwa na mwenyekiti, au kamishna aliyethibitishwa kwa niaba ya tume ya wakfu, na katibu

Sheria ya zuio la kodi haitatumika katika mali ya wakfu (Sura ya 339)

**156**. Vifungu vya sheria ya zuio la kodi, au sheria yoyote itakayoirekebisha au kuibadilisha, haitatumika katika mali yoyote ya wakfu ambayo inasimamiwa na tume ya wakfu kwa kufuatana na vifungu vya sheria hii

Adhabu

**157**. Mtu yeyote atakayefanya kosa katika Sheria hii akipatikana na hatia atatakiwa kulipa fidia isiyozidi shilingi elfu mbili tu au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote fidia na kifungo.

Kanuni

**158**.-(1) Waziri ataweka kanuni kwa kanuni zote au kwa dhumuni hili-

(a) Kuweka mwenendo utakaofuatwa na tume ya wakfu katika ufanyaji wa kazi zake, majukumu na kazi katika vifungu vya Sheria hii, ikijumuishwa na ukaimu wa majukumu, kazi na mamlaka au moja kati ya hizo, zaidi ya zile zilizotajwa katika kifungu cha 146, kwa mtu yeyote au watu.

(b) Kuweka muda na namna ya kukata rufaa katika mabaraza ya rufaa, ada itayotakiwa kulipwa, na mwenendo mzima utakao fuatwa katika rufaa hiyo;

(c) Kuwa kitu chochote kinachotakiwa kuwekwa katika viungu vya Sheria hii;

(d) Kwa ujumla wake, katika kuvitekeleza vizuri vifungu vya Sheria hii

(2) Kanuni zitakazotengenezwa na kifungu hiki kitatoa kuhusiana na uvunjifu wa vifungu vyake, fidia ambayo haitazidi fidia iliyowekwa katika kifungu cha 157 cha Sheria hii.

## SEHEMU YA XVI
## MALI ZA KIISLAM (MALIPO YA SADAKA)

Busara ya Afisa wa Wilaya kufanya malipo

**159**. Katika hali yoyote ambapo, katika Sheria za Kiislamu, mali yote au sehemu yake inalipwa katika hazina (Beit-el-Mal), afisa wa wilaya anaweza, kwa busara yake , kuagiza kuwa mali yote au sehemu ya kiasi cha mali kilipwe lakini kisizidi shilingi elfu moja, itakayogawiwa, kwa usawa kama atakavyoona inafaa, baina ya mume, mke au wake, au wategemezi wengine wa marehemu.

Ila ikiwa mali ni ya aina ambayo Sheria hii inatumika, afisa wa wilaya hatatoa agizo katika kifungu hiki bila kuwa na ruhusa ya Mahakama ambayo ina mamlaka katika usimamizi wa mali au, kama mali inasimamiwa na kabidhi-wasii

## SEHEMU YA XVII
## MENGINEYO

Vifungu vinavyotumika kwa msimamimizi aliyeambatanishia wasii

**160**. Katika sehemu ya XII na XIII vifungu vinavyomhusu wasii vitatumika pia kwa msimamizi aliyembatanishwa na wosia.

Matunzo ya wosia wa watu walio hai

**161**. Sambamba na vifungu vya kanuni za uthibitisho wa mirathi, wosia wa mtu aliye hai unaweza ukatunzwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na kila wosia uliotunzwa utahifadhiwa katika masijala chini ya uangalizi na maelekezo ya Mahakama Kuu.

Hati ya kiapo kama ni shirika la amana

**162**. Afisa yeyote aliyethibitishwa kwa dhumuni na shirika la amana au mkurugenzi au mwanachama wa serikali anaweza, kwa niaba ya shirika, kuchukua kiapo, kuapa katika hati ya kiapo, kutoa dhamana au kufanya kitu chochote au kitu ambacho Mahakama itahitaji kwa ajili ya kuipa shirika uthibitisho wa wosia au usimamizi, na vitendo vya afisa aliyethibitishwa, mkurugenzi au mwanachama, vitaibana shirika hilo

Uhalali wa ugawaji katika wosia na haki ya matunzo

**163.** Hakuna kitu katika Sheria hii kitakacho-

(a) halalisha mirathi yoyote ambayo vinginevyo ingekuwa ni batili

(b) itabatilisha ugawaji wowote ambao vinginevyo ungekuwa wa halali; au

(c) Kumnyima mtu yeyote haki yoyote ya matunzo ambapo vinginevyo angepewa.

Marekebisho

**164.** [Marekebisho ya baadhi ya Sheria]

Sheria Fulani kutotumika

**165**.-(1) Sheria zilizotolewa kama sehemu ya kwanza ya jedwali la kwanza hazitatumika Tanzania kwa kiasi kilichoelezwa katika safu ya nne ya jedwali hilo

(2) [Kufutwa kwa baadhi ya Sheria]

**166**.-(1) Muendelezo wa Sheria zinazohusu utolewaji wa

Mabakisho

uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi, uchaguzi wa wasimamizi na usimamizi wa mali hautaathiriwa kwa kufutwa au kutotumika kwa ingizo lolote au kutotumika kwa vifungu vya jedwali la kwanza na la pili, na kama kuna ombi limefanywa la utoaji au uchaguzi katika ingizo hilo au vifungu au usimamizi wa mali yoyote umeanza, utaendelea kwa kufuata vifungu vya Sheria hii.

Sura ya 28

Sura ya 30

(2) Matoleo yote ya uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi yaliyofanywa Tanzania chini ya Sheria ya Mirathi ya India , 1865, au Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi ya India, 1881, kila uchaguzi wa wasimamizi katika sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache), kila usajili wa mirathi katika sheria ya Uthibitisho wa Wosia (Kupiga tena Mhuri) na kila agizo na maelekezo yaliyotolewa na Mahakama yenye mamlaka Tanzania chini ya Sheria zilizotajwa yatakuwa na nguvu kama vile yalifanywa katika vifungu vinavyohusika na Sheria hii, lakini bila kuathiri ujumla wa yaliyosemwa, uchaguzi wa msimamizi wa marehemu aliyekuwa mwafrika chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache) utakuwa na nguvu bila kujalisha kama thamani ya mali inazidi thamani ile ya mali chache.

(3) Bila kujalisha ufutwaji au kutotumika kwa Sheria yoyote au vifungu vyovyote vilivyopo katika jedwali la pili na la tatu-

Supp.58

(a) uchaguzi wa mteule wa wilaya;
(b) kanuni za usajili wa mirathi

Sura ya 28
Ukurasa wa 6

(c) kanuni za usimamizi wa mali chache

Supp.57

(d) agizo au muongozo uliotolewa katika kifungu cha 17 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache)

Sura ya 30
p.10

(e) Sheria ya Usimamizi wa Mali Chache

R.L.Cap.315
Sura ya 315

(f) Ruhusa iliyotolewa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi kwa Mashirika

Vitasemekana vimefanyika, vimetolewa au vimepewa, kama hali itakavyokuwa, katika vifungu sahihi vya Sheria hii

Vifungu vya mpito

**167**.-(1) Kama amana zimesajiliwa kwa jina la kundi la watu au mashirika.kwa niaba ya shirika la amana au ardhi au dhamana ambayo imesajiliwa kwa jina la kundi la watu au mashirika.amana hizo, ardhi au dhamana zitahamishwa kutoka kwenye kundi hilo la watu au mashirika .kwenda kwenye shirika au kama shirika litakavyoagiza

Ila hakuna hamisho litakalochukuliwa kama ni uvunjwaji wa maagano au sharti la kutochukua au litakalopelekea kunyang'anywa

(2) Ikiwa maombi yamefanywa katika Mahakama Kuu katika sehemu hii ya kusajili mirathi au hati za usimamizi katika sehemu ya X kuhusu mali za mtu aliyekufa kabla ya tarehe 20, oktoba, 1959 Mahakama Kuu kabla ya kusajili itajiridhisha kuwa kodi ya mirathi

imelipwa au dhamana juu ya malipo yake yametolewa kwa kamishina wa kodi za mirathi kama inavyotakiwa na kodi za mirathi Tanzania.
Ila kifungu hiki kidogo hakitatumika ikiwa maombi yanafanywa na au kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu

(3) Ikiwa mtoa wosia amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni na amerithisha mali ambayo itatoa riba chini ya vifungu vya sheria hii isipokuwa kifungu namba 130 au 312, ya Sheria ya Mirathi ya India ya mwaka 1865 kisha bila kujali kifungu cha 126 cha sheria hii vifungu vya Sheria hii vitaendelea kutumika.

(4) Ikiwa mtu ambaye mali zake zinasimamiwa chini ya vifungu vya mali hii, amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni, maneno ya aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 109 cha Sheria hii yatasomwa kana kwamba maneno "miezi mitatu" yamebadilishwa na maneno "miezi minne"

(5) Ikiwa mtu, mali zake, zinasimamiwa kufuatana na vipengele vya Sheria hii, amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni, na riba yoyote imelipwa chini ya vifungu vya 132,126 au 127 vya Sheria hii kwa kipindi baada ya tarehe hiyo, riba hiyo italipwa kwa kiasi kinachotajwa na Sheria hii katika tarehe hiyo.

Kubaki kwa mamlaka ya kabidhi wasii- muamana wa serikali
Sura ya 27
Sura ya 31

**168.** Sambamba na kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 124, hakuna kitu chochote katika Sheria hii kitatafsiriwa kukataza vifungu vya Sheria ya Kabidhi Wasii (Mamlaka na Kazi) au Sheria ya Muamana wa Serikali (Mamlaka na Kazi) au kuathiri haki, majukumu au upendeleo wa kabidhi wasii au muamana wa serikali au msaidizi wa kabidhi wasii.

JEDWALI LA KWANZA

NCHI AMBAZO KATIKA KIFUNGU CHA 7 KITATUMIKA

(Kifungu cha 7(6))

Muungano wan chi za Amerika
Jamhuri ya watu wa Italia
Jamhuri ya watu wa Ufaransa
Muungano wa nchi za Mexico
Shirikisho la Jamuhuri ya watu wa Ujerumani
Ufalme wa nchi za Norway
Ufalme wa nchi za Misri.
Ufalme wa Swideni

JEDWALI LA PILI

(Kifungu cha 16 (6))
[ Imefutwa .]

R. L. Cap. 445 s.141
Sura ya 445 kifungu 141

JEDWALI LA TATU

SHERIA ZILIZOFUTWA

SEHEMU YA I

| Mwaka | Namba. | JINA | kiasi kilichofutwa |
|---|---|---|---|
| 1865 | X | Sheria ya Mirathi ya India | sehemu ya XXIX mpaka XL (kwa pamoja) na kifungu cha 333. |
| 1881 | V | Sheria ya kihindi ya uthibitisho wa wosia na usimamizi | Sheria yote. |

SEHEMU YA II

[Imefutwa ]

## JEDWALI LA NNE

## UCHAGUZI WA MSIMAMIZI WA MALI CHACHE

## SHERIA YA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI (SURA YA 352)

(Kifungu cha 6)

Katika Mahakama ya ..........................................................................................
Usimamizi wa mirathi wa ……………………………………………………….
Leo.........................................siku ya.........................20…………………
nilichaguliwa kuwa msimamizi wa mirathi ( au wa mali zilizotajwa hapa chini) za marehemu aliyefariki katika ............................siku ya....................20................
Nitasimamia mali za marehemu vizuri na kwa uaminifu kama inavyoonyesha hapa chini.
(nakala ya wosia wa marehemu umeambatanishwa na mali itasimamiwa kama inavyotakiwa)

....................................................
*(Sahihi na cheo cha afisa wa Mahakama)*

Mimi (sisi) tunaapa na kusema kuwa mimi( sisi) nita/tutasimamia vizuri na kwa uaminifu mali za marehemu aliyetajwa, kwa kulipa madeni yake yaliyofikia muda, na kugawanya baki ya mali hiyo kama Sheria inavyosema, na nita(tuta) tunza hesabu za kweli za shughuli zote zinazohusu mali hiyo na kuzitoa mbele ya Mahakama muda wowote zinapotakiwa.
Leo.....................siku ya...................20........................

...............................................
(Sahihi ya msimamizi)

## JEDWALI LA TANO

## SURA YA 352

## SHERIA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

[SHERIA KUU]

### MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Kichwa cha Habari*

### SEHEMU YA I

### VIFUNGU VYA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria na Matumizi
2. Tafsiri.

### SEHEMU YA II
### MAMLAKA YA MAHAKAMA KATIKA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

3. Mamlaka ya Mahakama Kuu katika uthibitisho wa wosia na usimamizi wa mirathi.
4. Mamlaka ya Mahakama Kuu katika kusajili mirathi.
5. Mamlaka ya mteule wa Wilaya.
6. Mamlaka ya Mahakama za Wilaya.
7. Afisa wa ubalozi.
8. Madaraka chini ya Sheria hii yanaweza kwa usiri.
9. Kanuni za uthibitisho wa wosia.

### SEHEMU YA III
### ULINZI WA MIRATHI KABLA YA IDHINI YA KUIGAWA NA WASII WAKUJITIA.

10. Mpokeaji kabla ya kutolewa kwa idhini.
11. Kuuza kwa amri ya Mahakama.
12. Matumizi ya kanuni kwa wapokeaji mirathi.
13. Adhabu kwa kudharau Mahakama.
14. Hakuna mashtaka dhidi ya mpokeaji mirathi.
15. Haki tangulifu ya mpokeaji
16. Wasii wakujitia.

17. Uwajibikaji wa wasii aliyejiteua.

SEHEMU YA IV
KUKANA KWA WASIMAMIZI WA MIRATHI.

18. Kanusho la dhahiri la haki ya uthibitisho wa wosia.
19. Dondoo na kukataa kwa vitendo.
20. Madhara ya kukana.

SEHEMU YA V
UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI.

*A. Jumla*

21. Mashirika ya amana
22. Idadi ya wasii na wasimamizi
23. Watoto na watu wasio na akili nzuri

*B. UTHIBITISHO WA MIRATHI*

24. Utoaji wa uthibitisho wa wosia
25. Uthibitisho wa wosia kwa kutumia nakala, hawala, au maandishi ya wosia ulioandikwa au maandishi ya wosia wa mdomo
26. Kibadilisho cha Wosia inachoonekana baada ya mirathi kuthibitishwaa
27. Nakala ya wosia iliyothibitishwa nchi za nje
28. Madhara ya uthibitisho wa wosia

*C. Hati za usimamizi zilizoambatanishwa na wosia*

29. Ushindwa kwa wasii
30. Wakala wa wasii ambaye hayupo
31. Wakala wa mtu anayetakiwa kupewa hati za usimamizi
32. Kibadilisho wosia kinachopatikana baada ya hati za usimamizi kutolewa

*D. Hati ya usimimizi kwa mtu aliyefariki bila kuacha wosia*

33. Hati ya usimimizi kwa mtu aliyefariki bila kuacha wosia
34. Wakala wa mtu anaetakiwa kupewa usimamizi

*E. Hati za usimamizi kwa dhumuni maalumu*

35. Mpaka wosia upatikane
36. Wakati wa utoto
37. Wakati akili siyo nzuri
38. Kusubiri utowaji wa usimamizi

39. Kukusanya na kutunza mali
40. Mashtaka
41. Mali iliyochini ya amana

*F. Utoaji kwa kiasi*

42. Utoaji wa kiasi
43. Utoaji kwa kiasi kilichobaki

*G. Madhara ya utolewaji wa hati za usimamizi*

44. Madhara ya utolewaji wa hati za usimamizi

*H. Kifo cha wasii au wasimamizi na kuisha kwa muda katika utolewaji wenye kikomo*

45. Kifo cha mmoja kati wa wawakilishi
46. Kifo cha mwakilishi mmoja au mwakilishi aliyebakia
47. Kuisha kwa muda wa utolewaji wenye kikomo

SEHEMU YA VI
KUBATILISHWA NA KUBADILISHA TOLEO NA UONDOAJI WA WASII AU WASIMAMIZI

48. Kubadilisha makosa
49. Kubatilishwa kwa toleo na uondoaji wa wasii
50. Malipo ya wasii au msimamizi aliyebatilishwa
51. Kurudishwa kwa toleo lililobatilishwa

SEHEMU YA VII
MAZOEA NA MUONGOZO KATIKA UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI (TOFAUTI NA ZILE ZA MALI CHACHE)

52. Mwenendo mahakamani.
53. Ombi kwa Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya.
54. Mteule wa wilaya kusimamisha mwenendo wa kesi na kuipa taarifa Mahakama Kuu katika hali itakayojitokeza
55. Uombaji wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na na wosia
56. Maombi ya hati za usimamizi
57. Uthibitisho wa maombi
58. Pingamizi dhidi ya utoaji wa uthibitisho wa mirathi au usimamizi
59. Mwenendo wa kesi bayana ya pingamizi
60. Amri ya kutoa vidhibiti vya wosia

61. Mahakama inaweza ikamtafiti muombaji, kuhitaji ushahidi mwingine au kutoa wito
62. Muda kabla utolewaji wa usimamizi wa mirathi haujafanywa
63. Utoaji wa uthibitisho wa mirathi na usimamizi
64. Kukataliwa kwa hati za usimamizi wa mirathi
65. Maelekezo kwa wasii au msimamizi
66. Kiapo
67. Udhamini wa usimamizi
68. Utoaji wa masharti/hati ya usimamizi wa mirathi
69. Kutunzwa kwa wasii halisi
70. Uhalali wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi
71. Mpewaji pekee kuwa mwakilishi
72. Rufaa na mapitio

SEHEMU YA VIII
A. MAZOEA NA MAELEKEZO YA UCHAGUZI, NA UBATILISHAJI WA UCHAGUZI WA, WASIMAMIZI WA MALI CHACHE

73. Kutumika kwa Sehemu ya VIII
74. Uchaguzi wa wasimamizi
75. Usimamizi wa Kabidhi-Wasii na uchaguzi wa afisa wa mahakama au mtu muadilifu
76. Uchaguzi uthibitishwe muhuri wa moto
77. Dhamana ya usimamizi
78. Wosia
79. Uchaguzi unaweza kuwa kwa mali yote au baadhi ya mali
80. Athari za kuchaguliwa
81. Mali ambazo hazijadaiwa
82. Kupingwa kwa uchaguzi
83. Rufaa katika Mahakama Kuu
84. Mahakama za wilaya kupeleka taarifa Mahakama Kuu
85. Vizuizi katika utoaji wa uthibisho wa mirathi na hati za usimamizi wa mali chache.
86. Uhalali wa uchaguzi kuhusiana na mali inayozidi shilingi elfu kumi.
87. Usimamizi wa mirathi iliyo chini ya shilingi elfu moja

B. USIMAMIZI WA MALI CHACHE

88. Sheria inayotumika kwa mtu wa kabila fulani
89. Wosia wa mtu wa kabila fulani
90.-91. (Imefutwa)

SEHEMU YA IX

MALI ZINAZOSIMAMIWA KUTOKANA NA SHERIA ZA KIJADI, MILA NA SHERIA ZA KIISLAM.

92. Vipengele ambapo Sheria hii itatumika katika mali inayosimamiwa kwa kutumia sheria za kijadi pamoja na mila.
93. Athari za maelekezo ya Mahakama Kuu katika amri zilizowekwa na Mahakama ya Mwanzo.

SEHEMU YA X
USAJILI WA UTHIBITISHO WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI

94. Tafsiri
95. Usajili wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi iliyotolewa nje ya Tanzania
96. Vigezo vinavyotakiwa kabla ya kusajili mirathi
97. Dhamana
98. Madurufu na nakala

SEHEMU YA XI
MAMLAKA NA MAJUKUMU YA WASII NA WASIMAMIZI

99. Asili na mali ya wasii au msimamizi
100. Mamlaka kuhusiana na mshitaka na madeni
101. Mamlaka ya kuuza vitu
102. Matumizi kwa ajili ya uangalizi na usimamizi
103. Wasii au wasimamizi kutochukua faida yoyote kutoka kwenye mali
104. Mamlaka ya wasii au wasimamizi yanawezwa kufanywa na mmoja wao.
105. Mamlaka ya wawakilishi mahususi
106. Malipo ya gharama za msiba.
107. Orodha na mahesabu
108. Kazi za ujumla za usimamizi
109. Namna ya kulipa madeni
110. Madeni yalipwe kabla ya wausiwa
111. Kupungua kwa hiba ya wazi na usawa wa wausiwa
112. Kupungua kwa hiba mahsusi
113. Haki ya hiba maalum

SEHEMU YA XII
HIBA NA MALIPO YA MWAKA

114. Ridhaa inahitajika kwa muusiwa kupata mali yake
115. Ridhaa kwa hiba mahususi
116. Ridhaa ya wasii katika mali yake mwenyewe
117. Madhara ya ridhaa ya wasii
118. Kuanza kwa malipo ya mwaka kama muda haujawekwa katika wosia

119. Malipo ya malipo ya mwaka kama muda umewekwa
120. Vifungu vya ujumla kuhusiana na malipo ya mwaka
121. Uwekezaji katika amana inayoruhusiwa na Kanuni za Uthibitisho wa Wosia
122. Urithi unaotegemea jambo fulani
123. Maelekezo ya mtoa wosia katika uwekezaji
124. Watoto wanatakiwa wapate malipo au umiliki mara moja
125. Utolewaji wa hiba
126. Riba katika hiba ya wazi
127. Riba katika malipo ya mwaka
128. Baki ilipwe kwa muusiwa wa mali itakayobaki
129. Kuhamisha kwa mali kutoka Tanzania kwa wasii au msimamizi aliyepo katika nchi aliyokuwa akiishi marehemu

SEHEMU YA XIII
URUDISHAJI WA MALI KWA WAUSIWA

130. Urudishaji kama hiba imelipwa chini ya agizo la Mahakama
131. Hakuna urudishaji kama malipo yamefanywa kwa hiari
132. Urudishaji wa mali kama hiba imefikia muda wake baada ya sharti kutimizwa na muda kuongezwa
133. Pale wausiwa watakapotakiwa warudishe kwa usawa
134. Ugawaji wa mali
135. Pale mdai atakapomtaka wasii arudishe mali
136. Haki ya muusiwa kuwataka wausiwa wengine warudishe mali
137. Urudishwaji hautakuwa na riba

SEHEMU YA XIV
UFUJAJI WA MALI

138. Hatia itokanayo na ufujaji
139. Hatia ya kutojali

SEHEMU YA XV
USIMAMIZI WA MALI YA WAKFU

140. Tafsiri
141. Wakfu utakuwa wa halali
142. Uanzishwaji wa Tume ya Wakfu
143. Tume ya Wakfu kuwa mamlaka inayojitegemea na itakuwa na muhuri wa moto
144. Mikutano na kiwango/koramu
145. Usajili wa mali ya wakfu na amana
146. Tume ya Wakfu itafanya uchunguzi kuchukua usimamizi wa wakfu
147. Wadhamini wa wakfu wanaweza kuitwa kuleta uthibitisho wa usimamizi mzuri wa amana zao
148. Mikataba na makubaliano fulani yanayohusiana na mali ya wakfu ni lazima yathibitishwa na Tume ya Wakfu

149. Mali za wakfu hazitamilikiwa kwa maagizo au kwa kabidhi pingamizi baada ya kuanzishwa kwa sehemu hili
150. Jinsi ya kusimamia mali ya wakfu
151. Tume ya Wakfu inaweza ikauza mali ya wakfu katika mazingira fulani
152. Ruhusa inahitajika kujenga msikiti au kuanzisha makaburi
153. Ada
154. Ukaguzi wa mahesabu
155. Akaunti za benki
156. Sheria ya Usimamiaji wa Kodi haitatumika katika mali za wakfu
157. Adhabu
158. Kanuni

SEHEMU YA XVI
MALIPO YA KIISLAM (TUNU AU SADAKA)

159. Upendeleo wa afisa wa wilaya kufanya malipo

SEHEMU YA XVII
MENGINEYO

160. Vifungu vinavyomuhusu msimamizi aliyeambatanishiwa wosia
161. Uhifadhi wa wosia wa watu walio hai
162. Hati ya kiapo kama ni shirika la amana
163. Uhalali wa ugawaji wa mali kama haki ya matunzo imewekwa
164. Madadiliko ya sheria kadhaa
165. Sheria fulani kutotumika
166. Bakizo
167. Vifungu vya mpito
168. Bakizo la mamlaka ya Kabidhi- Wasii na muamana wa serikali

_____

MAJEDWALI

SURA YA 352

SHERIA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI

**Sheria inayoelezea utolewaji wa uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi, inaweka vifungu kuhusiana na mamlaka na kazi za wasii au wasimamizi wa mirathi; usimamizi wa mali iliyowekwa wakfu; malipo kwa ajili ya kukirimu au sadaka kwa mali za kiislamu, na masuala yanayohusiana na hayo.**

[1, Machi, 1963]

(Sura ya 445)
(Sura ya 29)
(Sura ya 30)
(Sura ya 326)

Sheria Namba
9 ya1963
55 ya 1963
33 ya 1964
9 ya 1965
41 ya 1966
18 ya 1970
23 ya1971
3 ya1979
12 ya 1979
10 ya1987

SEHEMU YA I

MASHARTI YA MWANZO

Jina la Sheria na atumizi

**1**.-(1) Sheria hii itaitwa Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi.

(2) Sambamba na kifungu cha 87 na Sehemu ya IX, Sheria hii itatumika katika usimamizi wa mirathi wa watu wote waliokufa huku wakiwa wakazi, au wameacha vitu, ndani ya Tanzania iwe kabla au baada ya tarehe ambayo Sheria hii itanza kutumika

Tafsiri

**2**.-(1) Katika Sehemu hi i, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"msimamizi" maana yake ni mtu ambaye amechaguliwa na

mahakama kusimamia mali ya marehemu ambapo hakukuwa na wasii, au hakuna wasii aliye tayari kufanya jukumu hilo, itajumuisha, pale Sehemu ya VIII itakapohusika na itategemeana na vifungu hivyo, mtu anayechaguliwa kuwa msimamizi katika Sehemu hiyo ;

"kibadilisho cha Wosia" maana yake ni hati inayohusiana na Wosia, na inaelezea, badilisha au inaongeza kitu katika ugawaji wa mali;

"shauri mbishano" inapohusishwa na utoaji wa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi maana yake ni kujitokeza kwa mtu kupinga muombaji asipewe usimamizi wa mirathi;

"mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu, na katika hali ambayo mteule wa wilaya ana mamlaka, mteule wa wilaya, lakini haihusishi mahakama ya wilaya;

"hiba maalumu" maana yake ni hiba iliyoelekezwa kulipwa katika mali mahususi;

Sura ya 11 "mahakama ya wilaya" maana yake ni mahakama chini ya Sheria ya Mahakama ya Mahakimu ;

"hakimu mteuliwa" maana yake ni hakimu mkazi aliyechagulia kukaimu wilaya katika kifungu cha 5;

"Wasii" ni mtu aliyechagualia na mtoa wosia asimamie mali zake atakapokua amefariki;

"hiba ya jumla" maana yake ni hiba yoyote isiyo hiba mahususi au maalumu;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya kisheria;

"uthibitisho wa Wosia" maana yake ni nakala ya wosia, au katika wosia wa mdomo, maelezo ya mdomo ya wosia huo, yaliyothibitishwa ma muhuri wa mahakama, inayotoa usimamizi wa mali za mtoa wosia;

"kanuni za uthibitisho wa Wosia" maana yake ni kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu cha 9;

"kanuni za mahakama" zinajumuisha kanuni zilizotengenezwa na Mahakama Kuu katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Usimamizi wa Haki na Matumizi ya Sheria na kanuni zilizomo au zilizotengenezwa na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai;

Sura ya 358

Sura ya 33

"mali chache" ni mali ambayo mahakama, mahakama ya wilaya iliyo na mamlaka katika uthibitisho wa wosia au usimamizi, imejirizisha kuwa haizidi shilingi elfu kumi ;
"hiba mahususi" maana yake ni hiba ya kitu kilichotajwa ;

"shirika la amana" maana yake ni-

(d) Muamana wa Serikali; au
(e) Kabidhi Wasii; au

benki yoyote au bima au mdhamini au kampuni ya amana ambayo in mtaji ( katika mali na hisa) isiyopungua paundi laki mbili na nusu wakati inatolewa, ambapo si chini ya paundi laki moja zimelipwa kwa pesa taslimu; au

(f) shirika lolote ambalo lina mtaji (katika mali na hisa) isiyopungua paundi laki mbili na elfu hamsini wakati wa kutolewa, ambapo si chini ya paundi laki moja zimelipwa kwa pesa taslimu, na kwa muda huo zimewezeshwa ( na sheria ya Bunge ya jamuhuri ya muungano, katiba ya kampuni, hati ya makubaliano au kitu kingine kinachohusiana na hiyo au kinachotoa mamlaka) ya kuchukua amana, lakini kwa muda mrefu kampuni hiyo haita, kwa mwaliko wa kampuni, mwongozo, tangazo au kwa nyaraka iliyotolewa na au kwa niaba ya, inasema au kutaja kuwa tuhuma zozote zinazoihusisha muamana wa serikali au mapato ya jumla ya jamuhuri wa muungano kuhusiana na kitendo au kutotendeka kwa jambo fulani katika kampuni hiyo wakati inatumikia kama wasii au msimamizi; na

"Wosia" maana yake ni tamko la kisheria la nia ya mtoa wosia kulingana na mali zake, na jinsi anavyotaka zitumike baada ya kifo chake;

(2) Bila kujali kitu chochote katika maana ya "shirika la amana" katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kampuni ambayo inaweza kuwa ni shirika la amana lakini kwa maana kuwa haijakidhi mahitaji yanayohusiana na mtaji katika aya ya (c) na (d) ya kifungu hicho linaweza likawa wasii au msimamizi katika hali yoyote kama Mahakama Kuu itakavyoamua, na hivyo kwa dhumuni la kuwa wasii au msimamizi litasemekana kuwa na mamlaka, haki na majukumu ya shirika la amana katika Sheria hii

## SEHEMU YA II

## MAMLAKA YA UTHIBITISHO WA WOSIA NA USIMAMIZI WA MALI

Mamlaka ya Mahakama Kuu katika uthibitisho wa wosia na usimamizi

**5.** Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka katika masuala yopte yanayohusu usimamizi wa mirathi,ambapo itakuwa na mamlaka ya kugawa mirathi inayotokana na wosia,na ile ya

hati za usimamizi wa mirathi ya marehemu,na pia kurekebisha au kutengua mirathi hiyo.

Mamlaka ya Mahakama Kuu kusajili mirathi fulani

**6.** Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusajili mirathi na hati za usimamizi wa mirathi uliofanywa na Mahakama zenye uwezo wa kusimamia mambo ya mirathi zilizopo katika nchi zilizokuwa koloni la Uingereza kwa mujibu wa Sehemu ya Kumi ya Sheria hii.

Mamlaka ya mteule wa wilaya

**5**.-(1) Katika nyakati tofauti tofauti Jaji Mkuu anaweza kuchagua mahakimu wa Mahakama za Wilaya kusilikiza mashauri ya mirathi kama mahakimu wateule

(2) Mahakimu wateule watakuwa na mamlaka katika mashauri yote yahusuyo mirathi na usimamizi wa mirathi huku wakiwa na malaka ya kuteua msimamizi wa mirathi na kutoa hati za usimamizi wa mirathi ikiwa kama marehemu, katika kipindi cha kifo chake alikuwa akiishi katika eneo ambalo hakimu huyo alichaguliwa-

(a)katika mirathi isiyo bishaniwa;

(b)atika mirathi inayobishaniwa,ila tu kama hakimu atajiridhisha kwamba thamani ya mirathi hiyo haizidi shilingi elfu kumi na tano, au iwapo Mahakama Kuu ikiamuru Hakimu kutekeleza mamlaka yake katika mazingira yanayoonyeshwa katika kifungu kidogocha(3)

(3) Hakuna kitendo cha mteule wa wilaya katika ufanyaji wa majukumu yake katika uthibitisho wa wosia na usimamizi wa mali kitakuwa batili kwa sababu ya kwamba imegundulika kuwa mali inazidi shilingi elfu kumi na tano, lakini hakimu huyo akilijua hilo katika mirathi inayobishaniwa, atatoa ripoti ya suala hilo katika Mahakama Kuu ambayo aidha itaagiza mwenendo wa shitaka uamishiwe kwake au itamruhusu mteule kuwa na mamlaka na suala hilo

(4) Hakimu mteuliwa hatokuwa na uwezo wa kushughulika na mamlaka ambayo bayana yamekewa kwa Mahakama Kuu

Mamlaka ya Mahakama za wilaya

**6**.- Mahakama ya Wilaya inayoongozwa na Hakimu wa Wilaya itakuwa na mamlaka katika usimamizi wa mirathi midogo, wakiwa na nguvu ya kuchagua msimamizi wa mirathi hizo ndogo, pale ambapo marehemu amefia katika sehemu ambayo Mahakama ina mamlaka kwa kutumia mfumo unaoonyeshwa katika jedwali la nne katika Sheria hii.

Afisa wa ubalozi

**7**.-(1) Ikiwa mtu ambaye ni raia wa nchi ambayo kifungu hiki kinatumika amechaguliwa kuwa wasii katika wosia wa marehemu aliyegawa mali zake Tanzania, au ni mtu ambaye anaweza akapewa usimamizi wa mali ndani ya Tanzania, mahakama kama itajiridhisha,

kufuatana na maombi ya afisa wa ubalozi wa nchi hiyo, ya kuwa mtu huyo sio mkazi wa Tanzania, na kama hakuna maombi ya usimamizi yaliyofanywa na wakala aliyeruhusiwa na hati haki ya uwakala kwa niaba yake, mahakama itampa afisa huyo usimamizi wa mali za marehemu kama ambavyo angepewa kama angekuwa amechaguliwa kama ilivyosemwa

(2) Hati inayotolewa kwa afisa wa ubalozi itapewa kwake kwa jina la ofisi na sio yeye binafsi, lakini mtu aliyepo katika ofisi hiyo atakula kiapo yeye mwenyewe binafsi. Hati hizo za usimamizi wa mali zitawekwa kutoka kwa afisa wa ubalozi kwa afisa mwingine atakaemrithi, na zitakuwa katika afisa huyo wa ubalozi kwa muda wote atakapokuwa ofisini pasipo kuwa na agizo la mahakama, au uhamishaji, au ugawaji au hati nyingine yoyote.

(3) Wadhamini hawatahitajika ikiwa kama usimamizi umepewa kwa afisa wa ubalozi katika kifungu hiki.

(4) Mtu yeyote ambaye ni raia wa nchi ambayo kifungu huki kinatumika-

(c) anastahili kupata pesa yoyote au kitu kingine Tanzania, ambacho ni moja kati ya mali za marehemu, au kupokea malipo Tanzania, ya pesa yoyote yaliyotimia kulipwa wakati wa kifo cha marehemu; au
(d) ni mmoja wa watu ambao pesa au kitu chochote cha marehemu, chini ya Sheria hii, kinaweza kulipwa bila ya hati ya uthibitisho wa wosia au uthibitisho wowote, kama ikiwa mtu huyo; sio raia wa Tanzania , afisa ubalozi wa nchi hiyo atakuwa na mamlaka ya kupokea au kutoa malipo halali ya pesa yoyote au mali yoyote kana kwamba ameruhusiwa na wakala aliyethibitishwa na hati ya uwakala afanye kwa niaba yake:

Isipokuwa kwamba hakuna mtu atakayeruhusiwa au kutakiwa na kifungu hiki kidogo kulipa au kupeleka pesa au mali kwa afisa ubalozi kama anajua kuwa kuna mtu alimeruhusiwa kupokea pesa au mali hiyo kwa niaba ya raia huyo

(5) Bila kuzingatia kifungu chochote kinachotoa ulinzi au upendeleo kuhusiana na vitendo vya kiofisi na nyaraka za afisa ubalozi, afisa ubalozi hatakuwa na ulinzi au upendeleo kuhusiana na kitendo alichofanya chini ya mamlaka yaliyowekwa kwake na kifungu hiki, au kuhusiana na nyaraka zozote zilizopo chini yake kwa muda huo.

(6) Kifungu hiki kinatumika kwa nchi zinazoonyeshwa katika Jedwali la kwanza,kupitia gazeti la serikali Waziri anaweza kuongeza au kupunguza nchi nyingine yeyote ya kigeni kutoka katika Jedwali la kwanza

Mamlaka katika Sheria hii yanaweza kufanywa sirini

8.Sambamba na kanuni zozote za uthibitisho wa mirathi, mamlaka ya mahakama au mahakama ya wilaya yanawezwa yakafanywa faraghani-

(a) katika shtaka linalobishaniwa; na

Sura ya 33

(b) katika shtaka lisilobishaniwa kwa kipomo kile kile kama vile mamlaka yakiwa yanafanywa faraghani katika dai linalofanywa kwa kulingana na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai au sheria yoyote itakayowekwa baada ya hiyo au kanuni zozote za mahakama.

Kanuni za uthibitisho wa wosia

**9**. Jaji Mkuu anaweza akaweka kanuni za uthibitisho wa mirathi kwa ajili ya kusimamia mienendo ya utolewaji wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi wa mirathi au uchaguliwaji wa msimamizi, kwa dhumuni hilo, katika Sheria hii imetolewa kuwa kanuni za uthibitishaji wa mirathi zinaweza zikatengenezwa, kwa ajili ya utunzwaji, na unakilishaji na ukaguzi wa wosia, matolea ya uthibitisho wa mirathi na usimamizi wa mali na uchaguzi wa wasimamizi, kwa ada inayojumiusha ada inayotolewa kwa wasimamizi katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 75 na fomu zake, na kwa ujumla kwa ajili ya utumiaji mzuri wa Sheria hii.

## SEHEMU YA III
## UTUNZAJI WA MALI WAKATI USIMAMIZI HAUJATOLEWA NA WASII WALIOJITIA

Mpokeaji wakati usimamizi haujatolewa

**10**. Ikiwa mtu amekufa na kuacha mali Tanzania, Mahakama inaweza, kama itaonekana kutokana na maombi ya Kabidhi Wasii au mtu yeyote mwenye masilahi na mali hiyo, au anayetunza au mwenye nguvu na mali hiyo wakati wa kifo cha marehemu, au kwa muda huyo ni wakili wa marehemu, kwamba kuna hatari kuwa mali hiyo inaweza ikapotezwa, itamchagua Kabidhi Wasii au mtu mwingine yeyote kama mahakama itakavyoona yafaa, kuwa mpokeaji wa mali hiyo huku toleo la uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi ikingojwa.

Mauzo kwa agizo la mahakama

**11**. Mahakama inaweza, kutokana na ombi litakaloombwa na mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10, au mtu yeyote mwenye maslahi na mali, kutoa amri ya kuuzwa kwa mali yote au sehemu ya mali hiyo, kama ikionekana kuwa kuuzwa kwa mali hiyo kutaifaidisha mali yote kwa ujumla.

Matumizi ya kanuni zinazohusu wapokeaji

**12**. Mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10 atatakiwa afuate miongozo yote ya mahakama inayowahusu wapokeaji kwa ujumla:

Ili mradi kwamba siyo Kabidhi Wasii wala Muamana wa Serikali atatakiwa kuweka dhamana ili kusimamia mirathi.

Adhabu kwa kidhihaki mahakama

**13**. Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka yototе, atatoa or atajaribu kutoa kutoka Tanzania sehemu yoyote ya mali ambayo

mpokeaji amechaguliwa katika kifungu cha 10, au ataharibu, au kuficha, or atakataa kutoa mali hiyo kwa mpokeaji, atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalipa fidia isiyopungua shilingi elfu tano au kwenda jela kwa muda usiopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.

Hakuna shtaka dhidi ya mpokeaji

**14.** Hakuna shtaka litaloletwa dhidi ya mpokeaji alichaguliwa katika kifungu cha 10 kutokana na suala lolote alilofanya au analotarajia kufanya linalohusu mali ya marehemu katika utekelezaji wa mamlaka aliyopewa; lakini mtu yeyote aliyeonewa na kitu chochote kilichofanywa, au kinachotarajiwa kufanywa, anaweza akaiomba mahakama muongozo kuhusu suala hilo, na mahakama itatoa amri kama inavyoona yafaa.

Haki tangulifu

**15**. Mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10 atakuwa na na haki tangulifu kwenye mali zilizokabidhiwa kwake kwa gharama na matumizi yote aliyoyafanya sawasawa katika kutimiza majukumu yake.

Wasii wa kujitia

**16**. Mtu yeyote ambaye ataingilia mali za marehemu au akafanya kitu chochote ambacho kingefanywa na ofisi wa msimamizi wa mirathi, kwa kipindi ambacho msimamizi wa mirathi hajachaguliwa, atakuwa amejiweka mwenyewe kuwa wasii aliyejitia.

Ili mradi kwamba-

(e) kuingilia vitu vya marehemu kwa lengo la kuvitunza au kugharamia gharama za mazishi au au kwa hitaji la haraka la familia au kitu; au

(f) kushughulika kwa hali ya kawaida na bidhaa za biashara za marehemu zilizopokelewa kutoka kwa mtu mwingine; au

(g) kitendo cha afisa wa utawala katika kifungu cha 14 cha Sheria ya Kabidhi-Wasii ( Majukumu na Shughuli);

Sura ya 27

(h) kitendo cha mpokeaji aliyechaguliwa katika kifungu cha 10, havipelekei mtu kuwa wasii aliyejiamulia

Hatia ya wasii aliyejiteua

**17**. Ikiwa mtu amekuwa wasii aliyejiteua mwenyewe, atatakiwa kujieleza kwa wasii atakae chaguliwa kihalali, au kwa mrithi au mdai wa marehemu, kulingana na mali ambazo zimepita mikononi mwake, baada ya kupunguza malipo apewayo wasii wa halali, na malipo yoyote yaliyofanya katika shughuli nzima ya usimamizi.

## SEHEMU YA IV
## KUJITOA KWA WASII

Ujitoaji dhahiri wa kuchukua usimamizi

**18.** Mtu anaetakiwa kupewa uthibitisho wa usimamizi wa Wosia anaweza kujitoa au kukataa kusimamia mirathi hiyo kwa mdomo siku ya kusikiliza kwa ombi lolote au kwa maandishi yaliyosainiwa na mtu anayejitoa yaliyoshuhudiwa mbele ya mtu ambaye kiapo kinaweza kutolewa mbele yake.

Wito na ujitoaji unaobuniwa

**19**.-(1) Mtu yeyote mwenye au anayedai kuwa na maslahi na mali ya marehemu au mdai wa marehemu anaweza kuomba wito

kwenda kwa msimamizi au wasimamizi wa mirathi waliochagulia na marehemu katika wosia wake, ili waje wakubali usimamizi huo au wajitoe katika usimamizi wa mirathi husika.

(2) Mtu yeyote aliye pokea wito huo anaweza kuhudhuria, lakini kama asipohudhuria, atachukuliwa kuwa amejitoa katika usimamaizi wa mirathi; na kama, alijitokeza, na hajaendelea kuomba uthibitisho wa usimamizi wa mirathi, mtu aliyeomba aitwe anaweza akaomba amri ya kwamba mtu aliyeitwa, isipokuwa kama ataomba na kupata uthibitisho wa usimamizi wa mirathi kwa muda utakaoamriwa, achukuliwe kuwa amejitoa katika usimamizi wa mirathi, na amri inaweza ikatolewa kama inavyopaswa.

Madhara ya kujitoa

**20.** Kujitoa katika usimamizi wa mirathi kuwe kwa maneno au kwa vitendo vinavoashiria kujitoa, hakutamruhusu mtu huyo aliyejitoa kuomba tena usimamizi wa mirathi:
Ili mradi kwamba mahakama kwa muda wowote inaweza ikamruhusu mtu aliyejitoa kufuta kujitoa kwake kwa dhumuni la kuchukua usimamizi wa mirathi, kama itaonekana kuwa ufutaji huo ni kwa faida ya mali au watu wenye masilahi na mali hiyo.

## SEHEMU YA V

## UTOAJI WA UTHIBITISHO WA WOSIA NA HATI ZA USIMAMIZI NA MAHAKAMA

*A. Vifungu vya Jumla*

Kampuni ya amana

**21**.-(1) Kampuni yenye dhamana/ kampuni ya muamana

(c) inaweza kuthibitishwa usimamizi wa mirathi inayotokana na wosia wa mtu yeyote,iwapo imetajwa kama msimamizi katika wosia huo;

(d) inaweza kupewa barua ya usimamizi wa mirathi

(2) Kampuni iliyo na dhamana inaweza kuthibitishwa kama msimamizi wa mirathi au kupatiwa barua ya usimamizi wa mirathi pekee yake au pamoja na watu wengine.

(3) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi haitatolewa kwa kundi la watu au mashirika au kwa mtu aliyeteuliwa na kampuni kufanya hivyo kwa niaba yake

Idadi ya wasii na wasimamizi

**22**.-(1) Uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi haitatolewa kwa watu zaidi ya wanne kuhusiana na mali moja, na hati za usimamizi wa mirathi, kama kuna utoto, au maslahi ya maisha yanaibuka katika wosia au katika mtu kifo bila wosia, utapewa ama kwa kampuni ya muamana pekee au pamoja na mtu au si zaidi ya watu wawili:
Ili mradi kwamba katika utoaji wa hati za usimamizi wa mirathi mahakama inaweza ikajikita katika ushahidi unaoonekana, ulioletwa na muombaji au na mtu yeyote, ya kuwa kuna au hakuna utoto au maslahi ya maisha, kama itakavyoelezwa na kanuni za uthibitishaji wa

mirathi.

(2) Kama kuna mwakilishi mmoja tu (na siyo kampuni ya muamana) katika utoto wa mnufaishwaji au uwepo wa masilahi ya maisha na mpaka mali zote zimemamilizwa kusimamiwa, mahakama inaweza, kwa ombi la mtu yeyote mwenye maslahi, au mlezi, kamati au mpokeaji wa mtu yeyote kuchagua mwakilishi au wawakilishi kwa kuongezea wasimamizi waliopo, kulingana na kanuni za uthibitisho wa mirathi.

Watoto na watu wenye matatizo ya akili

**23**. Usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi hauwezi kutolewa kwa mtoto chini ya miaka kumi na nane au mtu aliye na matatizo ya akili

*B- Uthibitisho wa Wosia*

Utoaji wa uthibitisho wa wosia

**24**.-(1)Usimamizi wa mirathi unaweza kutolewa kwa msimamizi aliyetajwa katika wosia

(2)Uchaguzi unaweza ukawa wa wazi au maana inayoashiria usimamizia

(3) Pale inapotokea wamechaguliwa executors tofauti, mirathi inaweza kutolewa kwao kwa pamoja na katika wakati tofauti

(4) Ikiwa msimamizi wa mirathi akichaguliwa kwa kwa ajili ya utekelezaji wa malengo fulani, basi uteuzi huo utahusisha yale mambo yaliyokusudiwa tu.

Uthibitisho wa wosia kwa kutumia nakala, hawala au maneno ya wosia wa mdomo

**25.**-(1)Pale inapotokea wosia umepotea au hauwezi kupatikana baada ya kufa kwa yule aliyeandika ,au umeharibika kimakosa,ajali na si kwa kitendo chochote cha mtoa wosia-

(c) ikiwa kama nakala ya wosia ilitunzwa, uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi unaweza kutolewa kwa kupitia nakala hiyo, mpaka pale wosia halisi au nakala ya wosia uliothibitishwa umepokelewa katika mirathi.

(d) ikiwa hakuna nakala au hawala ya wosia uliotunzwa, uthibitishwaji wa mirathi unaweza kutolewa iwapo tu kutakuwa na ushahidi wa kuthibitisha yaliyomo katika wosia, yenye ukomo katika hilo

(2) Pale ambapo wosia ulioandikwa unashikiliwa na mtu aliye nje ya nchi, na amekata au kupuuza kuwasilisha, lakini nakala yake inapatikana kwa msimamizi wa mirathi, mirathi hiyo inaweza kutolewa kwa kutumia nakala ya wosia huo kwa manufaa ya mali hiyo ya marehemu pasipo kusubiri nakala halisi.

(3) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi kuhusu wosia uliotolewa kwa mdomo utatolewa iwapo tu kutakuwa na ushahidi wa kuthibitisha yaliyopoa katika wosia

Kibadilisho cha wosia kinachopatikana baada ya uthibitisho wa wosia kutolewa

**26** .Ikiwa uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi umekwishatolewa, na kibadilisho cha wosia kikapatikana, uthibitishwaji mwingine wa usimamizi wa mirathi unaweza ukatolewa kulingana na badiliko hilo.

Ila ikiwa badiliko hilo la wosia kwa uwazi au kwa ufahamuzi linakataa uchaguzi wa msaimamizi wa mirathi ambaye amekwisha pewa mamlaka ya kusimamia mirathi, uthibithishwaji wa mirathi uliofanywa utabatilishwa na uthibishwaji wa mirathi utafanywa upya kwa wosia wa zamani na badiliko lake kwa pamoja

Nakala ya wosia iliyothibitishwa nje ya nchi

**27**. Ikiwa wosia umethibitishwa na kuhifadhiwa katika mahakama yenye mamlaka iliyoko nje ya Tanzania, lakini nakala sahihi na iliyothibitishwa ikaletwa, uthibitishwaji wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na nakala hiyo inaweza kutolewa.

Madhara ya uthibitisho wa wosia

**28.** Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi ukishatolewa huupa wosia nguvu na hushuhudia cheo cha msimamizi wa mirathi baada ya kifo cha mtoa wosia.

Kushindwa kwa wosia

**29**. Ikiwa

(g) hakuna msimamizi wa mirathi aliyechaguliwa; au

(h) msimamizi au wasimmizi wa mirathi waliochaguliwa kwenye wosia wamejitoa, au ni watu ambao hawawezi wakapewa uthibitisho wa usimamiaji wa mirathi; au

(i) wasimamizi wa mirathi waliochagulia wamefariki kabla ya mtoa wosia kufariki; au

(j) wasimamizi wa mirathi waliochagulia wamefariki kabla ya kupata uthibitisho wa usimamizi wa mirathi au kabla hawajamaliza kusimamia mirathi yote ya marehemu; au

(k) wasimamizi wa mirathi waliochaguliwa hawajajitokeza kuchukua uthibitisho wa usimamizi wa mirathi;

(l) barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia inaweza ikatolewa kwa mirathi yote ambayo haijaamriwa au sehemu ya mirathi hiyo ambayo haijaamriwa kwa mtu au watu ambao mahakama itaona yafaa wao waamru mirathi hiyo.

Ila kipaumbele kitapewa kwa makundi yafuatayo na kwa muongozo huu-

(i) muusiwa wa kwanza au wa mali itakayobaki ;

(ii) mwakilishi wa marehemu au muusiwa wa kwanza au wa mali itakayobaki ;

(iii) mtu au watu, ambao wananufaika na wosia na ambao wangeweza kupewa barua ya usimamizi wa mirathi ikiwa marehemu angekufa bila kuacha wosia;

(iv) mrithi mwenye masilahi yenye faida;na

(v) mdai wa marahemu.

Ili mradi kwamba, mahakama haitatoa barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambataniswa na wosia ambao umemtaja msimamizi wa mirathi husika, na ikiwa msimamizi huyo-

(i) anaishi na mahali alipo panajulikana; na

(ii) ni mtu ambaye anaweza kupewa uthibitisho wa

usimamizi wa mirathi

(iii) hajajitoa katika ofisi ya usimamiaji mirathi:

Isipokuwa kwamba kama wito umetolewa na kumuita msimamizi wa mirathi kuja kutwaa au kujitoa kuwa msimaizi wa mirathi na msimamizi huyo amejitoa au amesajilikiwa kuwa amejitoa kama inavoonekana katika kifungu cha 18 na 19.

Wakala wa wasii asiyekuwepo

**30**. Ikiwa msimamizi wa mirathi hayupo Tanzania na hakuna mtu nadani ya nchi ambaye yupo tayari kuwa msimamizi wa mirathi, barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia itapewa kwa wakala wake aliyewekwa kisheria na anayeishi ndani ya Tanzania, kwa dhumuni lenye ukomo kwa muda ambao msimamizi huyo hayupo mpaka atakaporudi na kuchukua uthibitisho wa usimamizi wa mirathi yeye mwenyewe.

Wakala wa mtu anayestahili kupewa hati za usimamizi

**31**. Ikiwa mtu ambaye anaweza kupewa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi katika kifungu cha 29 hayupo ndani ya Tanzania, barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia itapewa kwa wakala wake aliyewekwa kisheria na anayeishi ndani ya Tanzania, kwa kwa dhumuni lenye ukomo kama inavyoelezewa katika kifungu cha 30.

Kibadilisha wosia kilicho patikana baada ya hati za usimamizi kutolewa

**32**. Kifungu cha 26 kitatumika sawa katika utolewaji wa barua ya usimamizi wa mirathi iliyoambatanishwa na wosia kama inavotumika katika utoaji wa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi

*D.- Hati za Usimamizi kwenye Kifo bila Wosia*

Hati za usimamizi kwa aliyefariki bila wosia

**33**.-(1) Pale marehemu anapofariki bila kuacha wosia, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikatolewa kwa mtu yeyote ambaye, kufuatana na utumikaji wa kanuni za ugawaji wa mali za mtu anapofariki bila wosia, mtu huyo atakuwa ana haki ya kupata mali yote au sehemu ya mali ya marehemu.

(2) Ikiwa mtu zaidi ya mmoja wameomba hati za usimamizi wa mirathi, itakuwa ni upendeleo wa mahakama kumpa mmoja wao au wengi wao, na katika upendeleo huo mahakama itachukulia maanani maslahi ya haraka ya mali ya marehemu kwa kuangalia mtu mwenye maslahi zaidi kuliko yule mwenye maslahi machache katika mali ya marehemu.

(3) Kama hakuna mtu aliyeomba, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikatolewa kwa mdai wa marehemu.

(4) Kama mahakama ikiona ni muhimu au inafaa kumpa mtu yeyote usimamizi wa mirathi au sehemu ya mirathi zaidi ya mtu yule ambaye kwa hali ya kawaida alitakiwa apewe usimamizi wa mirathi, mahakama kwa upendeleo wake, na kwa kutilia maanani ujamaa, masilahi, usalama wa mali na uwiano wa kuwa mali itasimamiwa vizuri, itamchagua mtu huyo kama inavyoona yafaa kuwa msimamizi; na katika kila hali hiyo hati za usimamizi inaweza ikawa yenye

kikomo au kama mahakama itakavyoona ni sawa.

Wakala wa mtu anayestahili usimamizi

**34**. Ikiwa mtu anayetakiwa achukue hati za usimamizi wa mirathi yuko nje ya Tanzania na hakuna mtu aliye tayari kubeba jukumu hilo, hati za usimamizi wa mirathi inaweza ikapewa kwa wakala aliewekwa kisheria, na anayeishi Tanzania, wa mtu huyo, yenye kikomo mpaka mtu huyo achukue hati za usimamizi mwenyewe na katika muda huyo kwa dhumuni lolote lenye kikomo kutokana na mamlaka aliyonayo wakala huyo.

*E.Hati za Usimamizi wa Mirathi kwa Dhumuni Maalumu.*

Mpaka wosia upatikane

**36.** Pale ambapo hakuna wosia wa marehemu,lakini kuna sababu za kuamini kwamba kuna wosia, hati za usimamizi wa mirathi inaweza kutolewa,mpaka pale wosia au nakala iliyothibitishwa itakapo tolewa.

Wakati wa utoto

**36**.-(1) Ikiwa mtoto alitakiwa, isipokuwa kwa utoto wake, kupewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi, hati ya usimamizi iliyo au isiyo ambatanishwa na wosia inaweza, sambamba na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 22, ikapewa kwa mlezi wa mtu huyo na mali ya mtoto, au kwa mtu yule kama mahakama itakavyoona yafaa, kwa ukomo mpaka mtoto atakapofikisha umri wa kuchukua usimamizi yeye mwenyewe.

(2) Ikiwa kuna wasii wawili au zaidi ambao ni watoto au watu wanaofaa kupewa usimamizi, usimamizi katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatolewa kwa ukomo mpaka mmoja au wengine kati yao watakapochukua jukumu la usimamizi.

Wakati mtu hana akili sawa

**37.** Ikiwa mtu kichaa alitakiwa, ila kwa ukichaa wake, kupewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi iliyo au isiyo ambatanishwa na wosia, inaweza ikapewa kwa mtu ambaye uangalifu wa mali zake umewekwa kwenye mamlaka yenye nguvu, au kwa mtu yule kama mahakama itakavyoona yafaa, kwa matumizi na kwa faida ya mtu kichaa, kwa ukomo mpaka mtu yule atakaporudi kwenye hali yake ya kawaida na kuchukua usimamizi mwenyewe.

*Kusubiriwa kwa utoaji*

**38**. Wakati uamuzi wa shauri lolote linahusu uhalali wa wosia wa marehemu unasuburiwa, au shauri la kuchukua, au kupinga utoaji wa uthibitisho wa wosia au utoaji wa hati za usimamizi, mahakama iinaweza ikamchagua msimamizi ma mali ya marehemu, ambaye atakuwa na haki na mamlaka ya msimamizi mkuu isipokuwa kugawa mali hizo, na kila msimamizi atakuwa chini ya usimamizi wa mahakama na atawajibika kutokana na maelekezo ya mahakama.

Ukusanyaji na utunzaji wa mali

**39**. Kama katika hali yoyote inaonekana ni muhimu kutunza mali ya marehemu, mahakama inaweza ikatoa, kwa mtu yeyote ambaye inaona anafaa, hati za usimamizi yenye ukomo wa kukusanya na kutunza mali ya marehemu, na kulipa madeni yote yaliyofikia muda wake na vitendo vyovyote (tofauti na ugawaji wa mali kama mahakama itakavyoona ni sawa) kulingana na maelekezo ya mahakama.

Mashtaka

**40**.-(1) Ikiwa ni muhimu kwa mwakilishi wa marehemu kuwa

mmoja wa upande wa shauri lililopo mahakamani, na wasii au mtu anayetakiwa kuchukua hati za usimamizi hayupo tayari kuchukua wajibu huo, hati za usimamizi inaweza kupewa kwa mchaguliwa wa upande wa mashtaka wa shauri hilo, lenye ukomo wa kumwakilisha marehemu katika shauri hilo, au au shauri lolote linaloweza kuanzishwa kwenye suala hilo au kwenye mahakama yoyote baina ya pande hizo, au pande zingine, inayogusa shauri hilo, na mpaka amri ya mahakama itoke na utekelezwaji wake ufanywe kabisa.

(2) Ikiwa, miezi kumi na miwili imepita toka uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi itoke, na wasii au msimamizi aliyepewa hayupo Tanzania, mahakama inaweza ikatoa kwa mtu yeyote kama inavyoona sawa hati za usimamizi yenye ukomo katika dhumuni la kuwa na kufanywa upande mmoja wa shauri litakaloletwa dhidi ya wasii au msimamizi, na kuchukua amri ya mahakama itakayotolewa juu ya shauri hilo.

Mali ya amana

**41**. Ikiwa mtu amekufa, na kuacha mali ambayo alikuwa ndio mnufaikaji wa mwisho, au hakuwa na masilahi yeyote yenye faida katika hilo, na hajaacha muwakilishi wa jumla, au mtu ambaye hawezi au hayuko tayari kuchukua jukumu hilo, hati ya wosia, yenye ukomo kwa mali hiyo, inaweza ikatolewa kwa mnufaikaji, au kwa mtu yeeyote kwa niaba yake.

*F. Utolewaji kwa Kiasi*

Utoaji kwa kiasi

**42**. Ikiwa hali ya shauri inahitaji kiasi cha mali kithibitishwe au kitolewe hati za usimamizi iliyo au isiyoambatana na wosia, utolewaji huo utafanywa kulingana na kiasi hicho.

Utolewa wa kiasi kilichobaki

**43**. Ikiwa toleo la uthibitisho wa wosia u hati ya usimamizi iliyo au isiyoambatanishwa na wosia imetolewa kwa kiasi cha mali, toleo lingine linaweza likafanyika katika kiasi cha mali kilichobaki.

*G.Madhara ya Utoaji wa Hati za Usimamizi*

Madhara ya utoaji wa hati za usimamizi

**44.** Sambamba na vizuizi vilivyomo, kama usimamizi umetolewa kwa ajili ya dhumuni maalumu, kwa dhumuni hilo tu, hati za usimamizi inamwezesha msimamizi awe na haki aliyokuwa nayo marehemu kana kwamba amepewa usimamizi wakati wa kifo cha marehemu:

Isipokuwa kwamba hati za usimamizi hakitahalalisha kitendo chochote ingilivu cha msimamizi kinacholenga kupunguza au kuharibu mali ya marehemu aliyefariki bila kuacha wosia

*H. Kifo cha Wasii au Wasimamizi na Kuisha kwa Muda wa Toleo lenye Ukomo*

Kifo cha mwakilishi au wawakilishi

**45**. Ikiwa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi imepewa kwa zaidi ya wasii au msimamizi mmoja na mmoja wao akafariki, usimamizi wa mali zilizobaki, kama hakuna muongozo katika wosia au uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, utabaki kwa wasii au msimamizi au wasimamizi waliobakia.

Kifo cha mwakilishi

**46.** Pale wasii mmoja au wasii aliyebaki na aliyethibitisha

au mwakilishi aliyebaki

wosia akafa, au msimamizi mmoja au msimamizi aliyebaki, hati za usimamizi wa mirathi itatolwa kuhusiana na mali ambazo hazijaamuliwa, na mahakama itatumia vifungu vilevile ilivyotumia mwanzo katika utoaji wa hati hiyo ya ya usimamizi wa mirathi.

Ikiwa wasii mmoja au zaidi wamethibitisha wosia au hati za usimamizi iliyoambatanishwa na wosia imetolewa, mahakama inaweza ikatoa hati za usimamizi wa wa mirathi katika kigungu hiki bila kumuita wasii ambaye hakuthibitisha wasii.

Kuisha kwa muda kwa toleo lenye ukomo

**47**. Ikiwa usimamizi wa mirathi wenye kikomo umekwisha kutokana na kuisha kwa muda uliopangwa, au kwa kutokea suala lenye ukomo, au suala ambalo halikutarajiwa na kuna baadhi ya mali hazijaamuliwa, hati za usimamizi wa mirathi itatolewa kwa watu wale ambao wangeweza kupewa usimamizi huo kwa mara ya kwanza.

## SEHEMU YA VI
## PINGAMIZI NA MABADILIKO YA TOLEO NA KUONDOLEWA KWA WASII AU MSIMAMIZI

Kubadilisha makosa

48. Makosa katika majina au maelezo, au muda na mahali ambapo marehemu alifariki, au dhumuni katika usimamizi wenye ukomo, vinaweza kurekebishwa na mahakama, na tolea la uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi unaweza ukabadilishwa au kurekebishwa kama itavyotakiwa.

Kupingwa wa toleo na uondolewaji wa wasii

**49**.-(1) Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au utolewaji wa barua ya mirathi unaweza kutenguliwa au kubatilishwa kwa sababu zifuatazo-

(f) ikiwa mwenendo mzima wa utolewaji ulikuwa na mapungufu;

(g) kwamba utolewaji wa usimamizi wa mirathi ulipatikana kwa udanganyifu kwa kutoa shauri la uongo, au kwa kufichajambo la maana katika shauri;

(h) kwamba utolewaji wa usimamizi wa mirathi ulipatikana kwa njia ya dai lisilo la ukweli katika jambo ambalo ni muhimu katika sheria kuthibitisha utolewaji wa usimamizi wa mirathi, hata kama dai hilo lilitolewa kwa kutojua au kupitiwa;

(i) kwamba uusimamizi wa mirathi hiyo umekuwa duni na haupo tena;

(j) kwamba mtu aliyepewa usimamizi wa mirathi kwa kukusudia na kwa kutokuwa na sababu yoyote hajapeleka orodha ya jinsi alivyosimamia mali za marehemu au mahesabu kama inavyotakiwa katika Sehemu ya XI au ameleta orodha au hesabu ambazo si za kweli katika

sehemu hiyo.

(2) Ikiwa ikathibitika kuwa usimamizi stahiki wa mali za marehemu na masilahi ya wanufaishwaji unahitajika, mahakama itamuondoa wasii au msimamizi (tofauti na kabidhi wasii au muamana wa serikali) na kumuweka mtu mwingine katika ofisi ya wasii au msimamizi ambaye anaachia ofisi na atamuachia kila kitu kinachohusiana na mali husika.

Malipo yaliyofanywa na wawakilishi ambao wameondolewa

**50.**-(1) Ikiwa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi umetenguliwa, malipo yote yaliyofanywa na wasii au msimamizi kwa kipindi alichokuwa akisimamia, yatakuwa ni halali kwa mtu aliyefanya malipo hayo, bila kujalisha utenguliwaji huo.

(2) Wasii au msimamizi aliyetenguliwa kusimamia mirathi anaweza akajilipa kutoka katika mali ya marehemu kuhusiana na malipo aliyoyafanya ambapo mtu ambaye atapewa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi angeyafanya kihalali.

Kurudisha toleo lililotenguliwa

**51**.-(1) Ikiwa uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi ikitenguliwa kwa mujibu wa Sheria hii, mtu huyo ambaye alithibitishwa atatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi katika mahakama iliyompatia usimamizi huo.

(2) Ikiwa mtu huyo kwa makusudi na bila sababu yoyote ya msingi akishindwa kuwasilisha uthibitisho wa wosia au barua hiyo atakuwa anafanya kosa lenye adhabu ya faini isiyozidi shilling elfu mbili au kifungo kisichozidi miezi mitatu,au vyote kwa maana ya faini na kifungo

## SEHEMU YA VII
## UTARATIBU WA KUTOA UTHIBITISHO WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI( HAIJUMUISHI MIRATHI YENYE MALI CHACHE)

Kanuni zitakazotumika mahakamani

**52**. Tofauti na itavyoelezwa hapa, na sambamba na kanuni za uthibitisho wa mirathi zilizotengenezwa kwa dhumuni hilo-

(c) kesi zozote za uthibitishwaji wa wosia na utoaji wa hati za usimamizi wa mirathi zitafuata Sheria ya Mashauri ya Madai au marekebisho yoyote yatakoiondoa Sheria ya Mashauri ya Madai; na

Sura ya 33

(d) katika hali ambayo kuna mabishano, mwenendo wa mashtaka utachukua sura hii, muombaji atakuwa mdaawa na mtu yeyote atakayejitokeza kupinga atakuwa mdaiwa

Maombi kwenda Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya

**53**.-(1) Maombi ya uthibitishwaji wa wosia yatafanywa Mahakama Kuu au kwa mteule wa wilaya aliyechagulia katika eneo ambalo marehemu alikuwa akiishi katika kipindi cha kifo chake

(2) Ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi kwa mteule wa wilaya, kama imefanywa na imethibitishwa kama inavyotakiwa hapa, itakuwa ushahidi dhumuni la kuthibitisha utoaji wa hati ya uthibitisho au hati za usimamizi, na hakuna toleo litakalo pingwa kwa sababu ya

kwamba marehemu hakuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambayo mteule wa wilaya amechaguliwa isipokuwa kwa mwenendo wa kubatilisha toleo kama lilipatitaka kwa udanganyifu mbele ya mahakama.

Mteule wa Wilaya kusimamisha mashitaka na kutuma ripoti Mahakama Kuu

**54**.-(1) Ikiwa ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi limefanyikwa kwa hatimu mteule au-

(c) ombi limefanyika kuhusu mali inayozidi kumi na tano elfu, na likapingwa; au

(d) kama mteule wa wilaya akiona kuwa uthibitisho wa wasii au hati za usimamizi wa wosia haitakiwi kutolewa naye,

mteule wa wilaya atasitisha mwenendo wa mshitaka na ataipa taarifa Mahakama Kuu.

(2) Baada ya kuupokea ripoti hiyo, Mahakama Kuu inaweza ikamruhusu mteule wa wilaya kuendelea na shauri kwa kuzingatia ushauri ambao mahakana kuu utaona sawa, au inaweza ikakataza mwendelezo wa shauri na mteule wa wilaya kuhusu suala la ombi hilo,na kuwaruhusu mwombaji hao wapeleke maombi yao Mahakama Kuu.

(3) Pale Mahakama Kuu itakapokataza mwendelezo wa shauri hilo na mteule wa wilaya, maombi, pamoja na nyaraka zote zilizoletwa mahakamani, zitarudishwa kwa mleta maombi, ili ziweze kuwasilishwa Mahakama Kuu, isipokuwa kama mteule wa wilaya ataona ni muhimu kwa ajili ya haki kutoruhusu nyaraka hizo zitoke, kwa kuwa anaruhusiwa kufanya hivyo; na katika suala hizo nyaraka hizo zitatumwa na yeye Mahakama Kuu.

Maombi ya uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi iliyoambatanishwa na wosia

**55.**-(1) Ombi la uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, yatafanywa kwa maombi pamoja na wosia, au, katika hali zilizotajwa katika kifungu cha 25, nakala au maelezo ya maneno yaliyosemwa ikiambatanishwa na wosia na mmaombi yataeleza-

(f) tarehe and mahali marehemu alipokufa;

(g) kwamba maandishi yaliambatanishwa ni wosia wake wa mwisho na ni agano lake, au kama itakavyokuwa;

(h) kiasi na aina ya mali ambayo itatakiwa isimamiwe na muombaji;

(i) majina na anuani, kama zinajulikana, za wasii waliotajwa kwenye wasii, na, pale maombi yatakapokuwa ni ya uthibitisho wa wosia, kwamba muombaji ni wasii alietajwa kwenye wosia; na

(j) kama mwenendo wowote wa utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, au vinginenevyo kwa usimamizi wa mali umefanyika kabla katika mahakama nyingine yenye mamlaka, ikiwa ni ndani au nje ya Tanzania.

(2) Tofauti na mahitaji hayo, maombi yataelezea, pale maombi yatakapo takiwa kupelekwa kwa hakimu mteuliwa, kwamba marehemu wakati wa kifo chake alikuwa na makazi ya kudumu katika eneo la mamlaka la hakimu huyo mteuliwa.

(3) Ikiwa wosia, nakala, hawala, au maelezo ya maneno yaliyosemwa, yameandikwa katika lugha ambayo si kingereza, tafsiri iliyofanywa na mtu ambaye ni bingwa katika tafsiri, na kuthibitishwa na mtu huyo itaambatanishwa kwenye maombi.

Maombi ya hati za usimamizi

**56**.-(1) Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kuombwa kwa maombi yatakayokuwa na-

(g) tarehe na mahali ambapo marehemu alifariki;
(h) familia au ndugu wa marehemu pamoja na maeneo waishio;
(i) haki ambayo muomba maombi anadai;
(j) kiwango na aina ya mali ambayo yanatakiwa kuwa mikononi mwa muomba maombi;
(k) utafutaji wa kina umefanyika na hakuna Wosia uliopatikana; na
(l) au kama kuna shauri lolote kuhusu maombi ya barua ya usimamizi au lolote lile kuhusu usimamizi, limeanza kushughulikiwa na mahakama yoyote au mamlaka, iwe nadani ya Tanzania au nje ya Tanzania

(2) Ikiwa shauri la maombi ya usimamizi wa mirathi yapo chini ya hakimu wa wilaya mteuliwa, maombi hayo yanapaswa pia kutaja kama ziada, kwamba katika kipindi cha kifo cha marehemu alikuwa akiishi katika eneo hilo la mteule wa wilaya

Uthibitisho wa maombi

**57.**-(1) Maombi ya uthibitishwaji wa usimizi wa mirathi au barua ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kusainiwa na muomba maombi na wakili wake kama yupo na yanatakiwa kuthibitishwa na muomba maombi

(2) Pale ambapo maombi yanahusu uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi, au ya barua ya usimamizi wa mirathi yaliyoambatanishwa na wosia, maombi hayo yatatakiwa kuthibitishwa na angalau mmoja wa mashahidi katika wosia:

Ilimradi mahakama inaweza isihitaji uthibitisho wa shahidi, kama ikiridhika kuwa uthibitisho hauwezi kupatikana au hauwezi kupatikana kwa muda unaotakiwa, au utahitaji gharama kubwa kupatikana.

(3) Kama maombi au tamko linahitaji kuthibitishwa, na likawa na kitu ambacho mtu anaethibitisha anajua au anaamini kuwa ni uongo au haamini kuwa ni cha kweli, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la jinai and kama akitiwa hatiani atatumikia kifungo cha muda usiozidi miaka saba

Zuio kupinga utoaji wa uthibitisho wa wosia au usimamizi

**58**.-(1) Mtu yeyote aliye na maslahi katika mirathi ya marehemu anaweza kuweka zuio katika utoaji wa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi

(2) Zuio linaweza kuwekwa katika Mahakama Kuu, au pale ambapo marehemu alikuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambapo mteule wa wilaya amechaguliwa au maombi ya uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi imetolewa na mteule wa wilaya, na mteule wa wilaya husika.

(3) Mara baada ya zuio hilo kuwekwa kwa mteule wa wilaya,

hakimu huyo atatuma nakala ya zuio katika Mahakama Kuu.

(4) Ikiwa zuio limepelekwa Mahakama Kuu na inaonyesha kuwa marehemu wakati wa kifo chake, alikuwa na makazi ya kudumu katika sehemu ambayo mteule wa wilaya amechaguliwa, msajili atatuma nakala kwa mteule wa wilaya.

(5) Zuio litakuwa na nguvu kwa muda wa miezi minne baada ya tarehe lilipowekwa (isipokuwa likiondolewa kabla ya muda huo) lakini, sambamba na kifungu cha 59, linaweza likarudishwa.

Mwendendo baada ya kuwekwa kwa zuio

**59**.-(1) Sambamba na kama inavyotolewa na kifungu hiki, hakuna mwenendo utakaofanyika katika uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, baada ya zuio kuwekwa katika mahakama ambapo maombi yamefanyika kwa muda wote ambao zuio litakuwa na nguvu.

(2) Ikiwa zuio limewekwa, mtu yeyote aliyeomba uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi ataomba wito utolewe kwenda kwa mpingaji ili kumuita aje aseme, katika muda utakao kuwa umewekwa, kama anaunga mkono utolewaji wa uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi, na kama haungi mkono, kumtaka ajitokeze mbele ya mahakama katika maombi hayo.

(3) Ikiwa mpingaji atajitokeza, mahakama itaendelea na maombi kama invoonyeshwa katika aya (b)ya kifungu cha 52.

(4)Ikiwa mpingaji akitoa notisi ya kuwa anaunga mkono maombi, au akishindwa kutoa notisi kwa jinsi hiyo na akashindwa kujitokeza mahakamani kwa ajili ya maombi yake, kwa muda uliopangwa, zuio litasemekana kuwa limeondolewa na hakuna zuio lingine litakalowekwa na mpingaji mwenyewe au kwa niaba yake.

Agizo ya kuleta mahakamani makaratasi yahusuyo wosia

**60**.-(1) Mahakama inaweza ikatoa amri kwa mtu yeyote kutoa au kuleta mahakamani karatasi yeyote au maandishi ambayo au yanasemakana kuwa ni wosia, ambayo imesemekana kuwa ipo katika umiliki au chini ya uangalizi wa mtu huyo.

(2) Kama haitaonyeshwa kuwa karatasi yoyote au maandishi yapo katika umiliki au chini ya uangalizi wa mtu huyo, lakini kuna sababu ya kuamini kuwa ana uelewa wa uwepo wa karatasi hiyo au maandishi au ya wosia wa mdomo, mahakama itamuhitaji mtu huyo aje mahakamani kwa dhumuni la kuchunguzwa kuhusiana na suala hilo, na mtu huyo atatakiwa ajibu maswali kadri yatakavoulizwa kwake na mahakama na, kama ikiamriwa, kutoa karatasi hiyo au maandishi yaliyo katika umiliki wake au chini ya uangalizi wake.

Mahakama inaweza ikamchunguza mleta maombi, au ikahitaji ushahidi wa ziada na kutoa wito

**61**.-(1) Katika hali yoyote itakuwa halali kwa Mahakama, kama ikiona ni sawa-

(d) kumchunguza muombaji mwenyewe chini ya kiapo;

(e) kuhitaji ushahidi mwingine kuhusiana na kifo cha marehemu na usimamizi sahihi wa wosiawosia, au haki ya mleta maombi kuhusiana na hati za usimamizi, kama hali

itakavokuuwa; na

(f) Kutoa wito wa kuita watu wote au wale wanaodai wana masilahi katika mali ya marehemu waje waone mwenendo wa shauri kabla ya utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi.

(2) Wito utawekwa katika mahali pa wazi katika Mahakama, na viginevyo kuchapishwa au kufanywa ujulikane katika namna ambayo kanuni za uthibitisho wa wosia zitakavyoelekeza au Mahakama itakavyotoa maelekezo hayo.

Muda kabla toleo halijafanywa

**62**. Uthibitishwaji wa usimamizi wa mirathi unaotokana na Wosia hauwezi kutolewa mpaka kumalizika kwa siku saba, na barua ya usimamizi wa mirathi haiwezi kutolewa mpaka siku kumi na nne kumalizika, tangu mtoa Wosia au yule ambaye hakuacha Wosia kufariki.

Utolewaji wa uthibitisho wa wosia na usimamizi

**64.** Pale ikitokea kwa Mahakama kwamba uthibitishwaji wa msimamizi wa mirathi anayetokana na Wosia au barua ya usimamizi wa mirathi inatakiwa kutolewa, uthibitishwaji huo au usimamizi huo utatolewa chini ya muhuri wa Mahakama

Kukataa kutoa hati za usimamizi

**64**. Pasipo kuathiri kifungu chochote, Mahakama itakuwa na utashi wa kutoa amri, huku ikitoa sababu zilizo katika maandishi, kukataa maombi ya kutoa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mujibu wa Sheria hii.

Maelekezo kwa wasii au msimamizi

**65**. Mahakama inaweza kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa msimamizi wa mirathi juu ya mali ya marehemu au juu ya usimamizi wa mali hiyo.

Kiapo

**66**. Baada ya kuthibitishwa usimamizi wa mirathi kupitia Wosia au barua ya usimamizi wa mirathi, yule aliyepewa usimamizi atatakiwa kula kiapo cha uaminifu wa kusimamia mali za marehemu

Isipokuwa kifungu hiki hakitatumika pale mpewaji atakapokuwa ni muamana wa serikali au kabidhi-wasihi

Dhamana ya usimamiaji

**68.** Mtu yeyote ambaye amepewa hati za usimamizi na, kama Mahakama itaelekeza, mtu yeyote ambaye amepewa uthibitisho wa wosia atatoa dhamana akiwa mmoja au wadhamini zaidi, katika ukusanyaji, na katika usimamizi wa mali za marehemu

Isipokuwa Mahakama inaweza, kwa sababu nzuri, ikaachilia mbali suala la dhamana na wadhamini, au vyote, katika hali husika.

Kumpa mtu mwingine dhamana ya usimamizi

**68**. Mahakama inaweza, kutokana na maombi yaliyoletwa na ikijiridhisha kuwa uwekwaji wa dhamana haujafutwa, na kulingana na masharti ya dhamana, au kwamba pesa iliyopokelewa ilipwe katika Mahakama, au vinginevyo kama Mahakama inavyoona sawa, ikaweka watu fulani, ambao wataweza kufungua mashtaka katika dhamana hiyo kwa jina lake kana kwamba alipewa dhamana hiyo kwa mara ya kwanza na si Mahakama, na atatakiwa apokee, kama muamana wa watu wote wenye masilahi, kiasi chote kinachotakiwa katika uvunjwaji huo.

Matunzo ya

**69**. Wosia zote halali ambazo uthibitisho wa wosia na hati za

wosia halisi

usimamizi zilizoambatanishwa na wosia zimetolewa na Mahakama zitatunzwa na kuhifadhiwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na wosia wowote uliowekwa na nakala za kutolewa kwa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi, sambamba na uangalizi wa Mahakama Kuu na vifungu vya kanuni za uthibitisho wa wosia, zitakuwa wazi kwa ukaguzi.

Hitimisho la uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi

**70.** Uthibitisho wa wosia na hati ya usimamizi wa mirathi vitakuwa-

(d) Na nguvu kwa mali zote za marehemu zile zinazohamishika na zisizo hamishika zinazopatikana sehemu yeyote Tanzania

(e) Uthibitisho wa mwisho wa uwakilishi juu ya madeni yoyote ya marehemu, na watu wengine wanaoshikilia vitu ambavyo ni mali za marehemu

(f) Itawarudishia wadeni kwa kuwalipa madeni yao, na watu wote wanaoleta mali kwa mtu ambaye uthibitisho wa wosia au hati ya usimamizi wa mirathi umeshatolewa

Mpewaji pekee atakuwa muwakilishi

**71**. Baada ya uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi kutolewa, hakuna mtu zaidi ya yule ambaye usimamizi umetolewa atakaye kuwa na nguvu za kushitaki au kuendesha mashtaka yoyote, au vinginevyo kujifanya kuwa ni msimamizi wa marehemu, mpaka pale uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi itakapotenguliwa au kubatilishwa.

Rufaa na marudio

**72**.-(1) Rufaa itahusu amri ya kutoa au kupinga utolewaji wa wosia au hati ya usimamizi iliyofanyika katika mirathi inayobishaniwa kama kwamba agizo ni amri, na kutoka kwenye agizo lolote lililofikiwa katika hali ambayo rufaa ingekatwa kutokana na vipengele vya Sheria ya Daawa au Sheria yoyote itakayo ipokea Sheria hiyo.

Sura ya 33

Sura ya 33

(2) Vifungu vya Sheria ya Daawa vitatumika pamoja na mabadiliko yatakayobidi, kuhusiana ma mienendo ya shauri mbele ya mteule wa wilaya katika Sheria hii

## SEHEMU YA VIII
## B. MAZOEA NA HATUA ZA KUCHAGUA NA KUPINGWA UCHAGUZI WA, WASIMAMIZI KATIKA MALI CHACHE

Matumizi ya sehemu ya VIII

**73**.-(1) Sehemu hii itatumika pindi maombi yatakapofanyika mbele ya Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi kwa uchaguzi wa msimamizi wa mali chache, au pale maelekezo yatakapo tolewa, katika sehemu ya XI, kwamba sehemu hii itatumika katika mali chache husika.

(2) Isipokuwa kama itakavyotolewa katika sehemu hii, pale ambapo SEHEMU hii itatumika, vifungu vya sehemu ya IV, V, VI, na

VII (tofauti na vifungu vya 52(b), 60, 61, 62, 65, 70 na 71 havitatumika.

(3) Ikiwa sehemu hii itatumika Mahakama ya wilaya itatumia mamlaka yake yaliyowekwa katika Mahakama hiyo katika vifungu vya sehemu ya VII ambavyo vitatumika.

Uchaguzi wa wasimamizi

**74**. Mahakama ya wilaya inaweza ikamchagua kama msimamizi mtu mmoja au wengi wenye masilahi na mali katika usimamizi unaotakiwa na, katika kumchagua msimamizi huyo, isipokuwa kama kwa sababu yoyote inaona si vema kufanya hivyo, itazingatia mapendekezo yoyote ambayo yanaweza yakawa yamesemwa na marehemu.

Usimamizi wa kabidhi-wasihi, na uchaguzi wa afisa wa Mahakama au mtu asiye na masilahi

**75**.-(1)Pale ambapo Mahakama ya wilaya itakuwa na wazo kuwa, kwa kuchukulia a usalama wa mali na usimamizi unaotakiwa, inafaa kwamba mali isimamiwe na kabidhi-wasihi au afisa wa Mahakama ya wilaya, au mtu anayeheshimiwa na muadilifu anayeweza na aliye tayari kusimamia mali hizo, itaaahirisha maombi ya kumchagua msimamizi ili iweze kujiridhisha kuwa kabidhi wasihi atachukua usimamizi huo katika kifungu cha 52 cha Sheria ya Kabidhi Wasihi (Mamlaka na Majukumu)

Sura ya 27

au kumchagua afisa wa Mahakama ya wilaya au mtu yeyote kama ilivyooneshwa kwa msimamizi.

(2) Uchaguzi wa msimamizi katika sehemu hii hautafanyika kama kulikuwa na toleo lingine la uthibitisho wa mirathi au hati za usimamizi wa mirathi, au kama kabidhi wasihi amechukua usimamizi huo kihalali.

Uteuzi uwe na muhuri

**76**.-(1) Uteuzi wa msimamizi wa mirathi ndogo utafanyika chini ya muhuri wa Mahakama ya wilaya

(2) Kila msimamizi ataweka saini kwamba atasimamia mali za marehemu kwa uaminifu

Dhamana kwa usimamizi thabiti

**77**. Mahakama ya Wilaya, pale itakapoona inafaa, inaweza kumtaka msimamizi wa mirathi ndogo kuweka dhamana ili kuweza kusimamia mali za marehemu.

Wosia

**78**.-(1) Mahakama ya Wilaya inaweza kuruhusu Wosia kutolewa kwa ushahidi wa kuzungumza au kwa kiapo, na inaweza kukubali uthibitishwaji wa maelezo yaliyo katika Wosia huo ambayo yanaonekana ni ya msingi japo si ushahidi wa kisheria

(2) Nakala ya wosia, au kama wosia wa mdomo, maandishi ya maneno ya marehemu yataambatanishwa katika uchaguzi wa msimamizi

(3) Wasii halisi utawekwa na kutunzwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na kifungu cha 69 kitatumika, pamoja na mabadiliko yaliyobidi, katika wosia hizo na nakala za uchaguzi uliofanywa katika sehemu hii.

Uteuzi unaweza

**79**.Uteuzi wa msimamizi wa mirathi chini ya sehemu

kuwa kwa mali yote au sehemu ya mali hiyo

hii,inaweza kumpa usimamizi wa mali zote za marehemu au sehemu ya mali hizo zilizoorodheshwa katika uteuzi, na utakuwa na nguvu sehemu yoyote ile katika Tanzania

Madhara ya Uteuzi

**80**.-(1) Uteuzi wa msimamizi katika sehemu hii utaweka mali za marehemu chini ya msimamizi, ambaye, atakuwa na mamlaka sambamba na wajibu wote kama kwamba hati za usimamizi wa mali imepewa kwake.

(2) Msimamizi aliyechaguliwa katika sehemu hii, isipokuwa kama Mahakama ya wilaya ambayo imemchagua au vinginevyo itaamuru, hatatakiwa kupeleka orodha au mahesabu au kuweka dhamana.

(3) Kama msimamizi atatakiwa kupeleka orodha au mahesabu, kifungu cha 103 kitatumika kama kwamba Mahakama ya wilaya imetoa hati za usimamizi wa wosia kwa msimamizi

Mali zisizodaiwa

**81**. Msimamizi aliyechaguliwa katika sehemu hii ambaye ana mali katika himaya yake ambazo hakuna mdai halali kwa mwaka mmoja toka kifo cha mtoa wosia atamtaarifu Kabidhi- Wasii, na kama itahitajika Kabidhi- Wasii atazihamisha mali hizo kwa Kabidhi-Wasii, na mali hizo zitasimamiwa sambamba na vifungu vya 48 na 49 vya Sheria ya Kabidhi- Wasii (Mamlaka na Majukumu).

Sura ya 27

Utenguzi wa uteuzi

**82**. Uchaguzi wa msimamizi unaweza ukatenguliwa na Mahakama ya wilaya ambayo ilimchagua kwa sababu yeyote ambayo itaridhisha kutenguliwa kwa hati ya uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi au uondoaji wa wasii, na hali kama hizo.

Rufaa ziende Mahakama Kuu

**83**.-(1) Sambamba na Kanuni za Uthibitisho wa Wosia, kila uchaguzi, muongozo, au uamuzi wa Mahakama ya wilaya katika sehemu hili unaweza ukakatiwa rufaa katika Mahakama Kuu

(2) Kanuni za Uthibitisho wa wosia zinaweza zikazuia au zitatoa muongozo kuhusiana na haki ya kukata rufaa kwa kiasi chochote na hali yoyote.

Mahakama ya wilaya kutuma ripoti Mahakama Kuu

**84**. Kila Mahakama ya wilaya itapeleka ripoti ya mienendo yote katika sehemu hii Mahakama Kuu kama itakavyoonyeshwa na Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi

Uzuiaji wa kutoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika mali chache

**85**.-(1) Kama msimamizi wa mali chache amechaguliwa katika sehemu hii, hakuna uthibitisho wa wosia wa marehemu au hati za usimamizi wa mali zake utakaotolewa-

(c) na mteule wa wilaya, isipokuwa kama ya uchaguzi wa msimamizi umevunjwa na Mahakama ya wilaya ambayo ilimchagua; au

(d) na Mahakama Kuu isipokuwa kama ikiona kuwa utoaji huo ni muhimu katika kufikia haki, au katika kumlinda mnufaishwaji yeyote au mdeni

(2) Utolewaji na Mahakama Kuu wa uthibitisho wa wosia wa

marehemu au hati za usimamizi wa mali yake hutabatilisha uchaguzi wowote wa msimamizi katika sehemu hii. Na ubatilisho huo utakuwa na nguvu sawa kama ubatilishwaji wa hati za usimamizi.

(3) Isipokuwa kama inavyotolewa katika kifungu cha 86, hakuna kitu katika sehemu hii kitakachoathiri mamlaka ya kutoa au kubatilisha uthibitisho wa wosia wa marehemu au hati za usimamizi wa mali zake.

Uhalali wa uteuzi katika mali zinazozidi shilingi elfu kumi

**86**.-(1) Hakuna uteuzi wa wasimamizi katika sehemu hii utakaokuwa batili kwa sababu tu imejulikana kuwa thamani ya mali ya marehemu imezidi shilingi elfu kumi, lakini, Mahakama ya wilaya ikilijua hilo itatoa ripoti Mahakama Kuu, ambayo kama itaona sawa itatoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi.

(2) Kama Mahakama Kuu ikitoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika kifungu hiki, kifungu kidogo cha (2) 85 kitatumika.

Usimamizi wa mali chini ya shilingi elfu moja

**87.**-(1) Ikiwa thamani ya mali ni chini ya shilingi elfu moja haitakuwa na umuhimu wa kumchagua msimamizi, na mali hizo zitasimamiwa na mwenza wa marehemu aliyebaki au, kama hakuna mwenza, ndugu wa karibu wa marehemu ambaye yuko tayari, ambaye kwa dhumuni hilo atakuwa ameteuliwa kuwa msimamizi wa mali hiyo.

Ila kama Sheria hii inatumika katika sehemu ya IX, mtu atakayesimamia mali hiyo atakuwa ni ndugu wa kiume wa karibu wa marehemu;

Ila waziri kama akiona yafaa, ataagiza katika gazeti la serikali, kuongeza pesa itakayosimamiwa katika kifungu hiki.

(2) Kama Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi kuhusiana na mali yoyote chini ya mamlaka yake, anaweza kuzuia au kutoa mwongozo katika utekelezaji wa majukumu yaliyowekwa na kifungu hiki na anaweza akamuweka mtu yeyote badala ya mwenza au ndugu wa karibu, kama hali itakavyokuwa, kusimamia mali hiyo, ikiwa kwa mawazo ya Mahakama ubadilishwaji huo ni wa muhimu kuendana na mazoea na mila ambazo zinatumika na pande za mashitaka katika shauri hilo au inahitajika kwa sababu nyingine.

## B. USIMAMIZI WA MALI CHACHE

Sura ya 30

Sheria inayotumika kwa mtu wa kabila fulani

**88**.-(1) Mali yoyote ya marehemu, kutokana na agizo na maelekezo ya sehemu ya IX, zitasimamiwa kutokana na vifungu vifuatavyo-

Namba 33 ya mwaka 1947 kifungu cha 5; 35 cha mwaka 1961 jedwali la pili; sura

(c) Mali ya mtu wa kabila fulani zitasimamiwa kutokana na Sheria za kabila hilo isipokuwa kama marehemu katika muda wowote alikuwa ni mfuasi wa dini ya kiislam na

ya 277 kifungu cha 3 { sura ya 30 vifungu vya 19,20,na 21}

Mahakama yenye mamlaka na mali yake imejiridhisha kutokana na maneno au maandishi ya marehemu au matendo yake au aina ya maisha yake kuwa marehemu alikuwa na nia ya kuwa mali isimamiwe, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa kufuata Sheria za kiislam, na kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria hiyo.

(d) Mali ya mswahili itasimamiwa kwa kufuata Sheria za kiislam isipokuwa Mahakama iliyo na mamlaka na mali hiyo imejiridhisha kuwa kutokana na maneno au maandishi ya marehemu au matendo yake au aina ya maisha alikuwa na nia kuwa mali yake isimamiwe, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa kufuata Sheria za kimila, na kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria za kimila.

(2) Kama mtu yeyote katika muda wowote ambaye Sheria hii inatumika katika mali yake kwa ajili ya agizo, au maelekezo katika sehemu ya ix alikuwa anaamini katika dini ya kikristu, na Mahakama iliyo na mamalaka na mali yake imejiridhisha kuwa marehemu alikuwa ana nia ya Sheria zinazotumika Tanzania kwa watu wanaoamini dini ya kikristu zitumike katika usimamizi wa mali yake, aidha yote au sehemu ya mali hiyo, kwa hali hiyo mali itasimamiwa, aidha yote au sehemu yake, kama hali itakavyokuwa, kwa kutumia Sheria hiyo

(3) Rais anaweza, kama akiona sawa, baada ya muda fulani, kwa agizo litakalochapishwa katika gazeti la Serikali, kusema ipi ni Sheria ya kabila, ikiwa kwa ujumla wake au katika kipengele maalum

(4) Bila kujali Sheria yoyote ya mila au ya kiislam tofauti-

(c) kila mdai atakuwa na haki katika mali ya marehemu (ikijumuishwa haki ya kufuata mali); na

(d) Mtu yeyote hatanyimwa haki yake ya kurithi kitu chochote kwa sababu tu mtu huyo amejitoa katika dini fulani

Wosia wa mtu wa kabila

**89**.-(1) Katika usimamizi wa mali za marehemu, kwa kufuata agizo au maelekezo ya sehemu ya IX ya Sheria hii, mgao wowote wa mali unaogawa sehemu yoyote ya mali utatambuliwa kama wasii, kama utatimiza mahitaji haya-

(d) kama mali itasimamiwa kwa kutumia Sheria za kimila kama aidha-

(i) Ugawaji unatambuliwa kuwa halali na Sheria hiyo ya mila; au

(ii) Ugawaji ni halali kwa kufuata maelekezo ya

agizo la Waziri, ambapo linasema kuwa ugawaji wa mali, ulifanywa na marehemu au na mtu yeyote wa tabaka fulani ambalo linamjumuisha marehemu na limefanywa kwa kuzingatia Sheria ya Indian Succession Act, 1865, inayohusu wasii, na wa kiasi na vikwazo vitakavyowekwa ili uweze kuwa halali.

(e) ikiwa mali itasimamiwa kutokana na Sheria inayotumika kwa mali za watu wanaoamini dini ya kikristo, kama mgao huo umefanywa kwa kuzingatia vifungu vya Indian Succession Act, 1865, inayohusu wasii; na

(f) Ikiwa mali itasimamiwa kwa kuzingatia Sheria za kiislam, kama mgao utajulikana kuwa ni wa halali na Sheria hiyo.

(2) Ugawaji wa mali ambao kifungu hiki kinatumika, hautafuatwa mpaka uwe umethibitishwa kuwa ni halali na Mahakama iliyo na mamlaka katika mali hiyo

(3) Uhalisia wa ugawaji uliotajwa kuwa ni halali katika kifungu hiki, kama upo katika maandishi, utatunzwa na Mahakama; katika hali ambayo itakuwa imetolewa na kanuni za Mahakama, na nakala ya wosia atapewa msimamizi wa mali hiyo.

(4) Ikiwa mgao wowote wa mdomo umetajwa kuwa ni wa halali katika kifungu hiki, mgao huo utawekwa katika maandishi na Mahakama, na nakala moja atapewa msimamizi wa mali hiyo.

{Imefutwa na sura ya 277 kifungu cha 5; sheria namba 35 ya 1961 ya jedwali la pili}

**90**. (Sheria inayotumika katika mali za wasomali}

Imefutwa na sheria na 33 ya mwaka 1947 kifungu cha 35 cha mwaka 1961 jedwali la pili}

**91.** {Rejea sura ya 16 iliyofanyiwa mabadiliko 1928, katika sheria zingine}

## SEHEMU YA IX
## MALI ZINAZOSIMAMIWA KWA KUTUMIA SHERIA ZA KITAMADUNI, MILA NA SHERIA ZA KIISLAM

Hali ambazo Sheria hii itatumika kwa mali zinazosimamiwa kwa Sheria za kimila namba 9 ya 1963; 9 ya 1965
Sura ya 29

**92**.-(1) Vifungu vya Sheria hii havitatumika katika usimamizi wa mali ambazo Mahakama ya mwanzo ina mamlaka isipokuwa-

(d) kama waziri, akitoa agizo litakalochapishwa katika gazeti la serikali, kuwa itatumika katika aina fulani ya mali, au mali zilizopo mahali fulani, katika mali fulani zilizopo mahakama fulani; au

(e) Mahakama Kuu, aidha yenyewe au kwa maombi ya Mahakama ya wilaya, au mali ikiwa si mali chache, ya mtu mwenye masilahi, ikitoa maelekezo kuwa itatumika; au

(f) Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu mkazi, yenyewe au kutokana na maombi ya mtu yeyote mwenye masilahi, ikitoa maelekezo kuwa itumike katika mali fulani chache,

katika hali hiyo vifungu vya Sheria hii vitatumika kwa namna na kiasi ambacho Sheria hii imetaja

Ila Mahakama ya wilaya haitatoa maelekezo yoyote katika aya ya (c) ya hiki kifungu kidogo ikiwa agizo la usimamizi wa mirathi limefanywa, au mwenendo kuhusiana na urithi umeanza katika Mahakama ya mwanzo, isipokuwa kama mwenendo umehamishiwa katika Mahakama ya wilaya katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mahakimu wa Mahakama

Sura ya 11

(2) Ikiwa Mahakama imetoa mwongozo kwamba Sheria hii itatumika, yenyewe itakuwa na mamlaka ya mwanzo kuhusiana na mali hiyo, au itatoa agizo kwa mteule wa wilaya awe na mamlaka (na aidha katika hali zote vifungu vya Sheria hii tofauti na SEHEMU YA VIII, vitatumika) au inaweza kama mali ni chache, itaiamuru Mahakama ya wilaya inayokaliwa na hakimu wa wilaya iwe na mamlaka (ambapo vifungu vya Sheria hii tofauti na sehemu ya IV,V na VI na vifungu vya 51 (1), 53, mpaka 59 (kwa pamoja), 63,64,66, mpaka 69 (kwa pamoja) na 72 vitatumika)

(3) (Imefutwa na Sheria namba 55 ya mwaka 1963:Sura ya 537)

Madhara ya maelekezo ya Mahakama Kuu kwa agizo lililofanywa na Mahakama ya mwanzo

**93**.-(1) Ikiwa agizo la kusimamia mali limefanywa na, au mwenendo kuhusiana na mirathi umeshaanzishwa katika Mahakama ya mwanzo, Mahakama Kuu haitatoa agizo lolote katika aya (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 88 isipokuwa kama ikiona ni sawa kwa masilahi ya haki au kwa ulinzi wa mnufaishwaji yeyote au mdai mali hiyo isimamiwe kwa kutumia Sheria hii.

(2) Kama Mahakama Kuu imetoa agizo lolote katika mazingira yoyote ambayo yamekwishasemwa, itaijulisha Mahakama ya mwanzo ambayo agizo la usimamizi lilitolewa, au mashtaka yalipoanzishwa, kama hali itakavyokuwa, au kusitisha mwenendo huo mpaka utoaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi ukamilike, au msimamizi amechaguliwa katika Sheria hii.

(3) Ikiwa agizo la usimamizi limepingwa na Mahakama ya mwanzo chini ya kifungu hiki, malipo yote ya halali yaliyofanywa na mtu aliyekuwa akitekeleza agizo hilo, bila kuzingatia upingwaji huo, yatakuwa ni malipo halali kwa mtu aliyeyafanya, na mtu anayestahili kutimiza agizo hilo atakuwa na mamlaka ya kujilipa kana kwamba alikuwa ni msimamizi ambaye usimamizi wake umepingwa katika sehemu ya VI.

## SEHEMU YA X
## USAJILI WA MIRATHI NA HATI ZA USIMAMIZI

Tafsiri

**94**. Katika sehemu hili na kifungu cha 4-

"Mahakama ya uthibitisho wa wosia" inamaanisha Mahakama yoyote au mamlaka, kwa jina lolote linalojulikana, ambayo ina mamlaka katika masuala ya uthibitisho wa wosia.

"Uthibitisho wa wosia" na "hati za usimamizi" inajumuisha uthibitishwaji na Sheria yoyote katika Jumuiya ya Madola ambayo uwiano sawa katika Sheria hii unapewa katika uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi

Usajili wa uthibitisho wa mirathi na hati za usimamizi zilizotolewa nje ya Tanzania

**95**. Ikiwa Mahakama ya uthibitisho wa wosia katika sehemu yoyote ya Jumuiya ya Madola, aidha kabla au baada ya kupitishwa kwa Sheria hii, imetoa uthibitisho wosia au hati za usimamizi kuhusiana na mali ya marehemu, na uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi zilizotolewa, kama iliyotolewa na nakala yake ikapelekwa Mahakama Kuu, na kusajiliwa na muhuri wa Mahakama hiyo, itakuwa na nguvu na mamlaka sawa katika Tanzania kama imetolewa na Mahakama hiyo.

Masharti ya kuzingatiwa kabla ya kusajili

**96.** Mahakama Kuu, kabla ya kusajili uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi katika sehemu hii, itajiridhisha ikiwa ni hati za usimamizi kuwa dhamana imetolewa kwa kiasi kinachotosheleza kuilinda mali hiyo, kama ipo, Tanzania, na katika hali yoyote inaweza ikaomba ushahidi kama itakavyoona sawa, juu ya makazi ya marehemu.

Dhamana

**97.** Mahakama Kuu, kama ikiona sawa, ikiwa kuna maombi ya mdai yeyote, itahitaji kabla ya usajili, dhamana iwekwe kwa ulipaji wa madeni yaliyofikiwa muda wake kutoka kwenye mali kwa mdeni anayeishi Tanzania

Nakala zilizodurufiwa na kunakiliwa

**98**. Kwa dhumuni la Sheria hii, rudufu ya uthibitisho wa wasii au hati za usimamizi iliyosajiliwa na muhuri wa Mahakama iliyotoa vitu hivyo, au nakala iliyothibitishwa kuwa sahihi au chini ya mamlaka ya Mahakama iliyotoa vitu hivyo, vitakuwa na nguvu sawa kama nyaraka halisi.

## SEHEMU YA XI

## MAMLAKA NA MAJUKUMU YA WASII NA WASIMAMIZI

Namna na mali za wasii au msimamizi

**99**. Wasii au msimamizi wa marehemu, kwa hali yoyote, ni muwakilishi wa marehemu kwa dhumuni lolote,na mali zote za marehemu zitakuwa chini ya uangalizi wake

Isipokuwa, kifungu hiki hakimuwekei wasii au msimamizi-

(c) kitu chochote cha marehemu ambacho kinatakiwa kwenda kwa mhalifiwa.

(d) Kitu chochote kilichowekwa chini ya kampuni

Mamlaka juu ya mashitaka na madeni

**100**. Wasii au msimamizi ana mamlaka ya kushitaki kuhusiana na mashitaka yote yaliyoachwa na marehemu, na ana mamlaka ya kudai madeni yaliyofikiwa muda wa kulipwa wakati marehemu anafariki, kama alivyokuwa marehemu wakati wa uhai wake.

Mamlaka ya kuuza mali na kadhalika

**101**.Wasii au msimamizi anayo mamlaka , kutokana na mali iliyowekwa chini yake katika kifungu cha 99, ya kuuza kitu kinachohamishika, kama anavyoona ni sawa, na mamlaka na kuuza, kuweka rehani, kupangisha kuhusiana na mali isiyo hamishika iliyowekwa na Sheria iliyoandikwa juu ya muamana ya amana inayouzwa.

Matumizi ya uangalizi na usimamizi

**102**.Wasii au msimamizi anaweza, juu ya mamlaka nyingine ya matumizi yanayofanywa kihalali na yeye, kuingia gharama-

(c) kwa vitendo vile kama vitakavyokuwa sawa kwa utunzaji wa kitu chochote kinachohusu mali ya marehemu; na

(d) Kwa ruhusa ya Mahakama, au ya Mahakama ya wilaya iliyo na mamlaka katika shauri, juu ya vitu vilivyotolewa kidini, msaada au vitu vingine, na kwa maboresho, kama itakavyokuwa sawa na inavyotakiwa na vitu hivyo.

Wasii au msimamizi wasipate faida yoyote katika ofisi

**103**.-(1)Isipokuwa kama imesemwa waziwazi katika wosia, hakuna wasii au msimamizi anayetakiwa ajinufaishe kifedha kutoka katika ofisi ya usimamizi

(2) Kama wasii au msaidizi akinunua, moja kwa moja au vinginevyo, sehemu yoyote ya mali za marehemu, mauzo hayo yanaweza kubatilika kama kuna mtu mwingine ana masilahi na kitu hicho au mapato ya kitu hicho.

(3) Hakuna chochote katika kifungu hiki, kitakachotumika kwa ada yoyote iliyosemwa na Sheria.

Mamlaka ya wasii au wasimamizi yanaweza kufanywa na mtu mmoja

**104**. Ikiwa kuna wasii au wasimamizi, mamlaka yao yote yanaweza, kukiwa hakuna lolote ndani ya wosia au katika hati za usimamizi wa mirathi, kufanywa na mmoja wao aliyethibitisha wosia au aliyechukua usimamizi.

Mamlaka ya

**105.** Kwa kuondoa shaka, inatamkwa kuwa-

(c) msimamizi wa vitu ambavyo havijasimamiwa anayo

muwakilishi mahususi

mamlaka kuhusiana na vitu hivyo sawa na yule wasii au msimamizi wa kwanza; na

(d) Msimamizi ambaye amepewa usimamizi kutokana na kifungu cha 36 wakati wa utoto ana mamlaka yote ya wasii wa kawaida au msimamizi.

Orodha na mahesabu

**107**.-(1) Wasii au msimamizi, ndani ya miezi sita ya kupewa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, au katika muda ambao Mahakama iliyotoa usimamizi huo itahitaji, atatakiwa alete orodha ya vielelezo, vinavyoonesha vitu vyote vilivyo chini yake, na mikopo yote, na madeni yote aliyonayo mtu yeyote ambapo wasii au msimamizi anatakiwa katika mwaka mmoja baada ya kupewa usimamizi au kwa muda ule ambao Mahakama itahitaji, atoe mahesabu yanayoonyesha mali zilizokuja kwenye mikono yake na jinsi gani amevigawa.

(2) Kama usimamizi haujakamilika katika mwaka mmoja baada ya kutoa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi, wasii au msimamizi katika kipindi kisichozidi miezi sita, au katika muda wowote ambao Mahakama iliyotoa usimamizi huo itachagua, na baada ya kumaliza usimamizi, atatakiwa atoe vidhibiti vya hesabu vikionyesha mali ambazo zimepitia mikononi mwa msimamizi na namna ambavyo zimetumiwa tangu hesabu za mwanzo zitolewe.

(3) Kama wasii au msimamizi, akitakiwa na Mahakama kutoa orodha au hesabu katika kifungu hiki, akaacha kuitikia wito katika muda uliopangwa, atakuwa ametenda kosa la jinai, na akitiwa hatiani atatakiwa atoe fidia isiyopungua shilingi elfu mbili au atumikie kifungo kisichozidi miezi sita.

(4) Kama wasii au msimamizi akitoa orodha au hesabu za uongo huku akijua kuwa ni za uwongo katika kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa la jinai na kama atakutwa na hatia atatakiwa atumikie kifungo cha muda usiozidi miaka saba.

(5) Mnufaishwaji yeyote katika wosia, au mtu anayetakiwa apate sehemu ya mali katika urithi usiokuwa na wosia, au mdai ambaye hajaridhika anayo ruhusa ya kukagua orodha na mahesabu ya wasii au msimamizi.

(6) Kipengele hiki hakitatumika kwa kabidhi-wasii isipokuwa kama Mahakama itatoa maelekezo hayo.

Shughuli za ujumla za usimamizi

**108**.-(1) Wasii au msimamizi, anatakiwa, kwa uadilifu unaotakiwa, akusanye mali za marehemu, na madeni ambayo yamefika muda wake, alipe madeni ya marehemu na madeni na gharama za usimamizi, na kugawanya mali kwa watu au kwa dhumuni linaloendana na hilo au muamana kwa ajili ya watu hao au dhumuni au kwa kufuatisha vifungu vya Sheria hii kama itakavyotakiwa.

(2) Sambamba na vifungu vya Sheria hii, wasii au msimamizi hatakiwi kugawa mali za marehemu kabla ya kuisha kwa mwaka mmoja baada ya kifo cha marehemu.

Namna ya ulipaji wa madeni

**109**. Madeni yatalipwa kwa mpango ufuatao, kabla ya madeni yote-

(d) kwanza, gharama za mazishi kwa kiasi kinachotakiwa, kufuatana na hali ya marehemu, na gharama za kuuguzwa, zikijumuisha gharama za tiba, usafiri na malazi kwa mwezi mmoja kabla ya kifo chake.

(e) pili, gharama za kupata uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi, ikijumuisha gharama zilizotumika kuhusiana na mienendo yoyote ya Mahakama inayotakiwa ifanyike kwa ajili ya usimamizi wa mali; na

(f) tatu, ujira unaotakiwa kulipwa kwa kazi alizofanyiwa marehemu na mfanyakazi yoyoye, kibarua au mtumishi wa ndani, ndani ya miezi minne kabla ya kifo chake.

(2) Baada ya kulipa madeni yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1), kisha yatalipwa madeni mengine yeyote ya marehemu kulingana na jinsi yalivyoingiwa

(3) Sambamba na kilichoelezwa katika kifungu hiki, wasii au msaidizi atalipa madeni yote anayoyajua, kwa usawa na kwa idadi sawa, kama vile mali za marehemu zinavyoweza kutosha.

Madeni yalipwe kabla ya wausiwa

**110**.-(1) Madeni ya kila namna yatalipwa mbele ya muusiwa yoyote.

(2) Kama mali ya marehemu, inatakiwa ilipe madeni ya mbeleni, wasii au msimamizi hatatakiwa kulipa urithi wowote bila kuwa na malipo ya kutosha ya kulipa madeni kwa muda wowote yatakapojitokeza.

Kupungua kwa hiba wazi na usawa wa wausiwa

**111**.-(1) Kama mali, baada ya kulipa madeni, matumizi ya muhimu na hiba mahususi, hazitoshi kulipia hiba za wazi kwa kiasi kinachotakiwa, hiba ya wazi itapunguzwa kwa urari.

(2) Kama hakuna maelekezo mengine tofauti katika wosia, wasii hana haki ya kumlipa muusiwa mmoja na kumuacha mwingine au kubaki na pesa yoyote ya hiba yeye mwenyewe au kwa mtu yeyote ambaye ni muusiwa.

(3) Kwa dhumuni la mapunguzo, hiba ya maisha, kiasi kilichotengwa na wosia kitatoa malipo ya mwaka, na gharama ya malipo ya mwaka ikiwa hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili hiyo, kitakuwa kama hiba za wazi.

Kupunguwa kwa hiba mahususi

**112**.-(1) Ikiwa kuna hiba mahususi, na mali zinatosha kulipa madeni na matumizi ya muhimu, kitu kilichotajwa lazima kitolewe kwa muusiwa bila punguzo lolote.

(2) Ikiwa mali hazitoshi kulipa madeni na matumizi na hiba mahususi, punguzo litafanywa kutoka katika hiba mahususi kwa urari wa kiasi chake

Haki ya hiba maalum

**113**. Ikiwa kuna hiba maalumu, na mali zinatosha kulipa madeni na matumizi ya muhimu, muusiwa atakuwa na dai la juu la kulipwa hiba yake kutoka katika pesa ambazo anatakiwa kulipwa mpaka pesa hizo zitakapokwisha, na kama mpaka mali hizo

zinakwisha sehemu ya hiba hiyo haijalipwa, anaruhusiwa, kudai baki kwenye mali ya jumla juu ya hiba yake ambayo haijalipwa

SEHEMU YA XII
HIBA NA MALIPO YA MWAKA

Ridhaa ya inahitajika kwa muusiwa kupata hiba yake

**114**.-(1) Ridhaa ya wasii ni muhimu kwa muusiwa kuwa na haki na hiba yake.

(2) Ridhaa ya wasii katika hiba inaweza kuwa yenye sharti, na kama ina sharti lile ni lile linalotimilizika na kama halitatimizwa, hakuna ridhaa.

Ridhaa kwa hiba mahsusi

**115**.-(1) Ridhaa ya wasii katika urithi mahususi itatosha kuondoa masilahi yake kama wasii, na kuiweka mali hiyo kwa muusiwa, isipokuwa kama hali au mazingira ya mali yanahitaji mali hiyo iwekwe kwake kwa namna fulani

(2) Ridhaa inaweza kuwa ya mdomo, na inaweza kuwa ya moja kwa moja au kwa kuangalia matendo ya wasii.

Ridhaa kwa hiba ya wasii mwenyewe

**116**.-(1) Ikiwa wasii ni muusiwa, ridhaa yake inatakiwa ili apate hiba yake, katika njia ileile inayotakiwa ili kukamilisha urithi kwa mtu mwingine, na ridhaa hiyo yaweza kuwa iliyo wazi au ya vitendo.

(2) Ridhaa itakuwa ya vitendo kama katika hali ya kusimamia mirathi wasii akafanya kitendo chochote kinachoashiria tabia yake kama muusiwa na si kama wasii

Madhara ya ridhaa ya wasii

**117**. Ridhaa ya wasii katika hiba itaipa utambuzi toka kifo cha marehemu.

Kuanza kwa malipo ya malipo ya mwaka kama muda haujapangwa na wosia

**118**. Ikiwa malipo ya mwaka yametolewa na wasii, na hakuna muda uliowekwa kwa kuanza kulipa, yataanza katika kifo cha marehemu, na malipo ya kwanza yatafanywa baada ya kupita kwa mwaka mmoja.

Ila wasii anaweza akalipa malipo ya awali kabla muda huo haujaisha kwa kiasi ambacho kitakuwa kimetimia wakati wa kufanya malipo hayo ya awali.

Malipo ya mwaka kama muda umepangwa

**119.** Ikiwa kuna maelekezo kuwa malipo hayo yatafanyika kwa kipindi cha robo mwaka, au kwa mwezi, malipo yatafanywa mwisho wa robo ya kwanza au mwezi wa kwanza, kama hali itakavyokuwa, baada ya kifo cha marehemu, na kama wasii akiona yafaa, yatalipwa pale muda utakapofika; lakini wasii hatabanwa kulipa mpaka mwisho wa mwaka.

Vifungu vya jumla juu ya malipo ya mwaka

**120**.-(1) Malipo ya mwaka, kama hakuna maelekezo mengine tofauti, yatajilimbikiza siku hadi siku, na kama mlipwaji wa mwaka akifa katika vipindi vya malipo, sehemu ya malipo yake yatalipwa kwa wawakilishi wake.

(2) Ikiwa kuna maelekezo kuwa malipo ya kwanza yatalipwa ndani ya mwezi mmoja au katika mgawanyo wowote wa muda baada ya kifo cha mtoa wosia, au katika siku maalumu, malipo yanayofuata yatafanywa katika maadhimisho ya siku ambapo wosia unaruhusu malipo ya kwanza yafanyike

Uwekezaji wa amana inayoruhusiwa na kanuni za uthibitisho wa wosia

**121**.-(1) Ikiwa hiba, isiyo hiba mahususi, imepewa kwa maisha, kiasi kilichorithishwa mwisho wa mwaka baada ya kifo cha mtoa wosia itawekwa katika amana kama Kanuni za Uthibitisho wa wosia zitakavyoruhusu au kuongoza, na mapato yake yatalipwa kwa waasiwa kama yatakavyokuwa yamepatikana

(2) Ikiwa hiba wazi imepewa ilipwe katika muda ujao, wasii atawekeza kiasi kinachotosheleza katika amana kama Kanuni za Uthibitisho wa Wosia zitakavyo ruhusu au kuongoza, na masilahi yatakayo patikana yatawekwa katika mapato ya mali za marehemu.

(3) Ikiwa malipo ya mwaka yametolewa na hakuna pesa za kuilipia au zilizotengwa na wosia kuilipia, kiasi kinachotosha kutoa malipo ya mwaka kitawekezwa kwa dhumuni hilo katika amana kama Kanuni za Uthibitisho zitakavyoruhusu au kuongoza.

Urithi unaotegemea tukio fulani

**122**. Ikiwa urithi unategemea kitu kitokee mbeleni ndio urithi ugawiwe wasii habanwi kuwekeza kiasi cha hiba, lakini anaweza akaihamisha mali yote iliyobaki kwa muusiwa aliyebaki (kama yupo) kama akitoa dhamana ya kutosha kulipia hiba hiyo wakati kitu hicho au muda huo ukifika

Maelekezo ya mtoa wosia juu ya uwekezaji

**123**.-(1) Ikiwa mtoa wosia amerithisha baki ya mali yake kwa mtu na kwa masiha yake yote kwa maelekezo kuwa itawekwa katika amana zilizotajwa, mali ambazo hazikuwekwa katika amana wakati wa uhai wake zitabadilishwa katika pesa na zitawekwa katika amana

(2) Mabadiliko hayo na uwekezaji utafanywa katika muda na hali kama wasii atakavyoona yafaa, na, mpaka mabadiliko hayo na uwekezaji utakapokamilika, mtu ambaye kwa muda huo angestahili pato la pesa kama uwekezaji ungeshafanyika atapata riba ya asilimia nne kwa mwaka kulingana na bei ya soko (malipo yatalipwa kama ambavyo yangetakiwa wakati wa kifo cha mtoa wosia) ya sehemu hiyo ya pesa kama bado haijawekezwa.

Watoto wanaotakiwa wapate malipo au umiliki mara moja

**124**.-(1) Ikiwa, kwa masharti ya urithi, muusia anatakiwa apate malipo au apewe pesa au kitu alichorithishwa mara moja, lakini ni mtoto na hakuna maelekezo katika wosia wa kumpa mtu yeyote kwa niaba yake, wasii au msimamizi, isipokuwa kama mali hiyo italipwa au itawekwa kwenye Muamana wa Serikali kutokana na Sheria ya Muamana wa Serikali ( Mamlaka na Majukumu), atalipa au kupeleka mali hiyo katika Mahakama ambapo uthibitisho wa wopsia, au hati ya uthibitisho wa wosia ilitolewa, kwa ajili ya muusiwa

Sura ya 33

(2) Malipo hayo katika Mahakama, yatakuwa ni malipo halali ya pesa zilizolipwa

(3) Pesa hizo, zikilipwa katika Mahakama, zitawekezwa katika ununuzi wa amana kama Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi zinavyoruhusu au kuelekeza, ambapo, riba itayopatikana, itawekwa au italipwa kwa mtu anayestahili, au vinginevyo kutumika kwa faida yake, kama Mahakama itakavyosema

(4) Ikiwa muusiwa ni kata ya Mahakama Kuu, malipo yatafanywa katika Mahakama Kuu bila kuzingatia kwamba utolewaji wa uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa wosia ulifanywa na mteule wa wilaya na bila kujali kuwa vifungu wa Sheria ya Muamana wa Serikali itatumika.

(5) Ikiwa mali inasimamiwa na msimamizi aliyeteuliwa katika SEHEMU YA VIII la Sheria hii na hiba haijalipwa au kuhamishiwa kwa Muamana wa Serikali, msimamizi atalipa au atahamisha hiba hiyo kama vifungu vya Kanuni ya Uthibitisho wa Wosia vinavyohitaji.

Utoaji wa hiba

**125**.-(1) Muusiwa wa hiba mahsusi, anatakiwa apate sehemu yake, kama lipo, baada ya kifo cha marehemu

Ila urithi mahsusi unategemea kitu au jambo litokee mbeleni ili kupata nguvu, haitahitaji, utolewaji wa mali katikati ya kifo cha mtoa wosia na wakati wa kupewa hiba: utoaji wa mali katika hali hiyo hufanya baki katika mali ya mtoa wosia

(2) Muusiwa wa mali itakayobaki atatakiwa apate mali yake kutoka kwenye mfuko wa mali baki baada ya kifo cha marehemu

Ila ikiwa mali itakayobaki urithi wake utategemeea jambo au kitu kitokee mbeleni katika masharti yake haitajumuisha kipato kinachoweza kutokana na pesa zilizorithishwa katikati ya kifo cha mtoa wosia na kukabidhiwa kwa hiba; kipato hicho hakitagawiwa

Riba ya hiba ya wazi

**126**.-(1) Ikiwa hakuna muda uliowekwa kwa malipo ya hiba ya wazi, riba itaanza kuhesabiwa baada ya mwaka mmoja ya kifo cha mtoa wosia.

Ila-

pale hiba itakapokuwa imerithishwa ili kumaliza deni, riba itaanza kuhesabiwa wakati wa kifo cha marehemu

Ikiwa kiasi kimerithishwa kwa mtoto kwa masharti ya kulipiwa kwa matunzo yake kutoka katika kiasi hicho, riba italipwa wakati wa kifo cha marehemu.

(2) Ikiwa muda umewekwa kwa malipo ya hiba ya wazi, riba italipwa katika muda uliowekwa. Riba katika muda huo itakuwa ni sehemu ya mali ya marehemu iliyobaki.

(3) Kiasi cha riba kitakuwa ni asilimia nne kwa mwaka

Riba ya malipo ya mwaka

**127**.-(1) Hakuna riba itakayolipwa katika malimbikizo ya riba katika mwaka wa kwanza baada ya kifo cha mtoa wosia, japokuwa

kipindi kifupi kabla ya kuisha kwa mwaka huo kinaweza kuwa kimewekwa na wosia kwa kulipa malipo ya kwanza ya malipo ya mwaka.

(2) Ikiwa kiasi cha pesa kimetakiwa kiwekezwe ili kupata malipo ya mwisho wa mwaka, riba ya asilimia nne italipwa kuanzia siku ya kifo cha mtoa wosia.

Baki ilipwe kwa muusiwa wa mali itakayobaki

**128.** Ziada au baki ya mali ya marehemu, baada ya kulipa madeni na wausiwa, italipwa kwa muusiwa aliyebaki kama akiwa amechaguliwa na wosia.

Kuhamisha mali kutoka Tanzania kwenda kwa wasii au msimamizi katika nchi ambayo mtoa wosia alikuwa akiishi

**129.** Ikiwa mtu hana makazi ya kudumu Tanzania amekufa na kuacha mali Tanzania na nchi ambayo alikuwa na makazi ya kudumu wakati wa kifo chake na uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi imetolewa Tanzania kuhusiana na mali zake na utolewaji wa usimamizi katika nchi aliyokuwa akiishi kuhusiana na mali zake zilizopo nchini humo, wasii au msimamizi, kama itakavyokuwa, Tanzania, baada ya kupewa notisi kama inavyotakiwa na kifungu cha 134 na baada ya kulipa madeni yote halali yaliyofikisha muda wake kama anavyoyajua, anaweza, badala ya yeye mwenye kugawa mali iliyobaki kwa watu wanaokaa nje ya Tanzania ambao wanastahili, kuhamisha, kwa ruhusa ya wasii au msimamizi, kama itakavyokuwa, katika nchi aliyokuwa akiishi marehemu, mali iliyobaki kwake kwa ajili ya ugawaji kwa watu hao.

## SEHEMU YA XIII
## URUDISHAJI WA MIRATHI

Kurudishwa kwa hiba iliyolipwa kwa agizo la Mahakama

**130**. Wasii aliyelipa mirathi kwa kuzingatia agizo la Mahakama anaruhusiwa kumuita mrithi yeyote arudishe mali kama ikitokea kuwa mali hazitoshi kuwagawia warithi wote.

Hakuna urudishwaji kama malipo yamefanyika kwa hiari

**131**. Ikiwa wasii amelipa mirathi yeye mwenyewe, hawezi akamuita muusiwa kurudisha mali kama ikiwa mali zilizopo hazitatosha kulipa wausiwa wote.

Urudishwaji pindi hiba inapofikia muda wake na uongezwaji wa muda

**132.**-(1) Ikiwa muda uliotolewa katika wosia wa kutimiza sharti umepita, bila sharti hilo kutimizwa, wasii, bila udanganyifu, akagawa mali iliyowekewa sharti hilo, katika hali hiyo, kama muda zaidi umetolewa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mtu huyo akaruhusiwa atimize sharti hilo, mali haitadaiwa kwa wasii, lakini wale ambao aliwagawia watatakiwa warudishe kiasi hicho

(2) Kama wosia ukitaka muusiwa afanye kitu kwa muda uliotolewa, aidha kama sharti la kutimizwa ili apewe urithi wake au kama sharti ambalo lisipotimizwa bali mali ya urithi itapewa kwa mtu mwingine, au urithi utakuwa haina nguvu, kitu hicho ni lazima kifanywe kwa muda uliopangwa, isipokuwa kama ufanywaji wake

utazuiliwa kwa udanganyifu, na katika hali hiyo muda wa kutimiza utaongezwa kufuatiwa udanganyifu huo.

Pindi wausiwa wanapotakiwa warudishe kwa usawa

**133**. Kama wasii amelipa mali za urithi, na baadaye anatakiwa kulipa deni ambalo hakulijua mwanzo, anaruhusiwa kuwaita wausiwa warudishe kiasi kilicho sawa.

Mgawanyo wa mali

**134**.-(1) Ikiwa wasii au msimamizi ametoa notisi kama inavyotakiwa na Kanuni za Uthibitisho wa Mirathi, kwa wadeni na wengine wamtumie madai yao dhidi ya mali ya marehemu, muda wa kuleta madai ukiisha, atakuwa huru kugawa mali, au sehemu ya mali, katika kulipa madai halali anayoyajua, na hatakuwa na hatia kwa mali zilizogawiwa kwa mtu yeyote ambaye hakujua dai lake wakati wa ugawaji

(2)Kifungu hiki hakitazuia mdai au mlalamikaji yeyote kufuata mali, au sehemu ya mali, zilizopo kwa mtu aliyepokea mali hizo.

Pale ambapo wadai watamuita muusiwa arudishe

**135**. Mdai ambaye hajapokea malipo yake anaweza akamuita muusiwa ambaye amepokea mali arudishe, ikiwa kama mali za marehemu zilitosha ama hazikutosha wakati wa kifo chake kulipa madeni pamoja na warithi, na ikiwa kama malipo yalifanywa na wasii mwenyewe au la.

Haki ya wausiwa kuwataka wausiwa wengine warudishe

**136**.-(1) Ikiwa mali zilikuwa zinatosha kuwagawia wausiwa wote wakati wa kifo cha mtoa wosia muusiwa ambaye hajapokea urithi wake au ambaye ametakiwa arudishe, katika kifungu cha 135, hawezi akamtaka muusiwa ambaye amepokea mali yake kurudisha, ikiwa mali ililipwa kwake katika shitaka au la, hata kama mali zimekuwa chache kwa upotevu uliofanywa na wasii.

(2) Kama mali zilikuwa hazitoshi kuwalipa wausiwa wote wakati wa kifo cha mtoa wosia, muusiwa ambaye hajapokea urithi wake lazima, kabla hajamuita muusiwa yeyote kurudisha, amwendee wasii kama bado ana mali; lakini kama wasii hana mali au hatakiwi kulipa, muusiwa ambaye hajaridhika atawataka wausiwa wote walioridhika warudishe kwa usawa

(3) Urudishaji wa muusiwa mmoja kwenda kwa mwingine hautazidi kiasi ambacho mali ingetakiwa ipunguzwe kama mali zingegawiwa ipasavyo

Marudisho hayana riba

**137**. Urudishaji wa mali, hautakuwa na riba.

## SEHEMU YA XIV
## UHARIBIFU NA UFUJAJI WA MALI

Mashitaka kwa ufujaji

**138.** Pale wasii au msimamizi atatumia vibaya mali za marehemu, au akaiweka katika hatari ya kupotea au kuharibika, atapaswa kulipa hasara hiyo au uharibifu huo uliojitokeza

Mashitaka kwa kutojali

**139.** Pale wasii au msimamizi anasababisha hasara katika mali kwa kukataa kuwa sehemu ya mali ya marehemu, atapaswa kulipa fidia.

## SEHEMU YA XV
## USIMAMIZI WA MALI YA WAKFU
[R.L. Sura ya 326]

Tafsiri

**140**. Katika SEHEMU hii, isipokuwa kama maana itahitaji-

"kamishna" inamaanisha mwanachama wa Tume ya Wakfu aliyechaguliwa katika kifungu cha 142 cha Sheria hii.

"Muamana/kabidhi" inajumuisha mtu yeyote, aidha peke yake au pamoja na mwingine, anayesimamia kitu chochote sambamba na wakfu au kupokea kodi au fidia

"Wakfu" ina maanisha tunu au kujitoa katika Sheria za Kiislamu katika kitu chochote ndani ya Tanzania kwa ajili ya dini, neema au tunu kwa dhumuni au kwa matunzo na msaada kwa mtu yoyote wa familia ya mtu aliyepewa kitu hicho

"Tume ya Wakfu" ina maanisha Tume wa wakfu ya Tanzania iliyowekwa katika kifungu cha 142 ya Sheria hii.

Wakfu kuwa halali na wenye nguvu
Sura ya 114

**141**. Bila kujali vifungu katika Sheria ya ardhi na uhalalishwajina Sheria yeyote inayohusika Tanzania, mtu yeyote aliyeweka wakfu baada ya tarehe ambapo Sheria hii itaanza kutumika, kwa kutumia vifungu vya Sheria zilizotajwa na Sheria zilizotumika, wakfu utakuwa madhubuti na halali, hautakuwa kinyume na Sheria, dhoofu au batili na vifungu vyovyote vya Sheria iliyosemwa au Sheria inayotumika ambayo itaufanya wakfu huo uwe dhoofu au batili havitakuwa na nguvu.

Kuanzishwa kwa Tume ya Wakfu

**142**.-(1) Kinaanzishwa chombo kitakachojulikana na Tume ya Wakfu Tanzania

(2) Tume ya Wakfu itajumuisha watu wasiopungua nane watakao chaguliwa na Rais ambapo watu wasio pungua watano watakuwa Waislamu.

(3) Rais atamchagua mwenyekiti na katibu kutoka katika wanachama wa Tume ya Wakfu.

(4) Wanachana wa Tume ya Wakfu wataitumikia ofisi kwa kipindi chote Rais atakapokuwa madarakani

(5) Hakuna mwenendo au kitendo chochote cha Tume ya Wakfu kitakachobatilishwa kwa sababu ya kuwepo kwa upungufu wa wanachama wakati wa mwenendo huo au kitendo hicho.

Tume ya Wakfu itakuwa ni mamlaka inayojitegemea na itakuwa na muhuri

**143**.-(1) Tume ya Wakfu itakuwa ni kampuni, ambayo ina maisha ya muendelelezo, na mhuri wa moto na yenye mamlaka ya kupata, kumiliki au kujipatia mali aidha inayohamishika, au isiyo hamishika, na itakuwa na mamlaka yote, majukumu na kazi kama zitakavyokuwa zimewekwa na Sheria hii

(2) Tume ya Wakfu inaweza ikashitaki au kushitakiwa kwa jina la kampuni na inaweza kwa madhumuni yote kutajwa kwa jina hilo.

(3) Mhuri wa Tume ya Wakfu, ambavyo utakuwa wa namna

kama ambavyo Rais atathibitisha, itathibitishwa na saini ya mwenyekiti, au kamishna ambaye siye katibu aliyeruhusiwa kumwakilisha, na katibu, na mhuri huo utajulikana kiofisi na kimahakama.

(4) Nyaraka zote (zaidi ya zile zinazohusika na ardhi ambazo zitathibitishwa na mhuri wa moto wa Tume ya Wakfu) zinazotengenezwa, na maamuzi yote ya, Tume ya Wakfu yanaweza yakathibitishwa kwa mkono wa mwenyekiti, na kamishina aliye thibitishwa kumwakilisha, au katibu.

Mikutano na akidi

**144**.-(1) Tume ya Wakfu itafanya mkutano japo mara moja katika kila miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti ataongoza mikutano yote ya Tume ya Wakfu ambayo atakuwapo na kama asipokuwapo katika mkutano, makamishna waliopo watamchagua kamishna aongoze mkutano.

(3) Akidi ya Tume ya Wakfu itakuwa watu wanne ambao mmoja atakuwa aidha mwenyekiti au katibu.

Masijala ya mali za wakfu na amana Agizo namba 9 la 1956

**145.**-(1) Waziri anaweza kutoka kipindi fulani hadi kingine kwa kutumia notisi katika gazeti kuagiza kuwa kifungu hiki kitatumika katika sehemu yoyote Tanzania iliyoelezwa katika maelekezo hayo, na ikiwa hivyo kifungu hiki kitatumika kama inavyoelezwa

(2) Kama maelekezo yametolewa, kama inavyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha sehemu hii sehemu hii itatumika katika wakfu zifuatazo (ambazo zitajulikana kama wakfu zilizosajiliwa), na hii ni kusema kwamba-

(c) Wakfu yoyote ambayo mali yote au sehemu ya mali inajumuisha mali isiyohamishika, yote au sehemu iliyo katika sehemu yote au kipande cha sehemu ambapo kifungu hiki kimetumika; na

(d) Wakfu yeyote ambayo wadhamini wanakaa katika eneo ambalo kifungu hiki kimetumika

(3) Aidha wakfu imekuwa wakfu iliyosajiliwa, itaendelea kama wakfu iliyosajiliwa bila kujali mabadiliko yoyote katika hali ya kitu kilichomo, au hali iliyopo, au badiliko katika hali ya kawaida ya wadhamini hao;

(4) Tume ya Wakfu itaweka, maelezo kama itakavyoelezwa, orodha ya mali zote zilizo chini ya wakfu iliyosajiliwa pamoja wadhamini wote wa mali hiyo.

(5) Kila mdhamini wa mali iliyopo chini ya wakfu iliyosajiliwa, ndani ya miezi mitatu ya tarehe ambapo itakuwa ni wakfu iliyosajiliwa, ataiomba Tume ya Wakfu kuisajili wakfu hiyo, na maombi hayo yatakuwa katika fomu, na yatajumuisha maelezo yote na yataambatana na malipo yote yanayotakiwa.

(6) Kila mdhamini wa mali iliyoko chini ya wakfu iliyo sajiliwa, ndani ya miezi mitatu tangu iwe wakfu iliyosajiliwa au tangu awe mdhamini, ataomba tume ya wakfu asajiliwe, na maombi hayo yatakuwa katika fomu na yataambatanishwa na ada inayotakiwa.

(7) Ikiwa mtu ameacha kuwa mdhamini wa mali iliyoko chini ya wakfu iliyosajiliwa mtu huyo, ndani ya mwezi mmoja kabla hajaacha kuwa mdhamini, ataitaarifu tume ya wakfu kuwa anaacha kuwa mdhamini, na atajulikana kama mdhamini mpaka tume ya wakfu itakapojulishwa:

Isipokuwa-

(c) mtu huyo amecha kuwa mdhamini kwa sababu ya kifo chake, mtu aliyemrithi udhamini atatoa taarifa zinazohitajika katika hiki kifungu kidogo;

(d) Ikiwa kuna mdhamini zaidi ya mmoja wa mali iliyo chini ya wakfu iliyosajiliwa, taarifa inayohitajika katika kifungu hiki kidogo itatolewa na mdhamini aliyebakia.

(8) Katibu wa Tume ya wakfu, kwa cheti kitakachotolewa na kilichotiwa saini na yeye, atajulisha kila badiliko litakalofanyika katika wadhamini wa mali iliyo chini ya wakfu iliyosajiliwa-

Sura ya 334

(c) katika suala la mali inayohusiana na ardhi iliyosajiliwa katika Sheria ya Usajili wa Ardhi, au Sheria yoyote itakayo irekebisha au itakayokuja badala ya hiyo kwa msajili wa hati;

(d) kuhusu mali nyingine yoyote inayohusu ardhi ambayo haijasajiliwa, kwa msajili wa nyaraka,

Na kila hati husika itaeleza kinagaubaga ardhi inayohusika

(9) Ada zote zilizoelezwa katika jedwali la tano la Sheria hii, ambayo ni ya usajili au mali, zilizopo chini ya wakfu iliyosajiliwa na kwa ajili ya usajili wa wadhamini zitatozwa na Tume ya wakfu na kuwekwa katika mfuko utakaoitwa Mfuko wa Usimamizi.

(10) Mdhamini yoyote ambaye, bila sababu za kuaminika, akishindwa kutekeleza maelezo ya vifungu vidogo vya (2) au (3) vya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai katika Sheria hii

Tume ya Wakfu inaweza kufanya uchunguzi na kuchukua usimamizi wa wakfu

**146**.-(1) Ikitokea katika Tume ya wakfu kuwa-

(d) hakuna mdhamini wa wakfu aliyewekwa; au

(e) mdhamini yeyote ambaye amefanya au anafanya katika hali ambayo si sahihi, haijaruhusiwa au si halali; au

(f) badiliko katika usimamizi wa wakfu ni muhimu kwa ajili ya wakfu hiyo,

Tume ya Wakfu inaweza, kwa uamuzi wake yenyewe, au uamuzi wa mtu yeyote aliye na maslahi na wakfu hiyo, kufanya uchunguzi. Notisi ya uchunguzi huo itatolewa, kwa namna ambayo inakuwa inatakiwa, kwa watu wote wenye masilahi na wakfu na watu hao wataalikwa kwa notisi hiyo ili waje kutoa ushahidi mbele ya tume ya wakfu

(2) Baada ya kufanya uchunguzi huo, tume ya wakfu ikigundua kuwa hakuna mdhamini wa wakfu, au mdhamini yeyoye amefanya au anafanya katika hali ambayo si sahihi, haijaruhusiwa, au si ya kihalali, au mabadiliko katika usimamizi wa wakfu utakuwa wa faida katika

wakfu, tume ya wakfu itatoa agizo aidha mali iliyoko chini ya wakfu itasimamiwa na wakfu tume au kumchagua mtu au watu awe/ wawe mdhamini/wadhamini wa wakfu na agizo hilo litasema mali ambayo inahusika.

(3) Baada ya kutoa agizo katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki-

(c) kutangaza kuwa mali iliyochini ya wakfu itasimamiwa na tume ya wakfu, mali hiyo itakuwa sambamba na Sheria yoyote inayohusika na usajili wa ardhi kwa muda itakayo kuwa na nguvu, itawekwa chini ya tume ya wakfu;

(d) kumchagua mdhamini mpya au wadhamini wa wakfu, mali iliyo chini ya wakfu itaenda sambamba na Sheria yoyote inayohusiana na usajili wa ardhi kwa muda itakaokuwa na nguvu, kuwa chini ya msimamizi au wasimamizi wapya.

Isipokuwa maelezo ya kifungu kidogo hakitatumika katika hali ambayo agizo lililowekwa na tume ya wakfu limebadilishwa katika rufaa katika kipengele kidogo cha (5) cha kifungu hiki.

Sura ya 334

(4) Katibu wa tume ya wakfu atatuma nakala iliyothibitishwa na saini yake ya agizo lolote katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kwa msajili wa hati ikiwa agizo linahusu ardhi yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa ardhi au Sheria yoyote itakayobadilisha, au kuja badala yake na msajili wa nyaraka kama agizo litahusu ardhi yoyote ambayo haijasajiliwa.

(5) Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na agizo la tume ya wakfu katika kifungu hiki anaweza akakata rufaa katika baraza la rufaa, litakalo chaguliwa na Rais kwa ajili hiyo, kuwezesha kusikilizwa kwa suala hilo na baraza la rufaa, na uamuzi wa baraza la rufaa utakuwa wa mwisho na wenye hitimisho

(6) Mtu yeyote anayekata rufaa katika baraza la rufaa katika kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki atakuwa na haki ya kutokea au kuwakilishwa na wakili mbele ya baraza la hukumu katika usikilizwaji wa rufaa hiyo.

Wadhamini wa wakfu wanaweza wakaitwa kutoa ushahidi wa usimamizi mzuri wa amana

**147**.-(1) Tume ya wakfu wakati wowote itamuita mdhamini wa mali ya wakfu kuja kuiridhisha kama mali inasimamiwa vizuri na inaweza ikamuhitaji mdhamini atoe nyaraka au vitabu, aidha vya mahesabu au vinginevyo, anavyovimiliki au vilivyoko chini ya ulinzi wake vinavyohusu mali hiyo.

(2) Mdhamini yeyote atakayeshindwa kutimiza kigezo cha kutoa nyaraka au vitabu alivyonavyo au vilivyoko katika himaya yake kama inavyotakiwa na tume ya wakfu katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai tofauti kinyume na Sheria hii.

Mikataba na

**148.** .Hakuna mkataba au makubaliano ya aina yoyote

makubaliano Fulani yanayohusu wakfu lazima isibitishwe na tume ya wakfu

yanayohusu kuuza au vinginevyo kuchukua kitu chochote kilichopo chini ya wakfu au kutaka kuweka rehani kitu hicho au kutaka kupangisha kitu hicho kwa muda unaozidi mwaka mmoja utakuwa na nguvu isipokuwa ruhusa ya maandishi kutoka katika tume ya wakfu kutolewa kwanza.

Mali ya wakfu haitapatikana kwa maagizo au kwa kabidhi pingamizi baada ya kuanza kwa sehemu hii

**149.** Bila kuathiri kitu chochote tofauti na Sheria hii au Sheria itakayo kuwa na nguvu kwa muda huo, hakuna hati ya mali yoyote iliyopo chini ya wakfu, baada ya kuanzishwa kwa sehemu hii, itachukuliwa na mtu yeyote kwa sababu ya pingamizi au kwa sababu yoyote Sheria ya maagizo.

Namna mali ya wakfu itakavyosimamiwa

**150**.-(1) Sambamba na kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki mali zote zilizo chini ya wakfu ambazo zinasimamiwa na wakfu tume zitasimamiwa kwa kuzingatia nia ya muwekaji wa wakfu kama nia hizo ni halali katika Sheria za Kiislamu na zinaweza kufanikishwa, na ikiwa nia hizo zinaweza zikathibitishwa kwa kuangalia mila au ushahidi wowote unaopatikana kihalali.

(2):Katika hali ambayo katika wazo la tume ya wakfu, nia ya mtoa wakfu si halali, au haithibitiki au haiwezi kutimilika au kama mapato ya ziada yamebaki baada ya kutimiza nia ya mtoa wakfu, tume ya wakfu itatumia mali iliyo chini wa wakfu au mali ya ziada au mapato hayo, kwa ajili ya dini, tunu au kwa dhumuni la msaada kwa ajili ya Waislamu kama tume ya wakfu itakavyoona ni sawa.
Ila haitakuwa halali kwa tume ya wakfu kutumia mali yoyote, au mali ya ziada, au mapato katika hiki kifungu kidogo kwa dhumuni linalohusiana na wakfu nyingine kwa sababu tu kuna mali yoyote katika wakfu hiyo ya kwanza

Tume ya Wakfu inaweza ikauza mali ya wakfu katika hali Fulani

**151.** Kama itaonekana kwa tume ya wakfu kuwa nia yoyote ya mtoaji haitaweza kufanikishwa na kwamba ni vema kuwa mali au sehemu ya mali iliyowekwa chini ya wakfu ipangishwe, kubadilishwa au kuuzwa, tume ya wakfu itafanikisha mali hiyo au sehemu yake kupangisha, kubadilishwa au kuuzwa kama inavyotakiwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 150 cha Sheria hii.

Ruhusa inatakiwa kujenga au kuanzisha makaburi

**152.**-(1) Hakuna mtu ambaye ametoa mali kama wakfu au mdhamini wa kitu hicho atajenga au atasababisha kujengwa kwa msikiti au ataanzisha au kusababisha kuanzishwa kwa makaburi isipokuwa, kabla ya hapo amepata ruhusa ya tume ya wakfu kwa niaba hiyo, na ameiridhisha tume ya wakfu kuwa msikiti huo au makaburi hayo yametunikiwa au yatatunikiwa kwa hali inayoridhisha kwa utunzwaji wake na kuyaweka katika hali nzuri.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutimiza maelezo ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai tofauti na Sheria hii.

Ada

**153**.-(1) Kama mali yoyote ambayo iko chini wa wakfu inasimamiwa na tume ya wakfu, itatozwa ada kama itavyokuwa

inatakiwa

(2) Pesa zinazopatikana kutoka kwenye ada hizo zitatumiwa na tume ya wakfu katika shughuli za kila siku za Tume ya Wakfu.

(3) Kama baada ya miezi kumi na mbili ada hiyo itazidi matumizi ya kila siku ya tume ya wakfu, ziada itapewa kwa mfuko wa msaada wa tume ya wakfu.

(4) Mfuko wa msaada wa Tume ya Wakfu utatumia pesa hizo kwa ajili ya kutoa misaada kama tume ya wakfu itakavyoona inafaa.

Hesabu na Ukaguzi wa mahesabu

**154**. Tume ya Wakfu inaweka mahesabu sawa ya mali zote na pesa zinazopokelewa na mahesabu yatakaguliwa na mkaguzi aliyethibitishwa na rais kwa muda huo kama waziri atakavyoongoza.

Akaunti za benki

**155.** Tume ya Wakfu itafunguaa akaunti ya benki au hesabu za kibenki ambayo pesa zote zinazopokelewa na tume ya wakfu zitawekwa na pesa zote zitakazothibitishwa na tume ya wakfu zitatolewa. Akaunti hizo zitakuwa zinatunzwa na mwenyekiti, au kamishna aliyethibitishwa kwa niaba ya tume ya wakfu, na katibu

Sheria ya zuio la kodi haitatumika katika mali ya wakfu (Sura ya 339)

**156**. Vifungu vya sheria ya zuio la kodi, au sheria yoyote itakayoirekebisha au kuibadilisha, haitatumika katika mali yoyote ya wakfu ambayo inasimamiwa na tume ya wakfu kwa kufuatana na vifungu vya sheria hii

Adhabu

**157**. Mtu yeyote atakayefanya kosa katika Sheria hii akipatikana na hatia atatakiwa kulipa fidia isiyozidi shilingi elfu mbili tu au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote fidia na kifungo.

Kanuni

**158**.-(1) Waziri ataweka kanuni kwa kanuni zote au kwa dhumuni hili-

(e) Kuweka mwenendo utakaofuatwa na tume ya wakfu katika ufanyaji wa kazi zake, majukumu na kazi katika vifungu vya Sheria hii, ikijumuishwa na ukaimu wa majukumu, kazi na mamlaka au moja kati ya hizo, zaidi ya zile zilizotajwa katika kifungu cha 146, kwa mtu yeyote au watu.

(f) Kuweka muda na namna ya kukata rufaa katika mabaraza ya rufaa, ada itayotakiwa kulipwa, na mwenendo mzima utakao fuatwa katika rufaa hiyo;

(g) Kuwa kitu chochote kinachotakiwa kuwekwa katika viungu vya Sheria hii;

(h) Kwa ujumla wake, katika kuvitekeleza vizuri vifungu vya Sheria hii

(2) Kanuni zitakazotengenezwa na kifungu hiki kitatoa kuhusiana na uvunjifu wa vifungu vyake, fidia ambayo haitazidi fidia iliyowekwa katika kifungu cha 157 cha Sheria hii.

## SEHEMU YA XVI
## MALI ZA KIISLAM (MALIPO YA SADAKA)

Busara ya Afisa wa Wilaya kufanya malipo

**159**. Katika hali yoyote ambapo, katika Sheria za Kiislamu, mali yote au sehemu yake inalipwa katika hazina (Beit-el-Mal), afisa wa wilaya anaweza, kwa busara yake , kuagiza kuwa mali yote au sehemu ya kiasi cha mali kilipwe lakini kisizidi shilingi elfu moja, itakayogawiwa, kwa usawa kama atakavyoona inafaa, baina ya mume, mke au wake, au wategemezi wengine wa marehemu.

Ila ikiwa mali ni ya aina ambayo Sheria hii inatumika, afisa wa wilaya hatatoa agizo katika kifungu hiki bila kuwa na ruhusa ya Mahakama ambayo ina mamlaka katika usimamizi wa mali au, kama mali inasimamiwa na kabidhi-wasii

## SEHEMU YA XVII
## MENGINEYO

Vifungu vinavyotumika kwa msimamimizi aliyeambatanishia wasii

**160**. Katika sehemu ya XII na XIII vifungu vinavyomhusu wasii vitatumika pia kwa msimamizi aliyembatanishwa na wosia.

Matunzo ya wosia wa watu walio hai

**161**. Sambamba na vifungu vya kanuni za uthibitisho wa mirathi, wosia wa mtu aliye hai unaweza ukatunzwa katika masijala ya Mahakama Kuu, na kila wosia uliotunzwa utahifadhiwa katika masijala chini ya uangalizi na maelekezo ya Mahakama Kuu.

Hati ya kiapo kama ni shirika la amana

**162**. Afisa yeyote aliyethibitishwa kwa dhumuni na shirika la amana au mkurugenzi au mwanachama wa serikali anaweza, kwa niaba ya shirika, kuchukua kiapo, kuapa katika hati ya kiapo, kutoa dhamana au kufanya kitu chochote au kitu ambacho Mahakama itahitaji kwa ajili ya kuipa shirika uthibitisho wa wosia au usimamizi, na vitendo vya afisa aliyethibitishwa, mkurugenzi au mwanachama, vitaibana shirika hilo

Uhalali wa ugawaji katika wosia na haki ya matunzo

**163.** Hakuna kitu katika Sheria hii kitakacho-

(d) halalisha mirathi yoyote ambayo vinginevyo ingekuwa ni batili

(e) itabatilisha ugawaji wowote ambao vinginevyo ungekuwa wa halali; au

(f) Kumnyima mtu yeyote haki yoyote ya matunzo ambapo vinginevyo angepewa.

Marekebisho

**164.** [Marekebisho ya baadhi ya Sheria]

Sheria Fulani kutotumika

**165**.-(1) Sheria zilizotolewa kama sehemu ya kwanza ya jedwali la kwanza hazitatumika Tanzania kwa kiasi kilichoelezwa katika safu ya nne ya jedwali hilo

(2) [Kufutwa kwa baadhi ya Sheria]

**166**.-(1) Muendelezo wa Sheria zinazohusu utolewaji wa

Mabakisho

uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi, uchaguzi wa wasimamizi na usimamizi wa mali hautaathiriwa kwa kufutwa au kutotumika kwa ingizo lolote au kutotumika kwa vifungu vya jedwali la kwanza na la pili, na kama kuna ombi limefanywa la utoaji au uchaguzi katika ingizo hilo au vifungu au usimamizi wa mali yoyote umeanza, utaendelea kwa kufuata vifungu vya Sheria hii.

Sura ya 28

Sura ya 30

(2) Matoleo yote ya uthibitisho wa wosia na hati za usimamizi yaliyofanywa Tanzania chini ya Sheria ya Mirathi ya India , 1865, au Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi ya India, 1881, kila uchaguzi wa wasimamizi katika sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache), kila usajili wa mirathi katika sheria ya Uthibitisho wa Wosia (Kupiga tena Mhuri) na kila agizo na maelekezo yaliyotolewa na Mahakama yenye mamlaka Tanzania chini ya Sheria zilizotajwa yatakuwa na nguvu kama vile yalifanywa katika vifungu vinavyohusika na Sheria hii, lakini bila kuathiri ujumla wa yaliyosemwa, uchaguzi wa msimamizi wa marehemu aliyekuwa mwafrika chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache) utakuwa na nguvu bila kujalisha kama thamani ya mali inazidi thamani ile ya mali chache.

(3) Bila kujalisha ufutwaji au kutotumika kwa Sheria yoyote au vifungu vyovyote vilivyopo katika jedwali la pili na la tatu-

Supp.58

Sura ya 28
Ukurasa wa 6
Supp.57

Sura ya 30
p.10
R.L.Cap.315
Sura ya 315

(g) uchaguzi wa mteule wa wilaya;
(h) kanuni za usajili wa mirathi
(i) kanuni za usimamizi wa mali chache
(j) agizo au muongozo uliotolewa katika kifungu cha 17 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Mali Chache)
(k) Sheria ya Usimamizi wa Mali Chache
(l) Ruhusa iliyotolewa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi kwa Mashirika

Vitasemekana vimefanyika, vimetolewa au vimepewa, kama hali itakavyokuwa, katika vifungu sahihi vya Sheria hii

Vifungu vya mpito

**167**.-(1) Kama amana zimesajiliwa kwa jina la kundi la watu au mashirika.kwa niaba ya shirika la amana au ardhi au dhamana ambayo imesajiliwa kwa jina la kundi la watu au mashirika.amana hizo, ardhi au dhamana zitahamishwa kutoka kwenye kundi hilo la watu au mashirika .kwenda kwenye shirika au kama shirika litakavyoagiza

Ila hakuna hamisho litakalochukuliwa kama ni uvunjwaji wa maagano au sharti la kutochukua au litakalopelekea kunyang'anywa

(2) Ikiwa maombi yamefanywa katika Mahakama Kuu katika sehemu hii ya kusajili mirathi au hati za usimamizi katika sehemu ya X kuhusu mali za mtu aliyekufa kabla ya tarehe 20, oktoba, 1959 Mahakama Kuu kabla ya kusajili itajiridhisha kuwa kodi ya mirathi

imelipwa au dhamana juu ya malipo yake yametolewa kwa kamishina wa kodi za mirathi kama inavyotakiwa na kodi za mirathi Tanzania.
Ila kifungu hiki kidogo hakitatumika ikiwa maombi yanafanywa na au kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu

(3) Ikiwa mtoa wosia amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni na amerithisha mali ambayo itatoa riba chini ya vifungu vya sheria hii isipokuwa kifungu namba 130 au 312, ya Sheria ya Mirathi ya India ya mwaka 1865 kisha bila kujali kifungu cha 126 cha sheria hii vifungu vya Sheria hii vitaendelea kutumika.

(4) Ikiwa mtu ambaye mali zake zinasimamiwa chini ya vifungu vya mali hii, amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni, maneno ya aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 109 cha Sheria hii yatasomwa kana kwamba maneno "miezi mitatu" yamebadilishwa na maneno "miezi minne"

(5) Ikiwa mtu, mali zake, zinasimamiwa kufuatana na vipengele vya Sheria hii, amekufa kabla ya Sheria hii haijaingia nguvuni, na riba yoyote imelipwa chini ya vifungu vya 132,126 au 127 vya Sheria hii kwa kipindi baada ya tarehe hiyo, riba hiyo italipwa kwa kiasi kinachotajwa na Sheria hii katika tarehe hiyo.

Kubaki kwa mamlaka ya kabidhi wasii- muamana wa serikali
Sura ya 27
Sura ya 31

**168.** Sambamba na kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 124, hakuna kitu chochote katika Sheria hii kitatafsiriwa kukataza vifungu vya Sheria ya Kabidhi Wasii (Mamlaka na Kazi) au Sheria ya Muamana wa Serikali (Mamlaka na Kazi) au kuathiri haki, majukumu au upendeleo wa kabidhi wasii au muamana wa serikali au msaidizi wa kabidhi wasii.

## JEDWALI LA KWANZA

### NCHI AMBAZO KATIKA KIFUNGU CHA 7 KITATUMIKA

(Kifungu cha 7(6))

Muungano wan chi za Amerika
Jamhuri ya watu wa Italia
Jamhuri ya watu wa Ufaransa
Muungano wa nchi za Mexico
Shirikisho la Jamuhuri ya watu wa Ujerumani
Ufalme wa nchi za Norway
Ufalme wa nchi za Misri.
Ufalme wa Swideni

## JEDWALI LA PILI

(Kifungu cha 16 (6))
[ Imefutwa .]

R. L. Cap. 445 s.141
Sura ya 445 kifungu 141

## JEDWALI LA TATU

### SHERIA ZILIZOFUTWA

### SEHEMU YA I

| Mwaka | Namba. | JINA | kiasi kilichofutwa |
|---|---|---|---|
| 1865 | X | Sheria ya Mirathi ya India | sehemu ya XXIX mpaka XL (kwa pamoja) na kifungu cha 333. |
| 1881 | V | Sheria ya kihindi ya uthibitisho wa wosia na usimamizi | Sheria yote. |

SEHEMU YA II

[Imefutwa ]

JEDWALI LA NNE

UCHAGUZI WA MSIMAMIZI WA MALI CHACHE

SHERIA YA WOSIA NA USIMAMIZI WA MIRATHI (SURA YA 352)

(Kifungu cha 6)

Katika Mahakama ya ..........................................................................................
Usimamizi wa mirathi wa ………………………………………………………….
Leo..........................................siku ya..........................20…………………
nilichaguliwa kuwa msimamizi wa mirathi ( au wa mali zilizotajwa hapa chini) za marehemu aliyefariki katika ............................siku ya....................20................
Nitasimamia mali za marehemu vizuri na kwa uaminifu kama inavyoonyesha hapa chini.
(nakala ya wosia wa marehemu umeambatanishwa na mali itasimamiwa kama inavyotakiwa)

....................................................
*(Sahihi na cheo cha afisa wa Mahakama)*

Mimi (sisi) tunaapa na kusema kuwa mimi( sisi) nita/tutasimamia vizuri na kwa uaminifu mali za marehemu aliyetajwa, kwa kulipa madeni yake yaliyofikia muda, na kugawanya baki ya mali hiyo kama Sheria inavyosema, na nita(tuta) tunza hesabu za kweli za shughuli zote zinazohusu mali hiyo na kuzitoa mbele ya Mahakama muda wowote zinapotakiwa.
Leo......................siku ya....................20.........................

................................................
(Sahihi ya msimamizi)

## JEDWALI LA TANO

## KIWANGO CHA KODI YA MIRATHI

(Kifungu cha145)

Sheria namba 23 ya 1971; 3 ya 1979; 10 ya 1987; 15 ya 1990

| Thamani ya mali | Kiwango cha kodi |
|---|---|
| (a) Isiyozidi sh.2,000,000/= | - |
| (b) Inayozidi sh. 2,000,000/= lakini haizidi shs 2,100,000 | Shs. 11,970/= na 9% ya kiasi kinachozidi shs 2,000,000 |
| (c) Inayozidi shs 2,100,000/= lakini haizidi shs. 3,300,000/= | Shs. 11,970/= na 18% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,100,000/= |
| (d) Inazidi shs 2,300,000/= lakini haizidi shs. shs 2,700,000 | Shs. 47,975/= na 27% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,300,000/= |
| (e) Inazidi shs 2,700,000/= lakini haizidi shs. 3, 100,000 | Shs. 155,970/= na 36% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,700,000/= |
| (f) Inazidi shs 3,100,000/= lakini haizidi shs. 3, 500,000 | Shs. 299,970/= na 54% ya kiasi kinachozidi Shs. 3,100,000/= |

## KIWANGO CHA KODI YA MIRATHI

(Kifungu cha145)

Sheria namba 23 ya 1971; 3 ya 1979; 10 ya 1987; 15 ya 1990

| Thamani ya mali | Kiwango cha kodi |
|---|---|
| (g) Isiyozidi sh.2,000,000/= | - |
| (h) Inayozidi sh. 2,000,000/= lakini haizidi shs 2,100,000 | Shs. 11,970/= na 9% ya kiasi kinachozidi shs 2,000,000 |
| (i) Inayozidi shs 2,100,000/= lakini haizidi shs. 3,300,000/= | Shs. 11,970/= na 18% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,100,000/= |
| (j) Inazidi shs 2,300,000/= lakini haizidi shs. shs 2,700,000 | Shs. 47,975/= na 27% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,300,000/= |
| (k) Inazidi shs 2,700,000/= lakini haizidi shs. 3, 100,000 | Shs. 155,970/= na 36% ya kiasi kinachozidi Shs. 2,700,000/= |
| (l) Inazidi shs 3,100,000/= lakini haizidi shs. 3, 500,000 | Shs. 299,970/= na 54% ya kiasi kinachozidi Shs. 3,100,000/= |